

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA SABA**

**Kikao cha Arobaini na Nne – Tarehe 8 Juni, 2017**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Kikao cha Arobaini na Nne cha Mkutano wetu wa Saba. Karibuni sana, leo ni siku maalum na tuna mambo mengi kwa hiyo nitaomba ushirikiano wetu. Pia niwatangazie na mimi nina kiti kipya sasa kinachoashiria mwanzo mpya, chekundu kama cha kwenu, Katibu. *(Makofi/Kicheko)*

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**HATI KUWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI FEDHA NA MIPANGO:**

Taarifa ya Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Muhtasari wa Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2017/2018 *(Monitoring Policy Statement for the Year 2017/2018)*.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI – KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**SPIKA:** Swali la Kwanza kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mheshimiwa Maina Hamad Abdallah.

Na. 360

**Fedha zilizokusanywa na Halmashauri**

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH** aliluliza:-

Je, ni lini Serikali itaamua kurudisha fedha zilizokusanywa na Halmashauri kupitia vyanzo vyake vya ndani ili ziweze kutekeleza majukumu yake na mikakati iliyopangwa kwa ufanisi?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa George Simbachawene tafadhali.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Maida Hamad Abdallah, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Serikali za Mitaa zinakusanya mapato kupitia vyanzo vyake vya ndani kwa mujibu wa Sheria na Fedha za Serikali za Mitaa, Sura ya 290, kifungu cha 6, 7, 8 na 9. Ukusanyaji wa mapato hayo unasimamiwa na Sheria Ndogo zinazofafanua sheria mbalimbali za kodi zinazopaswa kukusanywa na mamlaka hizo.

Mheshimiwa Spika, mapato ya ndani yanayokusanywa na Halmashauri hutumika kwa shughuli za maendeleo na uendeshaji wa Halmashauri kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na Halmashauri zenyewe kwa kuainishwa katika mipango na bajeti zao za kila mwaka. Jukumu la Serikali Kuu ni kuidhinisha mapato na matumizi ya fedha hizo, kusimamia na kudhibiti matumizi ili kuhakikisha yanazingatia sheria na taratibu za fedha zilizowekwa na kuhakikisha zinatumiwa kwa madhumuni ya kuwaletea maendeleo wananchi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Spika, utaratibu wa kukusanya mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuwasilisha Serikali Kuu na kisha kuzirejesha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa haupo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Maida nilikuona.

**MHE. MAIDA HAMAD ABDALLAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii, ninayo maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwa kuwa kama alivyokwisha sema Mheshimiwa Waziri kwamba mapato ya Halmashauri ndiyo vyanzo vikuu vinavyoendeleza maendeleo katika Halmashauri. Kwa kuwa makusanyo yanayotokana na mapato na kodi ya ardhi na majengo urejeshaji wake kutoka katika mamlaka husika umekuwa ukisuasua huku Halmashauri zikiwa zimejipangia majukumu mbalimbali na hivyo utekelezaji wake kuchelewa. Je, Serikali haioni kwamba mtindo huu unaathiri utekelezaji wa haraka wa vipaumbele ilivyojipangia Halmashauri? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa ndani ya Halmashauri zetu kwa mujibu wa sheria wametakiwa kutekeleza agizo la kuwawezesha wanawake na vijana kwa kutenga asilimia 10 ili ziwaendeleze kiuchumi. Kwa kuwa changamoto hii imekuwa ikiathiri sana agizo hili, je, Serikali sasa ipo tayari kuleta waraka Bungeni wa mapendekezo ya kwamba mapato yanatokana na kodi za ardhi na majengo

baada ya makusanyo zibaki kwenye Halmashauri husika?  
(Makofi)

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa George Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kodi za ardhi na majengo zinakusanywa kwa sehemu, kwa mfano, kodi ya ardhi inakusanywa na kupelekwa Wizara ya Ardhi na baadaye kupelekwa Hazina na hupaswa kurejeshwa kwenye Halmashauri zetu asilimia 30. Urejeshaji huu haujawa mzuri kwa muda sasa, lakini katika bajeti ya mwaka huu tunaokwenda nao katika makusanyo yaliyopelekwa karibu shilingi bilioni 29 angalau kiasi cha shilingi bilioni 4.6 kimerejeshwa, kwa hiyo, utaona tunafanya hivyo.

Hata hivyo, wakati wa hotuba yangu ya bajeti nilisema tunajaribu kuangalia na kupitia sheria hizi ili tuweze ku-*harmonize* ili fedha ambazo zinakusanywa zirejeshwe kwa utaratibu mzuri zaidi. Kwa hiyo, nachotaka kuahidi tu ni kwamba kwa kodi hizi zote mbili, ya ardhi na majengo, Waziri wa Fedha atakaposoma Sheria ya Fedha kwa mwaka 2017/2018 kutakuwa kuna mabadiliko ambayo yatazingatia maoni mengi ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge wakati nawasilisha bajeti yangu lakini katika mazungumzo mbalimbali kupitia maswali ya Wahemishiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, kuhusiana na asilimia kumi ambayo inatolewa kama mikopo kwa vijana na akina mama, tutajaribu kuangalia kama tunaweza tukaanzisha sheria mahsusi kwa ajili ya jambo hili kwa sababu kwa sasa lilikuwa limewekwa kiseru tu lakini hakukuwa na sheria inayo-*enforce*. Hata hivyo na lenyewe tumeliweka katika utaratibu endapo tutapata fursa ya kuleta mabadiliko ya sheria mbalimbali basi tutaliweka na maandalizi yake sisi kama Wizara tayari tumekwishayafanya.

**SPIKA:** Nimekuona Mheshimiwa Cecilia Paresso na Mheshimiwa George Lubeleje, tuanze na Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niulize swali ndogo la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano imechukua mfumo wa kodi ya majengo kukusanywa na *TRA*, lakini kumekuwa na sintofahamu kubwa kwa wananchi wetu kwamba ni majengo yapi hasa ambayo yanatakiwa kulipiwa kodi katika Halmashauri zetu maana hata nyumba za tembe na udongo nazo zinachangiwa kodi. Nini kauli ya Serikali kuhusiana na jambo hili?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa George Boniphace Simbachawene.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli mwaka 2015 kupitia Sheria ya Fedha tulifanya marekebisho ya sheria na katika kifungu cha 25(2)(b) tulieleza kwamba chanzo hiki badala ya kuwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mijini kiende hata kwenye Mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizovijijini yaani *District Councils*. Hata hivyo, tafsiri ya mabadiliko haya haijatafsiriwa vizuri na mamlaka zenyewe kwa sababu mazingara haya yalikuwa ni mahsus kwa maeneo kama yafuatayo; kwa mfano, Ngurdoto pamoja na *establishment* yote kubwa ya hoteli, *facillities* na kumbi za mikutano unaikuta iko vijijini, huwezi ukaacha kukusanya pale *property rate* au Bagamoyo yako maeneo mengi sana ya hoteli ambazo zipo vijijini, yalikuwa ni maeneo maalum kama hayo.

Mheshimiwa Spika, ili uweze kukusanya chanzo hicho ni lazima itugwe Sheria Ndogo kutoka kwenye Halmashauri husika na sheria hiyo inatungwa Waheshimiwa Wabunge mkiwa wajumbe. Unakuta inatungwa Sheria ya Ndogo ambayo kabisa inakiuka tafsiri nzuri ya sheria iliyotungwa na Bunge.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kueleza tu kwamba tafsiri ya kwamba ukusanyaji wa *property rate* sasa unakwenda mpaka kwenye vijiji kwenye nyumba za tope na udongo si sahihi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, usahihi ni kwamba kwa mazingira maalum ya uwekezaji ambayo uko vijijini lakini unauona ni uwekezaji wa kimjini huko ndiko zinatakiwa kukusanywa. Si kwa nyumba ya mwananchi wa kawaida ambayo halingizi kipato chochote, hajapangisha mtu yeyote, yeye anaishi tu, hatujafikia hatua hiyo kama nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nichukue nafasi hii kuziagiza Mamlaka zote za Serikali za Mitaa ambazo zinafanya hivyo kukusanya kutoka kwenye nyumba za tope, nyumba za bati au nyumba zozote lakini ambazo haziingizi mapato, si za kibiashara na ziko vijijini, hapana, haitakiwi kukusanya na Serikali ya CCM haijaamua uamuzi huo bado. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniona. Kwanza nilitaka niongezee tu kwamba kwa mwaka huu ambao tunamalizia, *TRA* ilikusanya kodi ya majengo kwa Halmashauri 30 tu, Halmashauri nyingine zilitakiwa kuendelea na utaratibu wa kawaida wa kukusanya mapato hayo yanayotokana na kodi ya majengo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisisitize nchi yetu hii ili tuende ni lazima tuendelee kujenga utaratibu wa wananchi wetu kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya Taifa. Nitatoa ufafanuzi mchana kuhusu kodi hii ya majengo na nimwombe sana Mheshimiwa Cecilia Pareso avumilie tu kidogo mpaka ile hotuba itakayowasilisha Bajeti Kuu ya Serikali mchana tutafafanua zaidi kuhusu kodi hii. Ahsante. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia usije ukaandamana ukatoka nje ili upate kusikia maneno kuhusu wananchi wako. Mheshimiwa George Lubeleje.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mwaka 1998/1999, mimi nikiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Katiba ya Sheria na Utawala, Serikali iliamua *TRA* ijaribu kukusanya kodi ya majengo na walianzia na Halmashauri za Manispaa tatu za Ilala, Temeke na Kinondoni. Baadaye walishindwa, Serikali ikarudisha tena kodi hizo zikusanywe na Manispaa hizo. Sasa ni sababu gani za msingi tena Serikali imeamua kodi ya majengo ikusanywe na *TRA* na siyo Halmashauri zenyewe? *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango nimekuona, majibu.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Sababu ya msingi kwa nini Serikali ilifanya maamuzi kwamba sasa kodi hii ianze kukusanywa na Mamlaka ya Mapato, kwanza, niseme Mamlaka ya Mapato kazi yake ni kukusanya mapato yote wala siyo ya kodi peke yake.

Pili, tuliona udhaifu mkubwa katika ukusanyaji wa mapato katika ngazi ile na ndiyo maana lengo la Serikali ni kusema tutumie chombo ambacho kina wataalam waliobobea kwa ajili ya kukusanya mapato haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la kusema huko nyuma walishindwa kwani ukishindwa maana yake ndiyo basi tena. Mzee wangu Mheshimiwa Lubeleje tumepata uzoefu, tumejifunza kutokana na uzoefu, tumefanya maandalizi ya kutosha na tuna hakika awamu hii tutaikusanya kodi hii ipasavyo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea, bado tuko Wizara hiyo hiyo ya TAMISEMI, swali linaulizwa na Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, Mbunge wa Bukombe, kwa niaba yake namuona amesimama Mheshimiwa Lolesia Bukwimba.

Na. 361

**Uhamisho Madaktari Wilaya ya Bukombe**

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA (K.n.y. MHE. DOTO M. BITEKO)** aliuliza:-

Je, ni kwa nini Serikali iliamisha madaktari saba kwa mara moja kutoka Hospitali ya Wilaya ya Bukombe huku ikijua Wilaya ya Bukombe ina upungufu mkubwa wa madaktari?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Doto Mashaka Biteko, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli kuwa Ofisi ya Rais, TAMISEMI iliamisha madaktari sita katika Hospitali ya Wilaya ya Bukombe ikiwa ni utaratibu wa kawaida wa kuimarisha ufanisi katika utoaji wa huduma za afya kwa wagonjwa. Ili kuziba nafasi za waliohamishwa kwa lengo la kutoathiri utoaji wa huduma za afya hospitalini hapo, Halmashauri hiyo ilipelekwa madaktari wapya watano na badaye Serikali ilipeleka madaktari wengine watatu na kufanya jumla ya madaktari waliopelekwa Bukombe kuwa nane. Lengo lilikuwa ni kuboresha utoaji wa huduma katika hospitali hiyo.

**SPIKA:** Mheshimiwa Lolesia Bukwimba, nimekuona.

**MHE. LOLESIA J. BUKWIMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwanza nitoe shukrani kwa kupeleka madaktari wanane kwa awamu, watano halafu watatu. Hata hivyo, kuna tetesi kwamba kuna daktari mmoja



atahamishwa hivi karibuni. Napenda kujua kama ni kweli na kama siyo kweli basi nipate ufafanuzi kutoka kwa Mheshimiwa Waziri kwamba kama wakimhamisha yule watatuletea tena lini daktari mwingine? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa changamoto katika Hospitali ya Wilaya ya Bukombe ni sawa kabisa na changamoto iliyoko katika Halmshauri ya Wilaya ya Geita, tuna upungufu mkubwa sana wa madaktari pamoja na wauguzi. Je, Serikali inasemaje kuhakikisha kwamba Serikali inaleta watumishi wa afya katika Halmshauri ya Wilaya ya Geita?

**SPIKA:** Kuhusu swali la kwanza Mheshimiwa Lolesia unataka Mheshimiwa Waziri atueleze kuhusu tetesi? Mheshimiwa Waziri majibu ya maswali hayo.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, suala la kwamba kuna tetesi za kuhamishwa hivi karibuni kwa daktari mwingine labda kwa sababu anajua ambayo Waheshimiwa Wabunge wengi hawajui na labda pengine kwa sababu ya kuweka sawa niweke vizuri kwamba hata ule uhamisho wa mwanzo tulioufanya ulikuwa ni kwa sababu kulikuwa kuna shida ya kutafuta madaraka hali iliyopelekea daktari mmoja aliyekuwa anakaimu nafasi ile akashambuliwa mtaani ambapo ilionekana kama ni kutokana na mazingira hayo. Ndiyo maana tukafanya ule uhamisho na baadaye tukapeleka madaktari wengine. Kwa hiyo, kama ni tetesi zenye dhana ile ile na pengine hatua hizi zitakuwa zina sababu ile ile atahama, lakini haina maana kwamba hatutapeleka daktari mwingine kuziba nafasi hiyo.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ameuliza kuhusu upungufu wa madaktari kwa maeneo yote sasa siyo tu Bukombe na Geita, lakini pia najua tuna upungufu wa madaktari na wauguzi katika maeneo mengi. Mheshimiwa Rais ametoa kibali cha ajira za watumishi wengine 15,000 ambao wataziba nafasi ya hawa watumishi hewa waliokuwa na vyeti *fake* ambao wameondolewa. Kibali

hicho kinaendelea na katika kibali hicho pia tuna idadi kubwa tu ya wataalam wa afya ambao watakuja kwa ajili ya ku-*replace* lakini tuna ajira zingine 54,000 ambazo ni za mwaka huu wa fedha ambazo na zenyewe tunaamini katika kufanya hivyo tutaziba eneo kubwa sana la upungufu siyo tu wa idara hii ya afya lakini pia na idara nyingine kwa ujumla wake.

**SPIKA:** Nili kuona Mheshimiwa Flatei Massay.

**MHE. FLATEI G. MASSAY:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa sasa kutokana na vyeti feki vimeondoa kabisa watumishi wa afya katika zahanati zetu. Je, ni lini hasa hawa watumishi wataenda kuajiriwa yaani wanayo *time frame* kwa sababu sasa hivi zahanati zina shida katika huduma hii ya afya? Ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Massay, Mbunge wa Mbulu, je, ni lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kutokana na vyeti *fake*, watumishi takribani 12,000 wameondolewa katika utumishi wa umma.

Hata hivyo, kibali kilichotolewa na Mheshimiwa Rais ni cha watumishi 15,000 na tunaamini kabisa kwamba hawa watakwenda kuziba. Mchakato wake ilibidi kwanza tufanye uhakiki mzuri kwamba waliotoka ni wa idara zipi na zipi, walimu ni wangapi, manesi wangapi na madaktari wangapi. Kazi hiyo tumeimaliza na tumeshakabidhi Wizara ya Utumishi na mchakato unaendelea. Bila shaka wakati wowote tunaweza tukawaingiza katika ajira watumishi hawa wapya.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Maji na Umwagiliaji na swali linaulizwa na Mbunge wa Nyang'hwale, Mheshimiwa Hussein Nassor Amar, kwa niaba yake litaulizwa na Mheshimiwa Augustino Masele.

Na. 362

## Miradi ya Maji

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE (K.n.y. MHE. HUSSEIN N. AMAR)** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikitumia pesa nyingi sana kuanzisha miradi mikubwa na midogo ya maji.

(a) Je, Serikali inaweza kueleza ni miradi gani mikubwa na midogo iliyokamilika na isiyokamilika katika Jimbo la Nyang'hwele?

(b) Je, kama kuna miradi ambayo haijakamilika mpaka hapo ilipofikia imetumia fedha kiasi gani?

(c) Je, ni lini sasa miradi hiyo itakamilika katika Jimbo la Nyang'hwele?

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Augustino Masele. Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhandisi Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji na Umwagiliaji, naomba kujibu swali ya Mheshimiwa Hussein Nasser Amar, Mbunge wa Nyang'hwele, kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Nyang'hwele inatekeleza mradi mkubwa mmoja wa Nyamtukuza kupitia Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji. Mradi huu utahudumia jumla ya vijiji tisa vya Nyamtukuza, Nyarubele, Kakora, Kitongo, Ikangala, Kharumwe, Izunywa, Kayenze na Bukwimba ambavyo vinaendelea na ujenzi. Miradi ya maji iliyokamilika katika Halmashauri ya Nyang'hwele ni Kanyenze, kakora, Ikangala, Nyamtukuza na Kharumwa.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa Maji wa Nyamtukuza unaotuma chanzo cha Ziwa Victoria unatekelezwa kwa jumla ya fedha shilingi bilioni 15 na mpaka sasa Serikali imepeleka fedha shilingi bilioni 3.78 za kutekeleza miradi ya maji na usafi wa mazingira katika Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale.

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la Serikali ni kutuma fedha kwa Halmashauri zote zinazoendelea na ujenzi wa miradi ili kuhakikisha miradi yote iliyoanza inakamilika kabla ya kuanza kwa miradi mipya.

**SPIKA:** Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele, swali la nyongeza.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kuniruhusu niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, kwanza naipongeza Serikali kwa kuhakikisha kwamba miradi ya Kayenze, Kakora, Ikangala, Nyamtukuza na Kharumwa inakamilika, hongera sana kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Sasa napenda kuuliza, je, Serikali inaweza ikawaambia watu wa Nyang'hwale ni lini sasa huu mradi mkubwa wa vijiji tisa utakamilika?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Wilaya ya Mbogwe ipo jirani kabisa na Wilaya ya Kahama ambako kuna mradi mkubwa wa maji ya Ziwa Victoria, je, Serikali haioni kwamba ni wakati sasa umefika kuiweka Wilaya yetu ya Mbogwe katika programu ya kuweza kupata maji haya kutoka Kahama? Ahsante.

**SPIKA:** Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, Mhandisi Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, tuwahakikishie wananchi kwamba mradi huu utakamilika. Mradi huu wa Nyang'hwale umepata shida kidogo ya kiutendaji na shida yenyewe ni

kwamba Halmashauri ilitafuta mkandarasi mwingine wa kuleta mabomba na mkandarasi mwingine wa kujenga. Sasa yule mkandarasi wa kujenga hawezi kufanya kazi kama wa kuleta mabomba hajaleta na yule wa kuleta mabomba inaonekana kwamba ni kama kidogo yupo dhaifu kwa sababu hadi leo hajaleta mabomba na mkataba ni wa tangu mwaka 2014 mwezi wa pili. Hivi tunavyoongea sasa hivi ni kwamba tayari yapo mazungumzo kati ya Wizara yangu na Halmashauri ya Nyang'hwale kuhusiana na huyu mkandarasi ambaye ameshindwa kutekeleza majukumu yake na mkataba wake ulikuwa ni wa shilingi bilioni tano. Yule mkandarasi wa kujenga tayari ameshakamilisha matenki, anachosubiri ni mabomba aweze kuyalaza ili wananchi wapate maji.

Kwa hiyo, hili Mheshimiwa Mbunge tunalishughulikia na mara tutakapomaliza nitakupatia majibu ili wananchi sasa waweze kuwa na uhakika ni lini hayo maji yatapatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, Halmashauri ya Mbogwe, kwa sasa tunaendelea, tayari kuna visima ambavyo tumechimba na kwa sasa Halmashauri imesaini mkataba wa visima sita ili tunaposubiri mradi mkubwa na kwa kuwa Geita ni miongoni mwa mikoa ambayo imepata msaada wa hizi fedha kutoka Serikali ya India, nikuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kupitia fedha hiyo basi tutaendelea kuhakikisha pia na Mbogwe inapata maji kutoka Ziwa Victoria.

Pia unayo fursa nyingine kupitia bomba la Lake Victoria linalokwenda Solwa, napo tayari tunaanza kuangalia kama tunaweza tukachukua maji kutoka Kahama pale kwenda kwenye ile milima kilometa 40 na baadaye tukayashusha kwenda Mbogwe. Wataalam wanafanyia kazi kama hilo litakuwa limekaa vizuri basi pia unaweza ukapata maji kutoka bomba la *KASHWASA*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Duh! Haya mambo ya maji ni hatari kubwa, Mheshimiwa Waziri wa Fedha unauona ujumbe huo? Hapa

*issue* ni maji. CUF hamjauliza swali la nyongeza tangu tuanze, tafadhali swali la nyongeza halafu nimesahau na Mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Singida utafuata. (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi.

**MBUNGE FULANI:** Siyo CUF huyo.

**MHE. MAFTAH A. NACHUMA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumuuliza Mheshimiwa Waziri, tatizo hili la maji katika Wilaya ya Nyang'hwale linafanana kabisa na tatizo la maji Mtwara Mjini na kwa kiasi kikubwa Mtwara Mjini kuna mradi ambao ulipangwa kutekelezwa kwa kupata pesa kutoka Benki ya Uchina ambapo mpaka sasa bado hizp pesa hazijapatikana.

Juzi nilikuwa namuuliza Mheshimiwa Waziri akaniambia kuna pesa zingine zimesainiwa maji yatoke Bonde la Ziwa Kitele mpaka Mtwara Mjini.

Je, Serikali iko tayari hivi sasa kutekeleza mpango wa muda mfupi wa kuchimba visima kwa kutumia gari za Idara ya Maji ambazo zipo pale Mtwara katika maeneo ambayo maji hakuna kama Kata ya Ufukoni na Likombe?

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, majibu kwa swali hilo lililoulizwa na Mheshimiwa Maftaha, Mbunge wa Mtwara Mjini.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza Serikali inaendelea kuhakikisha kwamba Mji wa Mtwara unapata maji safi na salama. Mwezi uliopita tumesaini mkataba wa shilingi bilioni tano ambao utatoa maji Mbue kwenye Bonde la Kitele kupeleka mjini. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Mbunge wewe ni Mbunge wa Mji wa Mtwara, kwa hiyo, maeneo yote ambayo yalikuwa hayajapata maji safi tunahakikisha kwamba yanapata hata kabla ya huo mradi mkubwa wa kutoa maji Mto Ruvuma kuleta Mtwara Mikindani.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusiana na huu mradi mkubwa wa kutoa maji Ruvuma, tayari Serikali iko kwenye hatua za mwisho kukamilisha mazungumzo na *Exim Bank* ya China ili sasa utekelezaji uanze. Kwa hiyo, nikuombe tu Mheshimiwa Mbunge kwamba uvute subira Serikali yako kupitia Wizara ya Maji na Umwagiliaji inaendelea kuzungumza na hawa wafadhili kwa maana ya Waziri wa Fedha (Hazina) wanaendelea kuzungumza na mfadhili ili mambo yakikamilika tuanze utekelezaji.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Singida, swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Wanawake wa Kongwa, Singida na wa nchi nzima wanasubiri utekelezaji wa kauli ya kumtua mwanamke ndoo. Leo hii Mheshimiwa Waziri anajibu swali kwa kusema kwamba mkandarasi alipata mkataba mwaka 2014 mpaka sasa eti wana mazungumzo. Naomba Mheshimiwa Waziri aendane na kauli ya kumtua mwanamke ndoo kwa kusitisha kwa haraka mikataba inayosuasua ili tuwaokoe wananchi wa Tanzania. Ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer* Gerson Lwenge, majibu ya maji.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa katika utekelezaji wa kuhakikisha kwamba Watanzania wanapata maji, tulianzisha hii Programu ya Maji na tukawapa hawa Wakurugenzi wa Halmashauri kusimamia miradi mingi. Toka tumeingia Awamu ya Tano, kitu cha kwanza tulichofanya tumeikwamua miradi mingi iliyokuwa imesimama baada ya fedha kuanza kwenda.

Mheshimiwa Spika, hatua ya pili, tunafanya mapitio ya mikataba yote ya hovy ambayo ilikuwa imeingwiwa halafu wanafika mahali wamekwama. Kwa hiyo, mikataba ile ambayo ilikwenda vizuri miradi imekamilika na sasa hivi kati ya miradi 1,800 miradi 1,300 imekamilika, bado hii 400 ambayo inaendelea kwa hatua mbalimbali.

Kwa hiyo, katika hii 400 kuna baadhi ya mikataba ambayo tunafanya mapitio kama huo mradi wa Nyang'wale ambao kidogo una figisu figisu kwamba mkataba wa kujenga matanki na kupeleka mabomba ni watu tofauti. Sasa mikataba ikiwa ya namna hiyo unakuta mmoja akizembea, utekelezaji unakuwa hafifu. Kwa hiyo, azma ya Serikali ya kuhakikisha kwamba tunamtua mama ndoo iko pale pale.

**SPIKA:** Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri wa Maji bado. *(Kicheko)*

**WABUNGE FULANI:** Bado. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Massare, Mheshimiwa Bura na Mheshimiwa Rhoda Kunchela.

**MHE. YAHAYA O. MASSARE:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niulize swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Mji wa Itigi wenye Kata tatu za Majengo, Itigi Mjini na Tambukareli na vijiji saba vya Kihanju, Songambebe, Tambukareli, Majengo, Ziginali, Itigi Mjini na Mlowa havina kabisa huduma ya maji toka nchi hii ipate uhuru na hata kabla ya wakati huo ikitawaliwa na mkoloni na kwa kuwa Halmashauri yetu inafanya juhudi na tumeandika barua kwa Wizara ya Maji kuomba Mhandisi wa Wizara hii aje atushauri namna gani ya kuweka miundombinu ya maji na kwa kuwa hadi leo hatujapata majibu.

Mheshimiwa Spika, nini kauli ya Serikali kwamba dhamira ya Serikali ikoje kuwasaidia wananchi wa Itigi na wenyewe wapate huduma hii ya maji kwa kuleta Mhandisi aweze kutushauri namna ya kuweka miundombinu ya maji?  
*(Makofi)*

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo la Mheshimiwa Yahaya Massare, Mbunge wa Itigi.



**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:**

Mheshimiwa Spika, kwanza nikuhakikishie kwamba kutokana na utaratibu uliowekwa na Wizara ya Maji na Umwagiliaji Awamu ya Tano ya kuhakikisha kila Halmashauri inatengewa bajeti, tumeendelea kutenga bajeti kwa kila Halmashauri ili waweze kutekeleza miradi ya maji katika Halmashauri zao kwa sababu wapo karibu na wanaelewa matatizo yanayowazunguka.

Mheshimiwa Spika, nakiri ni kweli Mheshimiwa Mbunge uliniambia kwamba barua kuomba wataalam kutoka Wizara ya Maji inawezekana imeshakuja tayari lakini nitaifuatilia. Tatizo kubwa ambalo liko kwenye Halmashauri yako ni kukosa wataalam wenye weledi na tuliongea na kushauriana kwamba sasa ulete barua ili tuweze kukusaidia wataalam ama tukuchukulie wataalam kutoka Mamlaka ya Maji ya Singida au Makao Makuu ili wakasaidiane na wataalam wa Halmashauri yako kuhakikisha kwamba tunafanya usanifu wa haraka na ulio bora na utekelezaji uendeleo. Kwa hiyo, nikuhakikishie kwamba tutakupatia wataalam Mheshimiwa Mbunge.

**SPIKA:** Mheshimiwa Bura.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kero ya maji iliyopo Nyang'hwale inawasumbua sana wanawake wa Wilaya ya Kongwa na Mheshimiwa Naibu Waziri nimekuuliza mara nyingi ukipita hapa jirani yangu kuhusu Wilaya ya Kongwa na ukaniambia umetoa fedha kwa ajili ya maji Wilayani Kongwa. Visima vinavyotoa maji Wilayani Kongwa havizidi vitatu, visima vingine vilivyobaki vilivyochimbwa na *World Bank* havitoi maji. Ni jana tu nimeongea na Mkurugenzi wa Kongwa akaniambia shida ya maji ya Kongwa ipo palepale, maji yanayotoka ni kwa maeneo machache sana.

Naomba leo Naibu Waziri aniambie maji yatatoka lini Kongwa ya kuwatosha wanawake wa Kongwa? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, hili swali unapojibu uwe na umakini mkubwa. Tafadhali majibu Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji kwa swali hilo muhimu. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, nina umakini mkubwa sana na Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa nimeifanyia kazi sana tangu nakuwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji. Ni juzi tu nilipeleka mtambo wa kuchimba visima Kongwa na kwamba tayari kuna visima vya kutosha ambavyo vimechimbwa lakini siyo kwamba tumekamilisha Jimbo zima au Halmashauri nzima ya Kongwa, kwa hiyo, tunaendelea. Kama bado kuna maeneo yanahitaji kupata visima tupo tayari kuendelea kuchimba na hasa kwa kuzingatia kwamba katika bajeti ya mwaka wa fedha 2017/2018 tumeweka fedha tena kwa ajili ya kuendelea kuwapatia akina mama maji.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie mama yangu Mheshimiwa Bura kwamba sisi tumedhamiria kuhakikisha kwamba kweli tunamtua mama ndoo kichwani. Yule ambaye hatatuliwa ndoo kichwani ni kwamba atakwenda kuchota maji umbali usiozidi mita 400 kutokana na sera yetu. Kwa bahati nzuri na mimi mwenyewe naishi Dodoma Mama Bura, kwa hiyo, tutakuwa pamoja na kwa vyovyote vile tuambatane tukaangalie maeneo mengine ambayo hayana ili tuweze kuyapatia maji. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Rhoda swali la mwisho.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante,...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Maji alisimama, majibu ya nyongeza tafadhali.

**WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, ili kulinda Kiti cha Spika kwa sababu wewe huwezi kuuliza swali la nyongeza, naomba nikiri kwamba Mji wa Kongwa tumepata kisima ambacho kinatoa maji mengi. Sasa hivi

kinachotakiwa ni kupeleka fedha ili tuweze kujenga miundombinu. Naomba nikuahidi kwamba tutapeleka fedha kwa ajili ya kujenga miundombinu ili wananchi wa Kongwa waweze kupata maji ya kutosha. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ubarikiwe sana Mheshimiwa Waziri. Mheshimiwa Rhoda.

**MHE. RHODA E. KUNCHELA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Kwa takwimu hizi, kutokana na bajeti ya Mheshimiwa Waziri, bado Serikali hii haijajipanga kutatua tatizo la maji nchini. Mkoa wa Katavi una vituo zaidi ya 148 vinahitaji ukarabati na hivi tunavyoongea, wakazi wa Mpanda pamoja na Katavi hawajapata maji karibu wiki mbili zimepita. Nini mkakati wa Serikali kuhakikisha hivi vituo 148 vinafanyiwa ukarabati na wananchi wanapata maji kwa wakati?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji na Umwagiliaji, *Engineer* Isack Kamwelwe.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani na kuunda Wizara ya Maji na Umwagiliaji, Mkoa wa Katavi tayari tumeshachimba visima zaidi ya 40 na wananchi wanapata maji. Kwa hiyo, huduma ya maji katika Mkoa wa Katavi imeongezeka. Kwa sasa tumeshasaini mkataba mmoja ili kuleta bomba lingine kutoka Ikorongo kwa ajili ya Mji wa Mpanda na tayari mkandarasi yuko kazini na tunatarajia kusaini mkataba mwingine wa pili ili kuongeza kiwango cha maji kutoka kilichopo sasa hivi cha lita 3,150,000 ili twende zaidi ya lita milioni sita. Kwa hiyo, kwanza ni kwamba maji Katavi tayari yanaendelea kuongezeka.

Mheshimiwa Spika, lakini pili tulipeleka mashine ili kufanya ukarabati wa visima vyote ambavyo vilikuwa havitoi maji kwa maana ya kuvifanyia *flushing* na zoezi hilo limefanyika na linaendelea kufanyika ili kuhakikisha vile visima ambavyo uwezo wake wa kutoa maji ulikuwa umepungua basi vinaendelea kutoa maji wananchi waendeleo kupata

huduma. Kwa hiyo, si kweli kwamba Serikali imeshindwa kutoa maji, tayari kiwango kilichokuwepo tumeongeza na tunaendelea na tutafikisha asilimia 85 itakapofika mwaka 2020.

**SPIKA:** Tunaendelea na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, swali linaulizwa na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile.

Na. 363

### **Mpango wa Kujitathmini kwa Vigezo vya Utawala Bora (APRM)**

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM** aliuliza:-

Tanzania ni moja kati ya nchi wanachama wa Nchi za Kiafrika wa Kujitathmini Wenyewe kwa Vigezo vya Utawala Bora (APRM).

Je, Serikali imejitathmini kwa kiasi gani katika dhana nzima ya demokrasia na utawala bora, utawala wa kisiasa, usimamizi wa uchumi na maendeleo ya kijamii?

**SPIKA:** Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Mheshimiwa Dkt. Kolimba.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mbunge wa Mtambile, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kujitathmini Kiutawala Bora Barani Afrika (APRM) ulibuniwa na Wakuu wa Nchi za Kiafrika kwa lengo la kuimarisha utawala bora katika nchi zao. Nchi hujitathmini yenyewe kwanza na kutoa ripoti

na mpango kazi na kisha nchi nyingine zilizojiunga katika mchakato huu huja kuitathmini nchi hiyo na kutoa ripoti ya nchi ya utawala bora. Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi 35 zinazoshiriki katika mchakato huu ambapo ilijiunga mwaka 2004 na Bunge la Tanzania liliridhia makubaliano hayo mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, katika mchakato wa kujitathmini, Watanzania wa kada mbalimbali waleleza mambo bora yaliyofanywa na nchi yetu na kuonesha changamoto zilizopo. Tathmini hizi ziliangazia maeneo makuu manne ambayo ni utawala bora katika siasa na demokrasia, usimamizi wa uchumi, utendaji wa mashirika ya kibiashara na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, katika tathmini iliyofanyika na ripoti yake kutolewa mwaka 2012, baadhi ya maeneo ambayo Tanzania ilibainika kufanya vizuri ni pamoja na kuingia kwa amani katika Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa, kurithishana madaraka ya Urais kwa mujibu wa Katiba, matumizi ya lugha kuu ya Kiswahili, kuimarika kwa jitihada za kupambana na rushwa, kuboresha usawa wa jinsia, usuluhishi wa migogoro, Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuwekwa wazi na mafanikio katika kupanuka kwa utoaji huduma za jamii na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya changamoto za utawala bora zilizobainishwa ni pamoja na changamoto kama Tume ya Uchaguzi; ukuaji wa uchumi usiowiana na kupungua kwa umaskini; tatizo la fedha haramu na dawa za kulevya; changamoto katika utoaji wa huduma za kijamii ikiwa ni pamoja na elimu iliyo bora na uhaba wa vifaa katika huduma za afya.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa uratibu wa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki inaendelea kutekeleza hatua zenye lengo la kutatua changamoto za utawala bora zilizobainishwa kwenye Ripoti ya *APRM*. Inatarajiwa mwaka huu 2017, Serikali ya Tanzania itawasilisha Ripoti ya Utekelezaji wa Mpango Kazi wa *APRM* kwenye kikao

cha Wakuu wa Nchi na Serikali wanaoshiriki mchakato wa mpango huu.

**SPIKA:** Mheshimiwa Masould Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza, msingi mkubwa wa Serikali iliyopo madarakani unatokana na ridhaa ya wananchi, lakini hali ya maisha ya wananchi wetu ni duni, mzunguko wa fedha ni mdogo sana, wananchi wanalalamika sana kwamba fedha imepotea/haipo mtaani na kasi ya ongezeko la maisha magumu imekuwa kubwa kupita kiasi. Kwa muda mrefu sana Serikali hii imekuwa ikijisifia wanakusanya zaidi lakini hali ya uchumi wa wananchi wetu imekuwa mbaya sana. Nimuombe Mheshimiwa Waziri atuambie leo fedha ambazo zilikuwa zinaonekana kwa muda mrefu katika mzunguko mtaani sasa ziko wapi na wana mkakati gani wa kuboresha hali ya maisha ya Watanzania? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili, anasema kwamba mwaka huu 2017 mnataka kujitathmini wenyewe, katika kujitathmini wenyewe mtaandika kweli? Kwanza mambo yafuatayo, haki ya kupata habari kwa mujibu wa Ibara ya 18 ya Katiba yetu, Bunge haliko *live*, mikutano ya hadhara imepigwa marufuku...

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud sasa swali.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Spika, swali sasa linakuja, kwa kuwa Bunge haliko *live*, mikutano ya hadhara imepigwa marufuku, katika kujitathmini wenyewe mtaandika kweli haya au kuna haja ya kutafuta chombo kingine huru *APRM Number Two* ili iandike uhalisia kwa sababu mambo kama haya kweli mtaandika wenyewe? Nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Masoud nikuhakikishie haya yote uliyooonea Bunge liko *live* mpaka Pemba wanakusikia hivi sasa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tafadhali.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kuniona.

Mheshimiwa Spika, kwanza nalitaka nimuombe Mheshimiwa Masoud avute subira kidogo. Leo nitapata fursa ya kueleza kwa kirefu hali ya uchumi ambayo ni pamoja na masuala ya maisha magumu, mzunguko wa fedha, fedha imekwenda wapi, kwa hiyo, namuomba avute subira tu kidogo, asubuhi hii na mchana leo.

Mheshimiwa Spika, la pili, kuhusu kujitathmini, kila robo mwaka Serikali inajitathmini katika vigezo mbalimbali, kila robo mwaka, kila nusu mwaka na kila baada ya mwaka mzima. Taarifa zipo, ukienda kwenye tovuti ya Wizara ya Fedha taarifa zipo, tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango taarifa zipo na sasa hivi mmeanza kugawiwa vitabu ambavyo vinatoa tathmini.

Mheshimiwa Spika, siyo hivyo tu, katika ngazi ya Afrika Mashariki tunajitathmini ili kuweza kujua kama kweli tunaelekea kwenye vigezo ambavyo tulikubaliana tunapokwenda kwenye Umoja wa Shirika la Fedha. Kwa hiyo, tuna *convergence criteria* ambazo tunazitathmini nchi baada ya nchi na tunakwenda vizuri. Tanzania ni moja kati ya nchi ambazo kwenye *macro-economic convergence criteria* tuko vizuri. Nikuhakikishie tu kwamba hizi taarifa ziko wazi na hakuna mahali popote zitaminywa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa, Kamishna, swali la nyongeza.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, katika majibu ya Mheshimiwa Waziri kuhusu demokrasia, hivi tunavyozungumza wanafunzi wa CHASO wanaohusiana na Chama cha Demokrasia na Maendeleo wanazuiwa kufanya mahafali yao wakati wanafunzi wa Chama cha Mapinduzi wanaruhusiwa na kuna barua za polisi zinazuia mikutano hiyo. Unawezaje kusema tunafanya demokrasia kwa kiwango kikubwa wakati kuna upendeleo wa wazi kabisa? Ni sawa na kwenye ndondi, mmoja amefungwa mikono halafu unasema upigane.

Je, Waziri atakuwa tayari kuliagiza Jeshi la Polisi liache kufanya upendeleo katika kutekeleza majukumu ya ku-*practise* demokrasia? (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki ndiyo inatoa vibali kwa wanafunzi kufanya mahafali?

(*Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio*)

**SPIKA:** Bado napima kama swali hili linakubalika. Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi.

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, niseme tu mambo mawili, moja, alilosema Mheshimiwa Masoud la mikutano ya hadhara, mikutano hii haijazuiwa ila imewekewa utaratibu na duniani kote *standard* ya mikutano ya hadhara ni kama hivi tunavyofanya sisi hapa sasa. Tusifanye vitu kimazoea, duniani kote *standard* ya mikutano ya hadhara ni hivi tunavyofanya sisi, nendeni hata kule tulikojifunza demokrasia ya siasa ya vyama vingi huu ndiyo utaratibu wanaotumia. Mwaka jana Marekani imefanya uchaguzi, mmemuona Hillary akishukuru? Aliyeshinda ndiye anaendesha Serikali kwa utaratibu wa Kiserikali wa kuendesha taratibu, hili liko wazi duniani kote wala si la kuuliza, ndiyo utaratibu unaotumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu mikutano aliyoisemea Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, niseme tu taratibu ziko wazi. Kama CCM wamefuata taratibu wakapewa mikutano,



chama kingine chochote wanachotakiwa ni kufuata taratibu zilezile waweze kupewa mikutano...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila mpangilio)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, hili na lenyewe liko wazi. Kama wengine hawajafuata utaratibu hawatapewa tu kwa sababu CCM walipewa, watapewa kwa kufuata utaratibu. Mheshimiwa Mchungaji Msigwa tumekuwa tukifanya hivyo kote na si sehemu yako tu, mbona kuna sehemu nyingine CHASO haohao wamepewa mikutano? Kwa hiyo kinachotakiwa ni kufuata taratibu za kupewa mikutano hiyo. *(Makofi)*

Sasa Mheshimiwa Esther, Waziri wa Mambo ya Ndani akiongea unatakiwa unyamaze, nimeshajua kwa nini babu zangu kule Mara wanapiga wake zao. Mtu anapoongea, hasa Waziri ambaye ana Jeshi la Polisi unatakiwa unyamaze kimya umskilize. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, *message sent.*

Waheshimiwa Wabunge, nawashukuru. Maswali yamekamilika na kama tulivyosema leo ni siku maalum ina mambo mengi ambapo nitaomba sana usikivu wenu. Baadaye nitaendelea kutambulisha baadhi ya wageni tulionao lakini mpaka jioni tutakuwa na wageni wengi sana hapa mjengoni kwetu. Kwa kifupi tu wageni wote karibuni sana.

Nina matangazo machache, la kwanza ambalo napenda kuwajulisha Waheshimiwa Wabunge na naomba tusikilizane ni kwamba katika jitihada za kuhakikisha kwamba Bunge letu lina uwakilishi wa Watanzania wote na katika kuhakikisha tunawafikia wote hata wale wenye mahitaji maalum, nafurahi kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge na wananchi wa Tanzania kwamba kuanzia leo tuna mtaalam wa lugha ya alama ambaye anafanya kazi sambamba na watangazaji wa televisheni kwenye Kituo chetu cha Bunge kinachorusha matangazo *live*. Ndiyo maana nikamwambia

Mheshimiwa Masoud tunatangaza *live* na leo kutwa nzima ni *live*. Hivyo, Watanzania wasiosikia wanaweza sasa kufuatilia matangazo ya Bunge na kufaidika nayo, huduma hiyo imeanza rasmi leo na itaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Mkuchika, Mwenyekiti wa Kamati ya APNAC Tanzania anaomba niwatangazie Wajumbe wa APNAC Tanzania waliopata barua za mwaliko kuwa semina iliyoahirishwa jana itafanyika leo tarehe 8, Juni katika Ukumbi wa African Dreams saa saba mchana au mara tu baada ya kuahirisha shughuli za asubuhi hii, kwenye *around* saa sita na kitu. APNAC wale wenye barua, tukiahirisha shughuli za asubuhi wahini kule African Dreams, yapo maandalizi mazuri.

Naomba pia niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba Mbunge mwenzetu wa Jimbo la Mbarali, Mheshimiwa Haroon Mulla Pirmohamed ambaye kama mnavyofahamu ni mkulima wa mpunga pamoja na mazao mengine, katika mwezi huu Mtukufu wa Ramadhani aliniomba atoe sadaka na mimi nimemkubalia, ya kutoka shambani kwake ambapo atatoa sadaka ya mchele kwa Waheshimiwa Wabunge na watumishi wote wa Bunge leo. *(Makofi)*

Napenda kumshukuru kwa niaba yenu Mheshimiwa Haroon. Mchele huo ni ule mchele *grade one* kabisa unaoitwa mchele wa Mbeya, kwa hiyo, utakuwepo pale *basement* kila atakayetoka baada ya shughuli zetu za asubuhi hii mwenye nafasi apitie pale aweze kuchukua sadaka hiyo. Mgao huo ni wa bure, siyo kwamba kuna kununua, ni sadaka. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, nina tangazo muhimu naomba mlisikilize, nalo ni kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa, anawaalika katika futari leo jioni mara tu baada ya kuahirishwa hotuba ya bajeti. Futari hiyo itakuwa katika viwanja vya Bunge eneo ambalo huwa tunafanyia sherehe pale nyuma ya Jengo la Utawala. *(Makofi)*

Kwa niaba yenu naomba tumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa maandalizi hayo na kwa mwaliko huu ambao utajumuisha Waheshimiwa Wabunge wote, watumishi wote wa Bunge na wageni wote watakaokuwepo leo jioni pamoja na sisi kwa ajili ya shughuli za bajeti. Hivyo, nawaomba sana Waheshimiwa Wabunge wote tushiriki na wale ambao tunaandaaandaa futari majumbani huko basi tuahirishe, futari itakuwepo hapahapa. Tukishamalizana na Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango hapa tukitoka wote kwa pamoja tunakwenda kwenye futari pale nyuma, kwa hiyo, msisahau jambo hilo. *(Makofi)*

Upande wa kutambulisha baadhi ya wageni, naomba nitambulisha wageni 30 wa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, ambao ni viongozi wa Wizara na taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo ya Fedha wakiongozwa na Ndugu Doto James, Katibu Mkuu; karibu sana pale ulipo. Naibu Makatibu Wakuu watatu; Dkt. Khatibu Kazungu, Ndugu Dorothy Mwanyika na Ndugu Amina Shaaban; Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Ndugu Maduka Kessy na Gavana wa Benki Kuu, Profesa Benno Ndulu. Wameambatana na wageni wengine ambao ni viongozi mbalimbali wa idara na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Pia kuna mageni 34 ambao ni Washirika wa Maendeleo *(Development Partners)* wakiongozwa na Mwenyekiti wao ambaye ni Balozi wa Umoja wa Ulaya, Mheshimiwa Roeland va De Geer. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni wageni 53 wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambao ni wanafunzi wa Shule ya Msingi Ihefu kule *Sao Hill* kutoka Mafinga Mkoa wa Iringa. Mmependeza kweli kweli, karibuni sana wanafunzi na walimu kutoka kule Mafinga. *(Makofi)*

Tuna wageni 40 wa Mheshimiwa Omary Badwel ambao ni wanafunzi 33 na walimu saba kutoka Bahi Mkoa

wa Dodoma. Karibuni sana watoto wazuri wa kutoka Bahi.  
(Makofi)

Wageni waliotembelea Bunge kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 70 na walimu watano kutoka Chuo cha Utafiti (*Tanzania Research and Career Development Institute*) cha Mkoani Dodoma. Sikujua kama tuna *Career Institute* hapa Dodoma, karibuni sana. (Makofi)

Waheshimiwa Wabunge kwa sababu ya shughuli za leo, naomba sasa moja kwa moja tuendeleo na shughuli zilizoko mezani ili tuweze kuokoa muda, Katibu.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo

**SPIKA:** Leo tuendeleo miongozo tutachukua wakati mwingine.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Spika, Mwongozo.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI-KATIBU MEZANI:**

### HOJA ZA SERIKALI

#### Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018

**SPIKA:** Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango tafadhali tunaomba utuwasilishie Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka 2017/2018, karibu tafadhali.  
(Makofi)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2017/2018. Pamoja na hotuba hii nawasilisha Vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi

kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018, ambapo taarifa hizi ndiyo msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 itakayowasilishwa Bungeni baadaye hivi leo.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano wa Saba wa Bunge la Kumi na Moja la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tukiwa na dhamira ya kulinda na kuendeleza amani na maelewano hapa nchini na pia ari ya kufikia malengo yetu ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya bajeti za kisekta na shughuli nyingine za Bunge hili kwa umakini, utulivu na hekima kubwa. Ni matumaini yangu kuwa uzalendo uliojionyesha wakati wa kujadili hotuba za mipango na bajeti za kisekta utaendelea kudumishwa.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwa kuondokewa na Wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Dimani (CCM) na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha, Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Pia nitumie fursa hii kuwapa pole Wabunge wote waliopoteza wapendwa wao na wananchi wote waliopatwa na maafa mbalimbali katika mwaka huu, yakiwemo matukio ya kusikitisha ya kuondokewa na watoto wetu 32, walimu wawili na dereva wa Shule ya Lucky Vincent katika ajali Mkoani Arusha mwezi uliopita, wanafunzi watatu kule Mkoani Geita...

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nawaomba sana tuwe na usikivu tumsikilize Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Wanafunzi wawili na mzazi mmoja Mkoani Kagera kwa kuzama majini na askari

wetu nane na wananchi wengine waliouawa kikatili katika matukio ya kupanga Mkoani Pwani. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi.

**WABUNGE FULANI:** Amen.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, kipekee kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mbunge), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi madhubuti kusimamia mabadiliko yanayoleta tija katika utendaji Serikalini; kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii na kuendeleza misingi ya utawala bora. Uongozi wao umejipambanua katika kupambana na rushwa, ufisadi, ukwepaji kodi, uzembe na urasimu katika utumishi wa umma na ubadhirifu wa mali za umma lakini pia msisitizo wa umuhimu wa kila mwananchi kufanya kazi. Juhudi hizi zinapaswa kuungwa mkono kwa nguvu zote na viongozi na wananchi wote.

Mheshimiwa Spika, niruhusu pia niwapongeze kwa dhati Wabunge wapya walioingia Bungeni katika Mkutano huu wa Saba wa Bunge la Kumi na Moja ambao ni Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare, wote wa CCM na Mheshimiwa Catherine Ruge wa CHADEMA. Tunawakaribisha kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kutekeleza wajibu wa misingi wa Bunge wa kuishauri na kuisimamia Serikali kwa hekima na weledi na kuweka mbele maslahi ya Taifa kwa manufaa ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kutoka vyama vyote waliochaguliwa na Bunge hili kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki. Matarajio yetu ni kuwa watalinda na kusimamia lakini pia kutetea vema maslahi ya nchi yetu katika Bunge hilo la Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa maelekezo na ushauri wa kizalendo waliotupatia, ambao umesaidia kuboresha taarifa za mwenendo wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2017/2018 ninazoziwasilisha sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hotuba ninayoiwasilisha imegawanyika katika maeneo makuu matano. Eneo la kwanza ni utangulizi, la pili ni taarifa ya mapitio ya hali ya uchumi kwa mwaka 2016 na robo ya kwanza ya 2017, eneo la tatu, ni muhtasari wa mapitio ya utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017, eneo la nne, ni maeneo ya kipaumbele ya mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2017/2018 na mwisho ni majumuisho.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nianze kueleza mwenendo wa hali ya uchumi kwa mwaka 2016 nikianza na uchumi wa dunia. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia katika mwaka 2016 ilikuwa ni asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2015. Kupungua huku ni matokeo ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea ambapo ukuaji wa uchumi kwa nchi hizo kilikuwa asilimia 1.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2015, ikichangiwa na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma katika masoko mengi duniani na kupungua kwa tija ya uzalishaji na kasi ya uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 4.1 sawa na ilivyokuwa mwaka 2015. Ukuaji huu wa nchi zinazoendelea ulichangiwa zaidi na kupungua kwa ukuaji wa uchumi katika nchi za China na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kufuatia kuporomoka kwa bei za bidhaa na hasa bidhaa ghafi katika soko la dunia; kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa zinazozalishwa katika masoko mengi duniani.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei duniani uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 2.8 mwaka 2015. Kwa kiasi kikubwa mfumuko wa bei uliongezeka kutokana na kulegezwa kwa sera za bajeti na fedha kwa baadhi ya nchi na ukame uliochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo inayojulikana kama *La Nina*. Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka kufikia asilimia 0.8 kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 0.3 mwaka 2015, ambapo kwa nchi zinazoendelea za Asia, uliongezeka hadi asilimia 3.1 kutoka asilimia 2.7 mwaka 2015. Katika nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, mfumuko wa bei ulifikia asilimia 11.4 ikilinganishwa na asilimia saba mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, uchumi wa Afrika na katika Kanda nzima. Kwa upande wa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kasi ya ukuaji wa uchumi ilipungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi asilimia 1.4 mwaka 2016. Hii ni kutokana na kupungua kwa upatikanaji wa mikopo kutoka kwenye masoko ya Kimataifa uliosababisha miradi iliyopangwa katika kipindi hicho kushindwa kukamilika, kuendelea kwa migogoro ya kisiasa katika baadhi ya nchi na hususani Burundi, Libya, Chad, Sudan Kusini na DRC na kuporomoka kwa bei za baadhi ya mazao ghafi na hasa dhahabu na mafuta ya petroli.

Mheshimiwa Spika, kasi ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ilishuka kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2015 hadi asilimia 5.3 mwaka 2016 ijapokuwa Jumuiya hii iliendelea kuongoza kwa ukuaji miongoni mwa Jumuiya mbalimbali za Afrika. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya hii ilichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei ya bidhaa na kudorora kwa uchumi wa dunia.

Maoteo ya mwenendo wa uchumi katika ukanda huu yanaonesha utakua kwa wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2017 na asilimia sita mwaka 2018. Matarajio haya yanazingatia hatua zinazochukuliwa na nchi za ukanda huu katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara



kama vile kuwa na maeneo tengefu ya ujenzi wa viwanda na hususani viwanda vya nguo, bidhaa za ngozi, kilimo, madawa na vifaa tiba.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei katika nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2016 uliendelea kuwa wa kiwango cha tarakimu moja, ambapo Rwanda ilikuwa na asilimia 7.1, Uganda asilimia 5.4, Tanzania asilimia 5.2, Kenya asilimia 6.3 na Burundi asilimia 5.6. Aidha, kufikia Machi 2017, mfumuko wa bei wa nchi hizi ulipanda ambapo kwa Burundi ulifikia asilimia 21.1, Rwanda asilimia 13, Kenya asilimia 10.28, Uganda asilimia 6.4 na Tanzania asilimia 6.4. Hali hii ilichangiwa na ukame katika maeneo mengi ya ukanda huu kutokana na kuchelewa kwa msimu wa mvua.

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika yaani *SADC*, kasi ya ukuaji wa uchumi ilishuka kutoka wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2015 hadi asilimia 1.1 mwaka 2016 na kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya hii ilichangiwa na uhaba wa nishati ya umeme pamoja na ukame uliochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa. Licha ya kasi ndogo ya ukuaji, Jumuiya hii iliendelea kuwa ya tatu katika ukuaji miongoni mwa Jumuiya Barani Afrika na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2017. Mfumuko wa bei ulifikia asilimia 10.5 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.7 mwaka 2015, ukichangiwa na ukame na kuyumba kwa utekelezaji wa sera za mapato na matumizi kwa baadhi ya nchi wanachama. Matarajio ni kuwa mwaka 2017 mfumuko wa bei utapungua hadi kufikia asilimia 8.7 kutokana na kushuka kwa gharama za bidhaa, kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya umeme na udhibiti wa bei ya mafuta na kuimarika kwa hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kueleza juu ya uchumi wa Taifa na nitaanza na ukuaji wa uchumi na Pato la Taifa. Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia saba mwaka 2016, kama ilivyokuwa mwaka 2015. Kiwango hiki hata hivyo ni chini ya maoteo ya kufikia asilimia 7.2 kutokana na ukuaji wa baadhi ya shughuli kushindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji. Baadhi ya shughuli za kiuchumi ambazo

zilishindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji ni pamoja na sekta ya kilimo iliyokua kwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 2.9; biashara na matengenezo asilimia 6.7 ikilinganishwa na asilimia 7.8 za maoteo; huduma za malazi na chakula asilimia 3.7 kinyume na maoteo ya asilimia 8 na huduma za utawala asilimia 2.1 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 6.3.

Mheshimiwa Spika, aidha, zipo shughuli za kiuchumi zilizokua na hata kuzidi maoteo. Shughuli za kiuchumi zilizokuwa na viwango vikubwa ni pamoja na habari na mawasiliano ambayo ilikua kwa asilimia 13 dhidi ya maoteo ya asilimia 12; usafirishaji na uhifadhi wa mizigo ilikua kwa asilimia 11.8 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 8; uchimbaji madini na mawe ulikua kwa asilimia 11.5 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 9.2 na uzalishaji viwandani ulikua kwa asilimia 7.8 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 6.7.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kissekta katika pato la Taifa. Mchango wa shughuli za kilimo katika pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka 2015. Shughuli za viwanda na ujenzi ndiyo zilichangia asilimia 25.2 ya Pato la Taifa mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 24.3 mwaka 2015, ambapo mchango wa sekta za huduma ikijumuisha biashara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo, malazi, habari na mawasiliano, fedha, bima na upangishaji majumba, elimu na afya ulikuwa asilimia 39.1 katika mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 40 mwaka 2015. Kuongezeka kwa mchango wa shughuli za viwanda ni dalili kuwa azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda imeanza kuleta matokeo chanya ambapo tija na uzalishaji viwandani unaimarika. Pamoja na mengine hii inatokana na kuimarika kwa upatikanaji wa miundombinu na hasa nishati na usafiri.

Mheshimiwa Spika, wastani wa pato la kila mtu. Pato la Taifa kwa mwaka 2016 lilifikia shilingi 103,744,606 kwa bei za mwaka husika na kiasi hiki cha pato ukikigawanya kwa idadi ya watu wanaokadiriwa kuwepo Tanzania Bara ambao ni 48,676,698, inafanya wastani wa pato la kila mtu kufikia

shilingi 2,131,299 ikilinganishwa na shilingi 1,918,897 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Hata hivyo, katika thamani ya dola za Kimarekani, wastani wa pato la kila mtu liliongezeka kidogo kutoka dola za Kimarekani 967.5 mwaka 2015 hadi dola za Kimarekani 979.1 mwaka 2016, ikimaanisha kuwa bado tuna hatua ili kuingia katika kundi la uchumi wa kati. Kiwango cha chini cha uchumi wa kati ni takribani dola za Kimarekani 1,043. Hivyo basi, kasi ya ongezeko la pato la mwananchi katika thamani za dola halinabudi kuongezeka na hii itawezekana kwa kutanzia changamoto zilizopo hasa uzalishaji na tija katika sekta zinazoajiri wananchi wengi, kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa bei; kwa miaka minne mfululizo, wastani wa mfumuko wa bei nchini umeendelea kupungua, ukibaki katika kiwango cha tarakimu moja. Katika mwaka 2016, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2015. Kupungua kwa wastani wa mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na mwenendo wa kushuka wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na nchini, kuimarika kwa upatikanaji wa vyakula na kuwepo kwa sera madhubuti za usimamizi wa kibajeti na fedha.

Mheshimiwa Spika, mfumuko wa bei uliongezeka kidogo ambapo ulifikia asilimia 6.4 mwezi Aprili, 2017 na hivi jana takwimu mpya zilitoka mfumo wa bei kwa mwezi Mei umeshuka tena na kufikia asilimia 6.1. Hali ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei nchini ilichangiwa na hofu iliyotokana na kuchelewa kwa msimu wa mvua katika maeneo mengi nchini na hivyo kuwepo kwa taharuki ya kutokea upungufu wa chakula. Hata hivyo, maeneo mengi yamepata mvua ya kutosha na hivyo bei ya chakula nchini inatarajiwa kuimarika.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viwango vya riba; katika mwaka 2016 viwango vya riba za amana na mikopo vilipungua ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Riba za amana za muda mfupi zilipungua kutoka wastani wa asilimia 9.3 hadi asilimia 8.78. Viwango vya riba za amana za mwaka

mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 11.16 mwaka 2015 hadi asilimia 11.03 mwaka 2016. Vilevile viwango vya riba za mikopo ya hadi mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.22 hadi kufikia asilimia 12.87 mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu ulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa kibenki. Kufuatia hali hiyo, tofauti ya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kufikia asilimia 1.8 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 3.06 mwaka 2015. Hata hivyo, riba ya mikopo baina ya benki iliongezeka kufikia wastani wa asilimia 13.49 mwezi Disemba 2016 kutoka asilimia 7.29 kwa muda kama huo mwaka 2015. Riba kwa dhamana za Serikali ilipungua kutoka asilimia 18.25 mwezi Disemba 2015 kufikia wastani wa asilimia 15.12 mwezi Disemba 2016.

Mheshimiwa Spika, kufikia Machi, 2017 riba za amana za muda maalum ziliongezeka kidogo kuwa asilimia 10.89 na riba za amana za mwaka mmoja kufikia asilimia 12.03. Wakati huo huo, riba za mikopo ya hadi mwaka mmoja ziliongezeka kufikia asilimia 18.07. Ongezeko hili la riba za mikopo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2017 kunatokana na mabenki kuchukua tahadhari dhidi ya kuongezeka kwa makadirio ya mikopo chechefu na kupunguza maoteo ya faida. Kuongezeka kwa riba za amana kulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa kibenki katika kuvutia amana. Kwa upande mwingine, riba za mikopo baina ya benki zilipungua kufikia wastani wa asilimia 8.16 na kwa dhamana za Serikali asilimia 14.52.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa amana katika benki za biashara; kwa mwaka 2016 amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 2.3 kufikia shilingi bilioni 19,729.5 kutoka shilingi bilioni 19,293.7 mwaka 2015. Kati ya amana hizo, sekta binafsi ilichangia asilimia 97.1 ikilinganishwa na asilimia 95.6 mwaka 2015. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote ulipungua kufikia asilimia 31.6 mwaka 2016 kutoka asilimia 32.8 mwaka 2015. Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2017 amana katika benki za

biashara ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 19,853.4 ambapo sekta binafsi ilichangia asilimia 96.4.

Mheshimiwa Spika, mwenendo wa mikopo katika sekta binafsi; mikopo ya mablenki kwa sekta binafsi kwa mwaka 2016 iliongezeka kwa asilimia 7.2 kufikia shilingi bilioni 16,608.9 ikilinganishwa na shilingi bilioni 15,492.7 mwaka 2015. Ukuaji huu ulikuwa chini ya kiwango cha mwaka 2015 cha asilimia 24.8. Kiasi cha mikopo kilichotolewa kwa sekta binafsi mwaka 2016 kilifikia asilimia 16.2 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 17.1 mwaka 2015. Kiwango cha mikopo kilichotolewa kwa shughuli za uzalishaji, kilimo, uchukuzi na mawasiliano, viwanda, huduma za kifedha, umeme, majengo na ujenzi, kilipungua mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, wakati huo huo, mikopo ya shughuli za madini na uchimbaji mawe, biashara, utalii, hoteli na migahawa na shughuli binafsi iliimarika, japo kwa kasi ndogo. Mikopo iliyoelekezwa katika shughuli za biashara, ilikuwa asilimia 21 ya mikopo yote na shughuli binafsi asilimia 18.6. Mwenendo huu ulichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa ukwasi katika mablenki kutokana na tahadhari zilizochukuliwa na mablenki kufuatia kuongezeka kwa makisio ya viwango vya mikopo chechefu (*non performing loans*) na kupungua kwa maoteo ya faida.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2017, mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi iliendelea kuimarika, ikiongezeka kwa shilingi bilioni 77.4 kufikia shilingi bilioni 16,686.3. Hizi ni ishara njema za kuanza kuimarika kwa uchumi na shughuli za sekta binafsi na hususan za uzalishaji viwandani, majengo, mahoteli na migahawa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ukuzaji wa rasilimali, Tanzania ni mojawapo wa nchi chache za Afrika zilizojipambanua kuwa na utulivu wa uchumi jumla kwa muda mrefu sasa. Hii ikiwa ni pamoja na kuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei wa wastani na mwenendo wa thamani ya shilingi umekuwa thabiti. Hali hii

imekuwa kishawishi kikubwa cha mitaji kutoka nje kuja nchini. Katika mwaka 2016, ukuzaji rasilimali kwa bei za miaka husika uliongezeka kwa asilimia 3.4 kutoka shilingi 24,717,206 mwaka 2015 hadi shilingi 25,558,140. Hata hivyo, uwiano wa ukuaji rasilimali na pato la Taifa kwa bei za miaka husika ulipungua kufikia asilimia 24.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 27.2 mwaka 2015. Kiwango cha ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007 kilipungua kwa asilimia 4.3 kutoka shilingi 13,733,585 mwaka 2015 kufikia shilingi 13,140,451 mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, sekta ya nje; kwa mwaka 2016, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma kati ya Tanzania na nchi mbalimbali uliendelea vizuri. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 4.1 kufikia dola za Marekani milioni 9,285.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na dola za Kimarekani milioni 8,918.1 mwaka 2015. Aidha, uagizaji wa bidhaa na huduma nje ulipungua kwa asilimia 14.0 kwa mwaka 2016 kutoka dola za Kimarekani 12,528.2 mwaka 2015 kufikia dola za Marekani milioni 10,772.3. Mwenendo huo ulitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa nyingi zilizoagizwa kutoka nje isipokuwa kwa malighafi za viwandani zilizoongezeka ikichangiwa pia na kupungua kwa gharama za usafirishaji, huduma zitolewazo na Serikali na huduma nyingine za kibiashara.

Mheshimiwa Spika, biashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ziliendelea kuimarika na masoko kubadilika ambapo kwa mwaka 2016 sehemu kubwa ya mauzo yote nje ya nchi yalikuwenda katika nchi za Uswisi (asilimia 16.2), India (asilimia 12.4), Afrika ya Kusini (asilimia 12.2), China (asilimia 6.2), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (asilimia 5.6) na Kenya (asilimia 5.5).

Mheshimiwa Spika, hii inaonesha kuwa kumekuwa na mabadiliko kutoka masoko asilia kama vile Uingereza, Ujerumani na Canada. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi nchini Uswiss na India ni pamoja na dhahabu, mbegu za mafuta, vito vya thamani na mboga mboga. Bidhaa zilizouzwa Kenya zilikuwa ni chai, mahindi, vifaa vya ushonaji, mboga mboga na nafaka.

Vilevile bidhaa zilizouzwa Afrika ya Kusini zilikuwa dhahabu, madini ya shaba na chai. Pamoja na maendeleo haya, mauzo mengi nje ya nchi yaliendelea kuwa ya mazao ghafi yasiyongezwa thamani na hivyo kupata thamani ndogo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje, kiasi kikubwa kilitoka katika nchi za China, India, Falme za Nchi za Kiarabu, Afrika ya Kusini, Japan na Kenya, nchi ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 60.6 ya bidhaa zote zilizoagizwa. Bidhaa zilizoagizwa kutoka China ni pamoja na mitambo na bidhaa za marumaru, kwa Falme za Nchi za Kiarabu ni mafuta ya petroli na sukari na kwa upande wa Japan na Afrika ya Kusini ni magari na bidhaa za chuma, kuonesha kuwa uzalishaji nchini bado unategemea vipuri, malighafi na mitambo kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kufuatia mwenendo wa biashara kwa mwaka 2016, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,489.5, ikipungua kwa asilimia 58.6 kutoka nakisi ya dola za Marekani milioni 3,594.7 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, hali hii kwa kiasi kikubwa ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Hivyo, urari wa malipo yote kwa mwaka 2016, ukijumuisha urari wa biashara ya bidhaa na huduma, mapato ya vitega uchumi, uhamisho wa mali, malipo ya kawaida, uhamisho wa mitaji na malipo ya fedha katika uwekezaji, ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 305.5 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 199.1 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Januari hadi Machi, 2017, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia dola za Marekani milioni 2,224.8, ikichangiwa kwa kiasi kikubwa na mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia hasa huduma za utalii, dhahabu, bidhaa za mboga mboga na matunda.

## *NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

Aidha, katika kipindi hicho, uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ulikuwa dola za Marekani milioni 2,203.6 na hivyo kuendelea kuwa na ziada katika urari wa akaunti ya biashara ya bidhaa na huduma.

Mheshimiwa Spika, akiba ya fedha za kigeni na thamani ya shilingi; hadi kufikia Disemba 2016, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 4,325.6 ikilinganishwa na dola milioni 4,093.7 Disemba, 2015. Kiasi hicho kilikuwa kinaweza kulipia gharama za kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.2.

Mheshimiwa Spika, kufikia Machi 2017, akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Kimarekani milioni 4,482.6, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.3. Kuongezeka kwa akiba ya fedha za kigeni kumesaidia kurejesha utengamavu wa thamani ya shilingi.

Katika kipindi cha mwaka 2016 mwenendo wa thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ulikuwa wa kuridhisha ukipungua kwa wastani wa asilimia 8.8 tu ambapo dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 2,177.07 ikilinganishwa na shilingi 1,991.4 mwaka 2015.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Machi, 2017, dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 2,223.9 kutoka shilingi 2,172.6 ilivyokuwa ikinunuliwa mwishoni mwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, mabadiliko ya maisha ya watu; kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012 Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 2.7 kwa mwaka ambapo kufikia mwaka 2016 ilikadiriwa kuwa na watu 48,676,698.

Mheshimiwa Spika, kwa makadirio haya, Tanzania inakuwa ni nchi ya tano kwa idadi ya watu Barani Afrika ikitanguliwa na Nigeria, Ethiopia, Misri na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.



Mheshimiwa Spika, idadi kubwa ya watu na kasi ya ongezeko imekuwa ni changamoto kubwa katika harakati za kupunguza umaskini na kuimarisha utoaji wa huduma. Kwa kuzingatia hili, Serikali imeendelea kuongeza na kuboresha upatikanaji wa elimu msingi hususan kwa wasichana. Kwa upande mwingine, idadi kubwa ya watu imekuwa ni fursa kwa maana ya soko la bidhaa na huduma, ikiwa itaendana na maendeleo ya stadi, teknolojia, ujasiriamali na pato la kila mwananchi.

Mheshimiwa Spika, licha ya hatua hizi, bado kumekuwa na changamoto nyingine kufuatia kasi kubwa ya uhamiaji mijini ambapo kwa sasa takribani asilimia 30 ya watu nchini wanaishi mijini. Kasi hii ya mabadiliko ya idadi ya watu na uhamiaji mijini inadunisha kasi ya kuboresha upatikanaji wa nyumba na makazi yaliyopangwa na pia utoaji wa huduma zinazoendana na idadi ya wakazi katika miji yetu.

Mheshimiwa Spika, katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeendelea kuimarisha upimaji wa maeneo ya makazi, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuchukuwa hatua zinazolenga kuinua tija na faida katika shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, hatua hizo ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani, pembejeo, zana za kilimo, masoko, miundombinu ya umwagiliaji na kuondoa utitiri wa kodi katika shughuli za kilimo. Hatua pia zimeendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na uendeshaji wa shughuli za viwanda na biashara hasa vijijini. Lengo ni kupanua fursa za ajira mbadala kwa wakazi wa vijijini, ikiwa ndiyo njia ya kuaminika zaidi katika kudhibiti kasi ya watu kuhamia mijini. Huduma za mafunzo ya ufundi stadi zimezidi kuimarishwa ili wale wanaohamia mijini waweze kuajirika na kujajiri kwa urahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ustawi wa jamii, maisha ya watu yameendelea kuboreka kama inavyohibitishwa na taarifa ya Umoja wa Mataifa ya

Maendeleo ya Watu kwa mwaka 2016 ambapo kwa kigezo cha Fahirisi ya Maendeleo ya Watu (*Human Development Index*), ustawi wa Watanzania umeendelea kuimarika kutoka alama 0.521 mwaka 2014 hadi alama 0.531 mwaka 2015. Kigezo hiki huzingatia viashiria kadhaa vya maendeleo na ustawi na hasa muda wa kuishi baada ya kuzaliwa, elimu, ustawi wa kipato cha mwananchi. Kwa kutumia kigezo hiki, Tanzania ni nchi ya pili kwa ustawi wa maisha ya wananchi katika Ukanda wa Afrika Mashariki baada ya Kenya iliyofikia alama 0.555 katika kipindi hiki. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mafanikio ya Tanzania ni matokeo ya jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii katika elimu, afya, maji safi na salama na umeme katika maeneo ya vijijini na mijini. Mfano, idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme hadi Machi, 2017 ilifikia asilimia 67.5 ikilinganishwa na asilimia 40 iliyokuwa imefikiwa Aprili, 2016.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ya mijini, idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme ilifikia asilimia 97.3 Machi 2017 ikilinganishwa na asilimia 63.4 mwaka 2014/2015 na upande wa maeneo ya vijijini ilifikia asilimia 49.5 Machi, 2017 ikilinganishwa na asilimia 21.0 mwaka 2014/2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upatikanaji wa maji, idadi iliongezeka kutoka watu 21,900,000 Juni 2016 hadi 22,951,371 Machi, 2017. Kumekuwa na mafanikio pia kwa upande wa elimu ambapo uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza uliongezeka kutoka milioni 1.5 mwaka 2014 hadi milioni 2.1 mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, vilevile idadi ya wananchi wanaonufaika na huduma ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*NHIF*) imeongezeka kutoka 3,377,023 mwaka 2015/2016 hadi 3,880,088 Machi 2017. Wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*) wameongezeka kutoka 8,717,130 mwaka 2015/2016 hadi kufikia wanufaika 9,573,906 Machi, 2017. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na kupunguza umaskini wa mahitaji ya msingi, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa idadi ya Watanzania wanaokosa mlo mmoja kwa siku au kuishi kwa mlo mmoja inapungua kutoka kiwango cha asilimia 9.7 kwa sasa kufikia asilimia 5.4 na asilimia 4.4 ifikapo mwaka 2020 na mwaka 2025 kwa mtiririko huu.

Mheshimiwa Spika, hatua zinazochukuliwa kufikiwa lengo hili ni pamoja na kuimarisha uzalishaji na hivyo upatikanaji wa chakula katika kaya, kuongeza fursa za ajira mijini na vijijini, kuendelea na mpango wa kusaidia kaya maskini na kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wajasiriamali kuipitia mifuko ya maendeleo ya vijana, Wanawake na wajasiriamali wadogo.

Mheshimiwa Spika, licha ya mafanikio yaliyofikiwa kiwango cha umaskini kwa maeneo ya vijijini bado ni kikubwa ikilinganishwa na maeneo ya mijini. Umaskini vijiji umepungua kutoka asilimia 39.4 mwaka 2007 hadi asilimia 33.3 mwaka 2012, ikimaanisha kuwa japo vijijini umaskini unapungua lakini bado ni chini ya wastani wa kitaifa. Sababu yake ni kuwa kasi ya ukuaji wa uchumi haijagusa kundi kubwa la wananchi vijijini ambao wengi hutegemea shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi.

Mheshimiwa Spika, Sekta hizi ambazo ndizo msingi wa ustawi wa maisha ya wananchi vijiji zimekuwa na tija na kasi ndogo ya ukuaji kwa kipindi chote. Shabaha ya Serikali ni kupunguza wastani wa umskini vijijini kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 33.3 hadi asilimia 19.3 na asilimia 15 mwaka 2020 na mwaka 2025 kwa mtiririko huu.

Mheshimiwa Spika, kipimo cha mgawanyo wa kipato miongoni mwa wananchi (*Gini coefficient*) kwa upande wa Tanzania Bara kinaonesha kuwa tofauti ya kipato imepungua kutoka 0.37 mwaka 2006/2007 hadi 0.34 mwaka 2011/2012. Hata hivyo, tofauti ya kipato kati ya Jiji la Dar es Salaam na maeneo mingine na ile ya maeneo ya vijijini ni kubwa zaidi na hali hii imechangiwa na tofauti ya upatikanaji wa

huduma, miundombinu, fursa za ajira, athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi katika shughuli msingi za jamii husika.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria Tanzania ya mwaka 2015/2016, vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 51 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/2016. Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/2016. Kushuka kwa viashiria hivi kunatokana na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii ikiwemo afya ya uzazi na mama na mtoto nchini. Maelezo ya kina kuhusu hali ya uchumi yapo katika kitabu cha hali ya uchumi kwa mwaka 2016.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa Taifa wa mwaka 2016/2017. Mwaka 2016/2017 ulikuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mpango huu utatekelezwa hadi 2020/2021, ambapo msukumo ni kuchochea mageuzi ya uchumi kupitia ujenzi wa uchumi wa viwanda na kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu na kwa kuzingatia hili, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/2017 ulijielekeza katika maeneo makuu manne ya kipaumbele, ikiwa ni:-

(i) Kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda.

(ii) Kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu.

(iii) Kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji.

(iv) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa 2016/2017 umefafanuliwa kwa kina katika

hotuba za mipango na bajeti za Mawaziri wa sekta husika na kwa maana hiyo nitajikita kuelezea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi tu ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, kwanza nianze na miradi iliyopewa msukumo wa kipekee; hii ni miongoni mwa miradi ya kimkakati iliyobainishwa kwa utekelezaji katika mpango wa maendeleo wa miaka mitano na utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i) Ujenzi wa reli ya kati; tulisaini mkataba wa kusanifu na kujenga awamu ya kwanza ya mradi kutoka Dar es Salaam mpaka Morogoro kilomita 205 ambapo mkandarasi ameanza maandalizi ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa kambi, ofisi pamoja na kiwanda cha kukarabati mataruma. Mkandarasi amelipwa shilingi bilioni 300 malipo ya awali na Mheshimiwa Rais alizindua kazi ya ujenzi tarehe 12 Aprili 2017.

Mheshimiwa Spika, taratibu zinazoendelea ni kupata fedha na kuendelea na ujenzi sehemu za reli zilizobakia. Kwa sehemu ya Morogoro hadi Makutupora kilometa 336, Serikali inaendelea na mazungumzo na Mkandarasi aliyepatikana na kwa sehemu za Makutupora hadi Tabora kilomita 294, Tabora hadi Isaka kilomita 133 na Isaka hadi Mwanza kilomita 249, Serikali ipo kwenye mazungumzo na baadhi ya mabanki ambayo yameonesha nia ya kutoa mkopo nafuu kwa ajili ya ujenzi. *(Makofi)*

(ii) kuboresha shirika la ndege Tanzania; ndege mbili zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja zilinunuliwa na zilianza kutoa huduma tangu Oktoba 2016. Vilevile, maandalizi ya ununuzi wa ndege nyingine nne yamekamilika na mikataba imesainiwa, ambapo malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 56.89 tayari yamefanyika. Kati ya ndege hizo, moja inategemewa kuwasili Julai, 2017; mbili zinategemewa kuwasili Juni, 2018 na ya mwisho, ambayo itakuwa ya masafa marefu yenye uwezo wa kubeba abiria 262 inategemewa kuwasili Julai, 2018.

(iii) Makaa ya mawe Mchuchuma na Chuma Liganga; maandalizi yote ya ujenzi wa miradi hii yamekamilika, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Vilevile, kampuni ya *Sichuan Hongda Corporation Limited*, ambayo ndio mbia katika miradi hii, wametenga jumla ya Dola za Kimarekani milioni 300 kwa ajili ya kulipia sehemu ya mtaji yaani *equity* katika miradi. Mfumo uliokubalika na pande zote mbili ni mwekezaji kujenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuuendesha (*Build, Own and Operate - BOO*). Mahusiano ya umeme kwa *TANESCO* hayatajumuisha gharama za uwekezaji.

(iii) Mradi wa bomba la mafuta kutoka Hoima Uganda mpaka Bandari ya Tanga, hatua iliyofikiwa ni pamoja na kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya awali, kutolewa kwa vivutio vya kodi, kusainiwa kwa *Inter-Governmental Agreement*, kufanyika kwa tathmini ya njia ya bomba, kufanyika kwa tathmini ya mahitaji ya njia ya bomba, kufanyika kwa tathmini ya masuala ya kijamii na mazingira, kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa gati ya kupokelea mafuta Chongoleani katika bandari ya Tanga na kutangazwa kwa zabuni za kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya uchunguzi wa udongo.

(iv) Ununuzi na ukarabati wa meli kwenye Maziwa Makuu; hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika ziwa Victoria na ukarabati mkubwa wa *Mv. Victoria* na *Mv. Butiama*. Kwa upande wa *Mv. Liemba* katika ziwa Tanganyika, mjenzi amepatikana ambaye ni *M/S LEDA SHIPYARD*. Ujenzi wa meli mbili za mizigo ziwa Nyasa umekamilika. (*Makofi*)

(v) Uanzishwaji wa shamba la miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi; Shilingi billioni mbili tayari zimewekezwa katika mradi huu. Kazi zilizofanyika ni pamoja na kupima ubora wa udongo, vitalu vya mbegu za miwa vimeandaliwa na taratibu za kupata huduma ya wataalam wa kufanya

upembuzi yakinifu, uchunguzi wa mbegu za miwa, tathmini ya athari za mazingira na ujenzi wa barabara za kuingia katika eneo la mradi zinaendelea.

(vi) Ujenzi wa mitambo ya kusindika gesi kimiminika; hatua iliyofikiwa ni pamoja na kupatikana kwa eneo la mradi ambalo ni Likong'o Mkoani Lindi, kuundwa kwa timu ya majadiliano na kuandaliwa kwa hadidu za rejea, kupitia nyaraka muhimu zinazohusu mradi yaani sera, Sheria, mikataba, Kanuni na mikakati ya Serikali na kuanza kwa majadiliano na kampuni zinazoshiriki katika mradi juu ya masuala yatakayozingatiwa katika kuandaa mkataba kati ya kampuni husika na Serikali yaani *Host Government Agreement (HGA)*

(vii) Uendelezaji wa maeneo maalum ya kiuchumi ukianza na:-

(a) Kituo cha biashara cha Kurasini; kiasi cha fidia kilicholipwa kwa ajili ya kupata eneo la mradi ni Shilingi bilioni 101.04 na wananchi 1,019 tayari wamelipwa fidia. Eneo hili kwa sasa lipo chini ya umiliki wa Serikali kwa asilimia 100 na hivyo maandalizi ya mpango mahsusi wa uwekezaji katika eneo hilo yanaendelea.

(b) Eneo maalum la uwekezaji la Bagamoyo; Shilingi bilioni 26.66 zimetumika kulipa fidia kwa wananchi 1,155 kati ya wananchi 2,273 wanaopaswa kupisha mradi kwenye eneo la hekta 2,339.6.

(c) Kwa upande wa eneo maalum la uwekezaji Mtwara; tayari eneo la hekta 10 kati ya hekta 110 za eneo lililotengwa kwa ajili ya Mtwara *Special Economic Zone (SEZ)* limetangazwa kwa ajili ya matumizi ya bandari huru yaani *Free Port Zone* na maandalizi ya kuweka miundombinu, hususan barabara, kwa eneo hilo yanaendelea.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kujenga msingi wa uchumi wa viwanda; katika kutekeleza azma hiyo mwelekeo umeanza kuwa mzuri. Miradi ya viwanda

mbalimbali imeanzishwa kutokana na mchango wa sekta binafsi katika Mikoa mbalimbali nchini. Kwa mfano kwa Mkoa wa Pwani una jumla ya miradi mipya ya viwanda 82. Aidha, baadhi ya miradi mikubwa ya viwanda iliyoinduliwa na kuwekwa mawe ya msingi kwa Mkoa wa Pwani pekee ni pamoja na:-

Viwanda viwili vya *Tywford Tiles* Chalinze na *Goodwill Ceramic* Mkuranga vya kutengeza marumaru, Kiwanda cha nondo cha Kiluwa *Steel Industries Limited* Mlandizi Pwani ambacho kimeanza uzalishaji; Kiwanda cha *Global Packaging* Maillimoja Pwani ambacho kinafanya kazi; Kiwanda cha kutengeneza Juisi ya Matunda cha Bakhresa *Food Product Limited* - Mkuranga ambacho kimezinduliwa na kinafanya kazi; Kiwanda cha *Elyven Agric Company Limited* - Bagamoyo; Kiwanda cha Juisi cha Sayona *Fruits Limited* (Mboga Pwani); na Kiwanda cha *KEDS Tanzania Company Limited* - Kibaha Pwani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali imekuwa na mchango mkubwa kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda hivi, ikiwa ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa ardhi, kuweka miundombinu inayohitajika na kutoa vibali vya ujenzi lakini pia vivutio. Halmashauri na Serikali za Mitaa katika maeneo haya zimekuwa na msaada na ushirikiano mkubwa kwa wawekezaji ikiwemo kutoa maeneo ya viwanda ili kuhamasisha uwekezaji.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi wa Mikoa, Wilaya, Halmashauri na Serikali za Mitaa walioitikia kwa dhati wito wa Serikali wa kujielekeza katika kuvutia na kuwawezesha wawekezaji. Pia nitumie nafasi hii kuwapongeza sana wawekezaji wetu ambao wamejitokeza kuwekeza katika viwanda. Serikali inawaomba viongozi wa Halmashauri zote nchini kuiga mfano wa wenzao katika Mkoa wa Pwani wanaofanya jitihada zote katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinaandaa mazingira mazuri na maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya sekta binafsi. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, Serikali pia kupitia mashirika yake mbalimbali imeanza kuwekeza katika ujenzi wa viwanda, mwitiko wa kipekee na wa kupongezwa ni wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ambapo *PPF* na *MSSF* wanashirikiana kuwekeza katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari katika eneo la Mkulazi na Mbigiri Mkoani Morogoro. Pia *LAPF* wanajenga machinjio ya kisasa ya nyama pale kwa Makunganya Morogoro. Shirika la Taifa la Maendeleo *NDC* linashirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya uwekezaji katika eneo la viwanda la *TAMCO* Kibaha kwa uendelezaji wa viwanda vya nguo na uunganishaji wa magari na matrekta, ambapo kiwanda cha kuunganisha matrekta kimefikia hatua ya kuanza majaribio.

Mheshimiwa Spika, hatua nyingine zinazoendelea chini ya *NDC* ni pamoja na jitihada za kufufua Kiwanda cha *General Tyre - Arusha*, hatua za awali za uwekezaji katika mradi wa uchenjuaji wa magadi soda katika Bonde la Engaruka. Vile vile *NDC* kwa ubia na kampuni ya *TCIMRL* ya China imewekeza katika miradi ya Mchuchuma na Liganga.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa miundombinu na mazingira wezeshi; ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji miundombinu ya uhakika. Hivyo, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha miundombinu na huduma za uchumi wa viwanda. Miongoni mwa miradi hii ni ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II, megawati 240; upanuzi wa mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi I; ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 400 Iringa – Singida – Shinyanga; kV 220 Makambako – Songea (km 250); na *North West Grid* kV 400; usambazaji umeme Vijijini na Makao Mkuu ya Wilaya *REA Turnkey Phase III*, ambapo wateja 146, 831 sawa na asilimia 58.7 ya lengo wameunganishwa, lakini ukarabati wa njia ya reli ya kati.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa barabara hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Masasi – Songea – Mbambabay, sehemu ya Namtumbo – Tunduru kilomita 193; na Tunduru – Mangaka – Mtambaswala kilomita 202.5; barabara ya Dodoma – Babati kilomita 261; Bagamoyo

– Msata na daraja la Ruvu chini; na kukamilika kwa Daraja la Kilombero katika barabara ya Ifakara – Mahenge. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi unaendelea na umefikia asilimia 16.4 na ujenzi wa barabara za juu za TAZARA na *Interchange* ya Ubungo umeanza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; Serikali inaendelea kutekeleza sera ya Elimu Msingi bila malipo; uboreshaji wa miundombinu na huduma za kujifunzia na kufundishia; kukamilika kwa ujenzi wa mabweni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Mloganzila; na kukamilika kwa ukarabati wa Vyuo vya Ualimu kumi.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha ujuzi na stadi za kazi, Serikali imekamilisha matayarisho ya sera ya Taifa ya ajira ya mwaka 2017, miongozo ya mafunzo kazini kwa vitendo kwa wanafunzi (*apprenticeship framework*) na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu yaani *internship framework*. Vilevile, Serikali imeingia mikataba na viwanda vya *TOOKU Garment* na *Mazava Fabrics* kwa ajili ya kutoa mafunzo ya stadi za ubunifu na ushonaji wa nguo viwandani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyozingatiwa ni pamoja na kupanua miundombinu ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini, huduma za afya na upimaji wa maeneo ya makazi.

Mheshimiwa Spika, maeneo mengine yaliyoendelea kutekelezwa ni yale yaliyotoa fursa za ajira na ushiriki wa wananchi wengi katika shughuli za uchumi wa viwanda, ikiwa ni pamoja na kuandaliwa kwa programu ya muda mrefu na mfupi ya upimaji na umilika kwa ukarabati wa maghala 106 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Mbeya, Songea, Kalambo, Mbozi, Momba na Njombe na kuingizwa nchini kwa tani 231,140 za mbolea.

Mheshimiwa Spika, katika kuhamishia Shughuli za Serikali Kuu Dodoma; awamu ya kwanza imekamilika ambapo majengo ya ofisi za Wizara katika kipindi cha mpito na nyumba za makazi kwa baadhi ya viongozi zimepatikana. *TBA* na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma wanaendelea na kukamilisha ukarabati wa nyumba za makazi na ofisi. Vilevile, Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inaendelea na upimaji wa viwanja vya makazi na ofisi, ambapo watumishi wa umma wameandaliwa mkakati maalum utakaosaidia upatikanaji wa viwanja kwa ajili ya makazi.

Mheshimiwa Spika, aidha, Shirika la Nyumba la Taifa linaendelea na ujenzi wa nyumba mpya 300 za makazi na zinazotarajiwa kukamilika Septemba, 2017. Kwa upande mwingine, Serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni binafsi kutoka Switzerland, China na Zimbabwe pia Makampuni ya ndani ambayo yameonesha nia ya kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya maji kwa Mji Mpya wa Dodoma. Taasisi za Serikali kama vile *TBA*, *TANESCO*, *SUMATRA*, *TEMESA*, *TANROADS*, *TTCL* na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma zimekamilisha maandalizi ya awali ya kuboresha miundombinu muhimu itakayohitajika kuwezesha uendeshaji wa Serikali bila vikwazo katika kipindi hiki.

Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo; kwa mwaka 2016/2017, Serikali ilipanga kutumia shilingi bilioni 11,820.5 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, ambapo, Shilingi bilioni 8,702.6 zilikuwa ni za ndani na bilioni 3,117.8 za nje. Hadi Aprili 2017, fedha zilizokuwa zimetolewa ni shilingi bilioni 4,516.7, sawa na asilimia 38 ya bajeti ya maendeleo. Ikijumuisha fedha zilizotolewa kwa Halmashauri, fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha shilingi bilioni 3,608.9 fedha za ndani na shilingi bilioni 907.8 fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla kiasi cha fedha kilichotolewa ni chini ya maoteo ya mtiririko wa fedha kwa wakati husika. Hii ilichangiwa na sababu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupatikana kwa misaada na mikopo ya kibiashara kufuatia majadiliano na Washirika wetu

wa Maendeleo na mabenki kuchukua muda mrefu, kupanda kwa riba ya mikopo ya kibiashara katika soko la fedha la kimataifa na hivyo Serikali ilifanya uamuzi ya kuahirisha kukopa mikopo hiyo ya kibiashara. Hata hivyo, miradi ambayo ina vyanzo vya fedha mahsusi kama vile Wakala wa Nishati Vijijini, Mamlaka ya Elimu Tanzania, Mfuko wa Barabara, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Mfuko wa Maji na Mfuko wa Reli ilipatiwa fedha zilizokusanywa kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, mikakati mbalimbali imewekwa kuhakikisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo zinapatikana kwa kiasi cha kuridhisha. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha fedha za misaada na mikopo nafuu zinapatikana kama zilivyoahidiwa. Pia kuimarisha makusanyo ya ndani ya Serikali na kuendelea kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi nchini. Aidha, Serikali ipo katika hatua ya mwisho za majadiliano na benki ya *Credit Suisse* ili kupata mkopo wa Dola za Kimarekani milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, changamoto za utekelezaji; utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/2017 umekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na mwenendo wa upatikanaji wa fedha, upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji na matayarisho hafifu ya miradi ambapo kwa baadhi ilionekana bayana kuwa ama ipitiwe upya au majadiliano yaanze upya ili kulinda maslahi ya Taifa.

Mheshimiwa Spika, kwanza, kwa upande wa upatikanaji wa fedha; kwa upande wa makusanyo ya mapato ya ndani, haya yamekuwa yakiongezeka na yamekuwa yakipatikana kwa wakati. Kumekuwepo na ucheleweshaji wa kupatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu na mikopo ya kibiashara kutoka nje, majadiliano yamechukua muda mrefu na hivyo kuchelewa kupatikana kwa fedha kuelekeza kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, zipo hatua mbalimbali ambazo Serikali imechukua kukabiliana na changamoto hii, pamoja na kuzidi kuimarisha makusanyo ya ndani ya Serikali, msisitizo ni kuhakikisha kuwa fedha zilizopatikana zinaelekezwa kwenye miradi yenye tija, kuendelea kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi nchini, ikiwa ni pamoja na wawekezaji wadogo na hususan upatikanaji wa mikopo nafuu na maeneo ya uwekezaji lakini pia kuhuisha sheria, kanuni, taratibu na kupunguza ada, kodi na tozo za uwekezaji na uendeshaji biashara. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na baadhi ya taasisi za fedha na mabanki ili kupata mikopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji; Baadhi ya miradi imekuwa na utekelezaji hafifu kutokana na migogoro ya ardhi na kutokamilika kwa hatua za kulipa fidia, uhakiki umeonesha kuwepo kwa udanganyifu katika gharama na watu wanaostahili kulipwa fidia katika maeneo mengine. Hali hii ililazimisha madai kupitiwa upya na hivyo kucheleweshwa kuanza kwa utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kuongeza kasi ya kupata maeneo maalum ya uwekezaji na maeneo ya viwanda kwa ngazi zote za mikoa. Halmashauri zote zimeagizwa na tayari baadhi zimetenga maeneo ya viwanda na biashara ndogo ndogo. Vilevile, mashirika ya umma yenye ardhi kama vile *NDC* yametumia maeneo hayo kuingia ubia na wawekezaji binafsi.

Mheshimiwa Spika, upande wa upungufu katika maandalizi ya miradi; Serikali imechukua hatua za kuimarisha maandalizi ya miradi, ambapo imeandaa na kuweka utaratibu wa Maofisa kutumia kikamilifu mwongozo wa usimamizi wa uwekezaji wa umma. Pamoja na kuandaa mwongozo huo, Serikali imechukua hatua ya kutoa mafunzo kwa wataalam wanaohusika na uratibu wa miradi ya

maendeleo katika Mikoa na Halmashauri zote nchini lakini pia Wizara, Taasisi, Idara zinazojitegemea na Wakala wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo yapo katika kitabu cha Mpango, Sura ya Tatu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze kwa kifupi Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/2018. Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018 utakuwa ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano na msukumo wake ni kufanikisha utekelezaji wa malengo ya mpango wa miaka mitano hasa kwa miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea tokea mwaka huu tunaomaliza sasa.

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa mpango wa maendeleo umezingatia yafuatayo kama mwongozo:-

Kwanza ni Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa miaka Mitano; Sera na mikakati mbalimbali za Kisekta, Kikanda na Umoja wa Afrika; Ajenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Ajenda ya 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Vilevile, umezingatia mwenendo wa uchumi wa Taifa, kikanda na kidunia kwa mwaka 2016 na maoteo kwa mwaka 2017. Umezingatia pia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2016/2017 na changamoto za utekelezaji zilizojitokeza.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa ushirikishwaji wa jamii katika maandalizi ya mpango huu, mchakato wa maandalizi ya mpango huu umezingatia dhana ya ushirikishwaji mpana wa wadau ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi za Serikali, Taasisi za Utafiti za Elimu ya Juu, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, pia maandalizi yalipata maoni ya Waheshimiwa Wabunge katika Mkutano wa Tano wa Bunge la 11 wakati tulipowasilisha Mapendekezo ya Serikali kwa Mpango wa Maendeleo ninaouwasilisha sasa. Katika Mkutano tajwa, Waheshimiwa Wabunge walitoa maoni na mchango mkubwa ambao umetuwezesha kuandaa Mpango huu.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa maoni mahsusi ya Waheshimiwa Wabunge ilikuwa; Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* upewe kipaumbele; kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara; utekelezaji wa mkakati wa kujenga Zahanati katika kila Kijiji na Vituo vya Afya kila Kata; kuimarisha upatikanaji wa madawa na vifaa tiba; kuendeleza maeneo ya viwanda vidogo na maeneo mahsusi ya *EPZ/SEZ*; kutoa kipaumbele kwa utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe - Mchuchuma na chuma – Liganga; kuboresha elimu ya juu na kuongeza wigo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi; kuboresha miundombinu ya barabara na programu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri wa wadau wengine ambao umezingatiwa katika maandalizi ya Mpango huu ni pamoja na: Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango; upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na nafuu; uimarishwaji wa miundombinu msingi ya bandari na nishati ya umeme; na kuboresha utoaji wa huduma msingi za ustawi wa jamii, hasa elimu, afya, maji, uboreshaji wa mipango miji, nyumba na makazi na utunzaji wa mazingira.

Mheshimiwa Spika, shabaha na malengo ya uchumi jumla kwa mwaka 2017/2018 ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 7.0 ya mwaka 2016;

*NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)*

(ii) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja;

(iii) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani kufikia asilimia 16.5 ya Pato la Taifa;

(iv) Mapato ya kodi kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/2018;

(v) Matumizi ya Serikali kufika asilimia 24.9 ya Pato la Taifa;

(vi) Kuwa na nakisi ya bajeti ya asilimia 3.8 ya Pato la Taifa;

(vii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na

(viii) Kuhakikisha utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, Maeneo ya Kipaumbele katika mpango 2017/2018. Kwa kuzingatia shabaha na malengo haya, miradi iliyobainishwa kuwa ya kipaumbele kwa mpango wa maendeleo wa mwaka 2017/2018 ni ile inayotarajiwa kutoa matokeo makubwa kuendana na malengo ya dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wenyewe. Mingi ya miradi hii utekelezaji wake ulianza mwaka huu wa fedha, hivyo inaendelea.

Mheshimiwa Spika, hii ni pamoja na miradi ya ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*; kuhuisha Shirika la Ndege la Tanzania, na hasa kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege zile nne; miradi ya Chuma - Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma; Uanzishwaji na Uendelezaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; Mtambo wa Kuchakata Gesi Asilia kule Lindi na Shamba la Kilimo na Uzalishaji wa Sukari Mkulazi. Malengo ya utekelezaji kwa maeneo haya kwa



mwaka 2017/2018 tumeyainishwa katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo Sura ya Nne.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine ya kipaumbele itakuwa katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; ikihusisha miradi ya uendelezaji wa eneo la viwanda *TAMCO* - Kibaha; Tathmini ya matumizi ya eneo la viwanda *General Tyre* – Arusha; Mradi wa Magadi Soda – Engaruka; kuimarisha mfumo wa Taifa wa maendeleo ya wajasiriamali; uendelezaji wa maeneo ya viwanda vidogo katika Mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Kigoma na Mtwara; ujenzi wa Ofisi za *SIDO* katika mikoa mipya. Maeneo mengine ni pamoja na kuendeleza viwanda vya ngozi, kupanua mnyororo wa thamani wa pamba hadi nguo na uzalishaji wa madawa na vifaa tiba nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika lengo hili, Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji binafsi hususan katika viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusindika nyama, maziwa, maji, misitu, chokaa, mawe urembo, *gypsum* na mazao ya vyakula na matunda. Serikali itaendelea kuziimarisha taasisi zake ili kuwekeza katika viwanda kwa njia ya ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu; Miradi katika eneo hili ni ile itakayolenga kuimarisha upatikanaji wa fursa za elimu na mafunzo ya ufundi, ambapo tutagharamia elimu msingi bila malipo; Kupanua ruzuku na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; Ununuzi wa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; Ukarabati na upanuzi wa Maktaba ya Mkoa – Dodoma; Ujenzi wa Vyuo vitano vya *VETA* katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe, Rukwa na Kagera. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Afya na Maendeleo ya Jamii, hatua zitaendelezwa za kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa; tutahakikisha upatikanaji wa

vifaa vya kisasa; kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika hospitali, Vituo vya Afya na Zahanati; kuongeza uhibitaji wa magonjwa ya kuambukiza, na kudhibitaji maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, hususan kwa vijana.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa miradi ya maji; ukarabati na upanuzi wa huduma za maji Vijijini; kuboresha huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam; mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Kahama, Nzega, Igunga, Tabora hadi Sikonge; ujenzi na ukarabati na upanuzi wa huduma za maji mijini na vijijini, na kutoa maji Mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara-Mikindani; kujenga na kuimarisha hifadhi ya vyanzo vya maji na misitu, upandaji miti, uvunaji wa maji; kuhimiza matumizi ya teknolojia jadidifu na hifadhi ya mazingira. Hatua nyingine ni pamoja na kupanua upatikanaji wa maji safi, utunzaji wa mazingira na kuimarisha uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara; katika eneo hili, Serikali itaendelea na azma yake ya kupanua miundombinu ya huduma za kiuchumi kufikia azma yake ya kuboresha mazingira ya biashara, ikihusisha miradi inayoendelea ya ukarabati wa miundombinu ya reli, barabara na madaraja katika barabara za Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi; Manyoni – Tabora – Uvinza; Tabora – Koga – Mpanda; ujenzi wa barabara za juu *TAZARA* na Ubungo *Interchange*; ujenzi wa Daraja la *Selander* na miundombinu ya mabasi yaendayo kasi awamu ya II, III na IV Jijini Dar es Salaam. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, aidha, miradi ya bandari ikijumuisha bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Bagamoyo, bandari kavu ya Ruvu na bandari ya Maziwa Makuu Victoria, Tanganyika na Nyasa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usafiri wa anga, Serikali itaendelea na ujenzi wa jengo la abiria *terminal* III katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere; upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kigoma, Tabora na

Mwanza; ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Geita, Sumbawanga, Shinyanga, Mtwara, Musoma, Iringa na Songea; na ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuimarisha utekelezaji wa mpango na miradi; Serikali itaendelea kuchukua hatua za kuimarisha mitaji ya benki za ndani ya maendeleo *TIB* na *TaDB* na kuanza utaratibu wa kuzitumia kama vyombo vyake vya ukusanyaji wa mikopo ya muda mrefu na ya gharama nafuu kwa wawekezaji. Aidha, eneo hili litajumuisha miradi ya kuendeleza na kusimamia matumizi ya ardhi, kuimarisha mipango miji, maendeleo ya nyumba na makazi, kuweka mfumo utakaowezesha nchi kufaidika na ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa, kuimarisha utawala bora na utawala wa Sheria.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuchochea ushiriki na maendeleo ya sekta binafsi na hasa sekta binafsi ya ndani, katika utekelezaji wa mpango na ujenzi wa viwanda. Serikali itaendelea kuboresha kanuni, taratibu na mifumo ya Taasisi ya ujenzi wa biashara na uwekezaji nchini. Kwa kuzingatia hili, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali:-

(i) Kufanya mapitio ya Sera, Sheria na Taratibu zinazochochea ushiriki wa sekta binafsi, ama kuwekeza moja kwa moja au kwa ubia na sekta ya umma;

(ii) Kutenga maeneo ya uwekezaji ili kupunguzia sekta binafsi usumbufu hususan upatikanaji wa ardhi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo mahsusi ya uwekezaji na kuyawekea maeneo hayo miundombinu ya msingi na kuikodisha kwa wawekezaji kwa gharama nafuu;

(iii) Kujenga miundombinu wezeshi hasa miundombinu ya umeme, barabara, maji na reli na kuifikisha katika maeneo ya shughuli za wawekezaji;

(iv) Kusimamia utekelezaji wa sheria na taratibu na kuhakikisha kuwepo kwa amani na usalama;

(v) Kuimarisha mifuko maalum ya kuchochea ushiriki wa sekta binafsi, kama vile *SAGCOT na PPP Facilitation Fund*;

(vi) Kuboresha huduma kwa wawekezaji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha *one stop centre* chini ya *TIC*, bandari ya Dar es Salaam na vituo vya utoaji huduma ya pamoja mipakani; (*Makofi*)

(vii) Kuweka utaratibu utakaoboresha upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na kuimarisha mitaji ya benki maalum ya maendeleo *TaDB* na *TIB*.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kuhamishia Makao Makuu ya Shughuli za Serikali Kuu Dodoma; katika mwaka ujao wa fedha Serikali itaendelea na utekelezaji wa azma ya kuhamishia shughuli za Serikali Makao Makuu Dodoma. Katika kutekeleza azma hii, Wizara zote zimeelekezwa kutenga fedha za kugharamia stahili za watumishi kwa kutumia ukomo wa bajeti uliotengwa kwenye mafungu yao. Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu upatikanaji wa maeneo ya kujenga Ofisi na nyumba za Viongozi wa Serikali kwa kuzingatia mahitaji na maboresho ya mpango wa ardhi katika Mji wa Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuitikia wito wa Serikali wa kujenga uchumi wa viwanda, Mifuko ya Hifadhi ya Jamii imeonesha nia ya kuwekeza katika miradi ya viwanda katika maeneo mbalimbali nchini. Baadhi ya miradi ambayo inatarajiwa kutekelezwa na mifuko katika mwaka ujao wa fedha ni pamoja na:-

Ufufuaji wa Kiwanda cha Sukari katika Gereza la Mbigiri Dakawa Morogoro; Kiwanda cha Kutengeneza Viatu katika Gereza la Karanga Moshi; Kiwanda cha Nguo cha Urafiki Dar es Salaam; Kiwanda cha Morogoro *Canvas Mill*; Kiwanda cha Chai cha Mponde kilichopo Lushoto Mkoani

Tanga; Kiwanda cha Kilimajaro *Machine Tools*; Kiwanda cha Kubangua Korosho cha Tandahimba na Newala. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile, mifuko hii inatarajia kuanzisha viwanda vipya katika maeneo mbalimbali, ikiwemo Kiwanda cha Dawa, Kiwanda cha Kuzalisha Bidhaa za Hospitali na Gesi ya Oksijeni, Kiwanda cha Kusindika Zabibu, Chinangali Dodoma; Viwanda vya Kusindika Nafaka na Ukamuaji wa Mafuta; na Kiwanda cha Kuzalishaji Wanga kutokana na zao la muhogo na viazi vitamu huko Lindi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu Miradi ya Kipaumbele kwa mwaka ujao wa fedha yapo katika kitabu cha Mpango sura ya Nne.

Mheshimiwa Spika, vihatarishi vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa mpango ujao, vipo vihatarishi mbalimbali vinavyoweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vihatarishi hivyo vinaweza kuwa vya ndani au vya nje. Kihatarishi kikuu cha ndani ni ufinyu wa rasilimali fedha na uwepo wa tofauti za mpangilio wa vipaumbele, mpango kazi na mtiririko wa upatikanaji fedha baina ya taasisi za utekelezaji. Vihatarishi vya nje ni pamoja na mitikisiko ya kiuchumi Kikanda na Kimataifa, majanga asilia na athari za mabadiliko ya tabianchi na mabadiliko ya kiteknolojia.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kushirikiana na wadau katika kutekeleza mpango huu, imebainisha na kuweka tahadhari kwa kuchukua hatua zifuatazo:-

Kwanza ni kuandaa bajeti yenye mwelekeo wa kupunguza utegemezi wa kibajeti, kwa kuwianisha vyanzo vya mapato na mkakati wa kukusanya na kuwianisha matumizi na upatikanaji wa mapato ya Serikali; Kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuimarisha sekta binafsi; kuchangia utekelezaji wa baadhi ya miradi na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu mpango na namna bora ya utekelezaji ili kuongeza ushiriki wa jamii na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ugharamiaji wa mpango kwa mwaka 2017/2018. Katika mwaka 2017/2018, shilingi trilioni 11,9 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo; ambapo shilingi trilioni 8.9 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 3.0 ni fedha za nje. Hivyo, fedha zilizotengwa katika bajeti ya maendeleo zimeongezeka kutoka shilingi trilioni 11.8 mwaka 2016/2017. hadi shilingi trilioni 11.99 mwaka 2017/2018 ikiwa ni sawa na asilimia 38 ya bajeti yote. Kiasi hiki ni kikubwa kwa 1.2% ya makadirio ya kutenga shilingi trilioni 11 kila mwaka kutoka mapato ya Serikali kama ilivyojidhihirisha katika mapitio ya utekelezaji wa mwaka wa 2016/2017.

Mheshimiwa Spika, Serikali itahakikisha kuwa kiasi cha fedha kilichopangwa kwa matumizi ya maendeleo kinapatikana na kugawiwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyokusudiwa kwa wakati. Hivyo, pamoja na juhudi za kupanua na kukusanya mapato katika vyanzo vya kawaida vya Serikali, msisitizo umewekwa katika kubaini na kukusanya kutoka vyanzo vipya. Mfumo wa ukusanyaji katika baadhi ya maeneo utafanyiwa mabadiliko ili kuongeza ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mashirika na Taasisi za Umma, katika historia ya nchi yetu na pia nchi nyingi zinazoendelea, Mashirika ya Umma yamekuwa na mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi husika. Kwa kutambua hili, Serikali imeelekeza mashirika na taasisi zake za umma za kibiashara kuchangia katika kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. Taasisi hizi zinaweza kutekeleza hili kupitia mapato au kwa kukopa kwa ridhaa ya Serikali kutokana na dhamana ya mali zao ili kugharamia utekelezaji wa miradi itakayobainishwa kuwa ya kipaumbele.

Mheshimiwa Spika, sekta binafsi, kama ilivyojidhihirisha mwaka 2016/2017, sekta binafsi ya ndani na nje imepokea kwa hamasa kubwa wito wa Serikali wa kuchochea uwekezaji hasa katika maeneo mengine zaidi ya kilimo na

madini. Serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara itaendelea kusimamia utekelezaji wa maazimio yenye lengo la kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na uendeshaji wa biashara nchini. Katika kuvutia uwekezaji kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Serikali itaendelea kuimarisha Mfuko wa Fedha wa miradi ya ubia yaani *PPP Facilitation Fund* kwa lengo la kugharamia uandaaji wa upembuzi yakinifu kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo tarajiwa ni ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi katika miradi ya kipaumbele kwa njia ya ubia. Serikali pia imeamua, kwa makusudi kuondoa mlolongo wa kodi kwa sekta ya kilimo na biashara ndogo ndogo kwa ajili ya kuinua uwekezaji wa sekta hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile, imechukua hatua za kuhakikisha upatikanaji wa maeneo ya viwanda na biashara ndogo kwa urahisi. Msukumo pia umewekwa kuboresha upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu na ya muda mrefu kwa wawekezaji ikiwa ni pamoja na kuimarisha benki za maendeleo nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu Ugharamiaji wa Mpango yapo katika kitabu cha mpango Sura ya Tano.

Mheshimiwa Spika, ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa. Moja ya changamoto za utekelezaji wa mpango wa maendeleo ni udhaifu katika ufuatiliaji wa miradi. Udhaifu huu unatokana na changamoto za upatikanaji wa rasilimali fedha pamoja na upungufu wa watumishi wenye uzoefu na utaalum wa ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, Serikali katika kuimarisha eneo hili imeamua kuweka mfumo wa mafunzo na malezi yatakayoharakisha kuimarisha utaalum wa kupanga, kutayarisha, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji

wa miradi. Nitumie fursa hii kuwaelekeza Maafisa Masuuli wote kutenga fedha za ufuatiliaji na tathmini kama sehemu ya gharama ya utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Spika, hatua pia zimechukuliwa kwa lengo la kuhuisha nyenzo za ufuatiliaji na tathmini na hii ni pamoja na kuandaa na kutoa mafunzo juu ya matumizi ya mwongozo wa usimamizi na uwekezaji wa umma. Katika mwaka ujao wa fedha mafunzo yatatolewa kwa maafisa wa ufuatiliaji na tathmini kuwawezesha kujua hatua za msingi katika kuandaa, kuratibu na kutathmini miradi ya maendeleo. Serikali kupitia Tume ya Mipango imeandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa za miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuimarisha vigezo vya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi, Serikali kupitia Tume ya Mipango itaratibu zoezi hilo kupitia Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa Miaka Mitano. Hatua hii itasaidia kuboresha upatikanaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya miradi husika kwa kuzingatia vigezo vya utekelezaji vilivyokusudiwa kwa kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu ufuatiliaji, tathmini na utoaji taarifa yapo katika kitabu cha mpango Sura ya Sita.

Mheshimiwa Spika, hitimisho. Tangu Serikali ilipotangaza dhamira ya kujenga uchumi wa viwanda kumekuwa na mwitiko wa uwekezaji wa umma na binafsi, unaotia matumaini makubwa. Jitihada hizi hazina budi kuungwa mkono hususan kuweka kusudio la kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na uendeshaji biashara nchini. Hivyo, hatua za mapitio ya sera, sheria, kanuni na mfumo taasisi wa usimamizi zitaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na mfumo unaoakisi kusudio hili kwa vitendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, hasa kutokana na ukweli kuwa sehemu kubwa ya viwanda vitakavyoanzishwa



vitatumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini, hatua za makusudi zitaendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija na ubora wa malighafi zinazolishwa nchini ili kukidhi mahitaji ya soko linalozidi kukua na kubadilika.

Mheshimiwa Spika, kuna kasi kubwa ya mabadiliko ya mfumo wa maisha na matarajio ya jamii hasa kundi kubwa la vijana. Matarajio haya ya vijana yanaweza kufikiwa tu ikiwa wataweza kuajiriwa au kuwa na shughuli ya kujajiri wenyewe. Kwa mantiki hiyo ni wajibu wa msingi kabisa wa Serikali kuzidi kupanua fursa za uwekezaji. Uwekezaji unaweza kuwa ama wa Serikali moja kwa moja, ubia kati yake na sekta binafsi au wa sekta binafsi moja kwa moja. Kwa kutambua hili, Serikali inahitaji sana ushirikiano na mshikamano kati yake na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano na mshikamano huu unapaswa kuwa mpana na wa kina katika nyanja zote, kuanzia kuibua, kupanga, kutekeleza na kufuatilia na kutathmini hatua za utekelezaji. Katika kutekeleza hili, msukumo utawekwa katika kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi kwa kuandaa mikutano na mashauriano ya mara kwa mara ikiwa ni pamoja na ile ya Baraza la Biashara Tanzania (TNBC) itakayojadili na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Awamu ya Tano ilitangaza toka mwanzo kabisa azma yake ya kujitanabaisha kuwa ya ukweli na uwajibikaji hasa katika kusimamia matumizi ya rasilimali zinazopatikana kwa manufaa ya Taifa na kila mwananchi. Kutokana na hili, Serikali inaendelea kujielekeza katika kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani kwa kufanyia mapitio ya mifumo na muundo wa usimamizi wa makusanyo ya kodi, malimbikizo ya kodi, kupanua wigo wa kodi na kusajili walipa kodi wapya, pamoja na utekelezaji wa mikakati ya kuongeza makusanyo.

Mheshimiwa Spika, msukumo pia utawekwa katika kuongeza matumizi ya teknolojia ya kielektroniki ili kupunguza

athari za upungufu wa kibinadamu katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi fedha na kumbukumbu. Hatua hizi zote ndizo zitakazoweza ustawi wa uchumi na utekelezaji bora wa mpango wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika uchumi na utekelezaji wa mpango yamechangiwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi, wakiwemo nchi marafiki, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Kwa niaba ya Serikali nawashukuru wadau wote hawa kwa michango yao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kumaliza hotuba yangu napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Ashatu K. Kijaji Mbunge; Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kwa ushirikiano wao wakati wote wa maandalizi ya kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Ndugu Doto James kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Wizara. Aidha, niwatambue Ndugu Maduka Kessy, Kaimu Katibu Mtendaji, viongozi na watumishi wote wa Tume ya Mipango kwa kufanikisha maandalizi ya hotuba hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya hali ya uchumi 2016, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/2018 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz) na [www.mipango.go.tz](http://www.mipango.go.tz).

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, wajadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono.

Nakushukuru sana Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yako nzuri sana kwetu Waheshimiwa Wabunge na kwa Taifa. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO DKT. PHILIP I. MPANGO AKIWASILISHA BUNGENI TAARIFA YA HALI YA UCHUMI 2016 NA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA KWA MWAKA 2017/2018 KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*"Tamaa yangu, na kwa kweli jitihada za Serikali ya Awamu ya Tano, zitakuwa katika ujenzi wa uchumi wa kipato cha kati ambapo sura na maisha ya Watanzania walio wengi yafanane fanane na nchi ya kipato cha kati. Njia moja ya kutufikisha huko ni uendelezaji wa viwanda."*

Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Tarehe 20 Novemba, 2015, BUNGENI, DODOMA.

**UTANGULIZI**

1. **Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18. Pamoja na hotuba hii nawasilisha vitabu vya Taarifa ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18, ambapo taarifa hizi ndio msingi wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/18 itakayowasilishwa Bungeni baadaye hivi leo.

2. **Mheshimiwa Spika**, awali ya yote napenda

kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uhai na afya njema na kutuwezesha kukutana katika Mkutano wa 7 wa Bunge la 11 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tukiwa na dhamira ya kulinda na kuendeleza amani na maelewano hapa nchini, na pia ari ya kufikia malengo yetu ya maendeleo. Napenda kukushukuru wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika pamoja na Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha majadiliano ya Bajeti za Kisekta na shughuli nyingine za Bunge hili kwa umakini, utulivu na hekima kubwa. Ni matumaini yangu kuwa uzalendo uliojionesha katika kujadili hotuba za mipango na bajeti za kisekta utaendelea kudumishwa.

**3. Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kutoa pole kwako, Waheshimiwa Wabunge wote na wananchi kwa kuondokewa na wabunge wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir aliyekuwa Mbunge wa Dimani (CCM) na Mheshimiwa Dkt. Ely Marko Macha, Mbunge wa Viti maalum (CHADEMA). Pia, nitumie fursa hii kuwapa pole wabunge wote waliopoteza wapendwa wao na wananchi wote waliopatwa na maafa mbalimbali katika mwaka huu, yakiwemo matukio ya kusikitisha ya kuondokewa na watoto wetu 32, walimu wawili na dereva wa shule ya Lucky Vincent katika ajali mkoani Arusha mwezi uliopita, wanafunzi watatu kule mkoani Geita, wanafunzi wawili na mzazi mmoja mkoani Kagera kwa kuzama majini na Askari wetu nane na wananchi wengine waliouawa kikatili katika matukio ya kupanga mkoani Pwani. Tunamwomba Mwenyezi Mungu aziweke roho za marehemu mahali pema, peponi.

**4. Mheshimiwa Spika**, kipekee kabisa, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais na Mheshimiwa Kassim M. Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi madhubuti kusimamia mabadiliko yanayoleta tija katika utendaji Serikalini, kuharakisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii nakuendeleza misingi ya utawala bora. Uongozi wao umejipambanua katika kupambana na rushwa, ufisadi, ukwepaji kodi, uzembe na urasimu katika utumishi wa umma

na ubadhirifu wa mali za umma lakini pia msisitizo wa umuhimu wa kila mwananchi kufanya kazi. Juhudi hizi zinapaswa kuungwa mkono kwa nguvu zote na viongozi na Wananchi wote.

**5. Mheshimiwa Spika**, niruhusu pia niwapongeze kwa dhati wabunge wapya walioingia Bungeni katika mkutano huu wa 7 wa Bunge la 11 ambao ni: Mheshimiwa Salma R. Kikwete, Mheshimiwa Dkt. Gertrude Pangalile Rwakatare, wote wa CCM na Mheshimiwa Catherine Ruge wa CHADEMA. Tunawakaribisha kuungana na Waheshimiwa Wabunge wengine kutekeleza wajibu wa msingi wa Bunge wa kuishauri na kuisimamia Serikali kwa hekima na weledi na kuweka mbele maslahi ya Taifa kwa manufaa ya Watanzania. Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge kutoka vyama vyote waliochaguliwa na Bunge hili kuiwakilisha nchi yetu katika Bunge la Afrika Mashariki. Matarajio yetu ni kuwa watalinda na kusimamia na kutetea vema maslahi ya nchi yetu katika Bunge hilo la Afrika Mashariki.

**6. Mheshimiwa Spika**, naomba nitumie fursa hii kuishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini; na Makamu wake, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa maelekezo na ushauri wa kizalendo waliotupatia, ambao umesaidia kuboresha taarifa za mwenendo wa uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/18, ninazoziwasilisha.

**7. Mheshimiwa Spika**, hotuba ninayoiwasilisha imegawanyika katika maeneo makuu matano (5): eneo la kwanza ni utangulizi, la pili ni taarifa ya mapitio ya Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016 na robo ya kwanza ya 2017; eneo la tatu, ni Muhtasari wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2016/17; nne, ni Maeneo ya Kipaumbele ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo kwa mwaka 2017/18; na mwisho, ni Majumuisho.

## MWENENDO WA HALI YA UCHUMI 2016

### Uchumi wa Dunia

8. **Mheshimiwa Spika**, Kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa mwaka 2016, ilikuwa asilimia 3.1 ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2015. Kupungua huku ni matokeo ya kupungua kwa ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea, ambapo ukuaji wa uchumi kwa nchi zilizoendelea kilikuwa asilimia 1.7 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 1.9 mwaka 2015, ukichangiwa na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa na huduma katika masoko mengi duniani na kupungua kwa tija ya uzalishaji na kasi ya uwekezaji. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi zinazoendelea ilikuwa asilimia 4.1 sawa na ilivyokuwa mwaka 2015. Ukuaji huu kwa nchi zinazoendelea ulichangiwa zaidi na kupungua kwa ukuaji wa uchumi kwa nchi za China na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara kufuatia kuporomoka kwa bei za bidhaa hasa bidhaa ghafi katika soko la dunia, kupungua kwa uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi na kushuka kwa mahitaji ya bidhaa zinazozalishwa katika masoko mengi duniani.

9. **Mheshimiwa Spika**, mfumuko wa bei duniani uliongezeka kufikia wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 2.8 mwaka 2015. Kwa kiasi kikubwa mfumuko wa bei uliongezeka kutokana na kulegezwa kwa sera za bajeti na fedha kwa baadhi ya nchi na ukame uliochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa (yanayojulikana kama *La Nina*). Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea uliongezeka kufikia asilimia 0.8 kwa mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 0.3 mwaka 2015, ambapo kwa nchi zinazoendelea za Asia, uliongezeka hadi asilimia 3.1 kutoka asilimia 2.7 mwaka 2015. Kwa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, ulifikia asilimia 11.4 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2015.

### Uchumi wa Afrika na Kikanda

10. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa nchi za Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara, wastani wa kasi ya ukuaji wa

uchumi ilipungua kutoka asilimia 3.4 mwaka 2015 hadi asilimia 1.4 mwaka 2016. Hii ni kutokana na kupungua kwa upatikanaji wa mikopo kutoka kwenye masoko ya kimataifa uliosababisha miradi iliyopangwa katika kipindi hicho kushindwa kukamilika, kuendelea kwa migogoro ya kisiasa kwa baadhi ya nchi (Burundi, Libya, Chad, Sudan Kusini na DRC), na kuporomoka kwa bei za baadhi ya mazao ghafi, hususan, dhahabu na mafuta ya petroli.

**11. Mheshimiwa Spika**, kasi ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki ilishuka kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2015 hadi asilimia 5.3 mwaka 2016 ijapokuwa Jumuiya hii iliendelea kuongoza kwa ukuaji miongoni mwa Jumuiya mbalimbali za Afrika. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi katika Jumuiya hii ilichangiwa na sababu mbalimbali ikiwemo kushuka kwa bei za bidhaa na kudorora kwa uchumi wa dunia. Maoteo ya mwenendo wa uchumi katika ukanda huu yanaonesha utakua kwa wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2017 na asilimia 6.0 mwaka 2018. Matarajio haya yanazingatia hatua zinazochukuliwa na nchi za ukanda huu katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na uendeshaji biashara kama vile kuwa na maeneo tengefu ya ujenzi wa viwanda (industrial parks), hususan, vya nguo, bidhaa za ngozi, kilimo, madawa na vifaa tiba.

**12. Mheshimiwa Spika**, Mfumuko wa bei katika nchi za Afrika Mashariki kwa mwaka 2016 uliendelea kuwa wa kiwango cha tarakimu moja, ambapo Rwanda ilikuwa na asilimia 7.1, Uganda asilimia 5.4, Tanzania asilimia 5.2, Kenya asilimia 6.3 na Burundi asilimia 5.6. Aidha, kufikia Machi 2017, mfumuko wa bei kwa nchi hizi ulipanda, ambapo kwa Burundi ulifikia asilimia 21.10, Rwanda asilimia 13.0; Kenya asilimia 10.28; Uganda asilimia 6.4 na Tanzania asilimia 6.4. Hali hii ilichangiwa na ukame katika maeneo mengi ya ukanda huu kutokana na kuchelewa kwa msimu wa mvua.

**13. Mheshimiwa Spika**, kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika, yaani SADC, kasi ya ukuaji wa uchumi ilishuka kutoka wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2015 hadi asilimia 1.1 mwaka 2016. Kasi ndogo ya ukuaji wa

uchumi katika Jumuiya hii ilichangiwa na uhaba wa nishati ya umeme pamoja na ukame uliochangiwa na mabadiliko ya hali ya hewa ya *La Nina*. Licha ya kasi ndogo ya ukuaji, Jumuiya hii iliendelea kuwa ya tatu kwa ukuaji miongoni mwa Jumuiya za barani Afrika na unatarajiwa kukua kwa wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2017. Mfumuko wa bei ulifikia asilimia 10.5 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 5.7 mwaka 2015, ukichangiwa na ukame na kuyumba kwa utekelezaji wa sera za mapato na matumizi kwa baadhi ya nchi wanachama. Matarajio ni kuwa kwa mwaka 2017 mfumuko wa bei utapungua hadi kufikia asilimia 8.7 kutokana na kushuka kwa gharama za bidhaa, kuimarika kwa upatikanaji wa nishati ya umeme, na uthabiti wa bei ya mafuta; na kuimarika kwa hali ya hewa.

## **Uchumi wa Taifa**

### **Ukuaji wa Uchumi na Pato la Taifa**

**14. Mheshimiwa Spika**, Pato la Taifa lilikua kwa wastani wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2016, kama ilivyokuwa mwaka 2015. Kiwango hiki hata hivyo ni chini ya maoteo ya kufikia asilimia 7.2 kutokana na ukuaji wa baadhi ya shughuli kushindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji. Baadhi ya shughuli za kiuchumi ambazo zilishindwa kufikia maoteo ya viwango vya ukuaji ni pamoja na: sekta ya kilimo iliyokua kwa asilimia 2.1 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 2.9; biashara na matengenezo asilimia 6.7 dhidi ya asilimia 7.8; huduma za malazi na chakula asilimia 3.7 kinyume na maoteo ya asilimia 8.0; na huduma za utawala asilimia 2.1 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 6.3. Aidha, zipo shughuli za kiuchumi zilizokua na hata kuzidi maoteo. Shughuli za uchumi zilizokuwa na viwango vikubwa vya ukuaji ni pamoja na: habari na mawasiliano asilimia 13.0 dhidi ya maoteo ya asilimia 12.1; usafirishaji na uhifadhi mizigo asilimia 11.8 dhidi ya maoteo ya asilimia 8.0; uchimbaji madini na mawe asilimia 11.5 dhidi ya maoteo ya asilimia 9.2; na uzalishaji viwandani asilimia 7.8 ikilinganishwa na maoteo ya asilimia 6.7.



## Mchango wa Kisekta katika Pato la Taifa

**15. Mheshimiwa Spika**, mchango wa shughuli za kilimo (mazao, ufugaji, misitu na uvuvi) katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 29.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 29.0 mwaka 2015. Shughuli za viwanda na ujenzi zilichangia asilimia 25.2 ya Pato la Taifa mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 24.3 mwaka 2015, ambapo mchango wa sekta za huduma (ikijumuisha biashara na matengenezo, usafirishaji na uhifadhi mizigo, malazi, habari na mawasiliano, fedha na bima, upangishaji majumba, elimu na afya) ulikuwa asilimia 39.1 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 40.0 mwaka 2015. Kuongezeka kwa mchango wa shughuli za viwanda, ni dalili kuwa azma ya Serikali ya kujenga uchumi wa viwanda imeanza kuleta matokeo chanya, ambapo tija na uzalishaji viwandani unaimarika. Pamoja na mambo mengine, hii inatokana na kuimarika kwa upatikanaji wa miundombinu, hususan, nishati na usafiri.

## Wastani wa Pato la Kila Mtu

**16. Mheshimiwa Spika**, Pato la Taifa kwa mwaka 2016 lilifikia Shilingi milioni 103,744,606 (kwa bei za mwaka husika). Kiasi hiki cha Pato kikigawiwa kwa idadi ya watu wanaokadiriwa kuwepo Tanzania Bara, ya watu 48,676,698, inafanya wastani wa Pato la kila mtu kufikia Shilingi 2,131,299 ikilinganishwa na wastani wa Shilingi 1,918,897 mwaka 2015, sawa na ongezeko la asilimia 11.1. Hata hivyo, katika thamani ya Dola za Marekani, wastani wa Pato la kila mtu liliongezeka kidogo kutoka Dola 967.5 mwaka 2015 hadi Dola 979.1 mwaka 2016, ikimaanisha kuwa bado kuna hatua ili kuingia katika kundi la uchumi wa kati. Kiwango cha chini cha uchumi wa kati ni kufikia Dola 1,043. Hivyo basi, kasi ya ongezeko la Pato la mwananchi katika thamani ya Dola haina budi kuongezeka. Hii itawezekana kwa kutanzua changamoto zilizopo hususan, uzalishaji na tija katika sekta zinazoajiri wananchi wengi hasa kilimo cha mazao, ufugaji na uvuvi.

## **Mwenendo wa Bei**

**17. Mheshimiwa Spika**, Kwa miaka minne mfululizo, wastani wa mfumuko wa bei nchini umeendelea kupungua, ukibaki katika kiwango cha tarakimu moja. Kwa mwaka 2016, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 5.2 ikilinganishwa na asilimia 5.6 mwaka 2015. Kupungua kwa wastani wa mfumuko wa bei nchini kulichangiwa kwa kiasi kikubwa na: mwenendo wa kushuka wa bei za mafuta ya petroli katika soko la dunia na nchini; kuimarika kwa upatikanaji wa vyakula nchini na hivyo wastani wa bei; na kuwepo kwa sera madhubuti za usimamizi wa bajeti na fedha. Mfumuko wa bei uliongezeka kidogo, ambapo ulifikia asilimia 6.4 mwezi Aprili 2017 lakini ukiwa ndani ya maoteo ya wastani wa tarakimu moja (asilimia 5 – 8) kwa mwaka 2017. Hali ya kuongezeka kwa mfumuko wa bei nchini ilichangiwa na hofu iliyotokana na kuchelewa kwa msimu wa mvua katika maeneo mengi nchini na hivyo kuwepo kwa taharuki ya kutokea upungufu wa chakula. Hata hivyo, maeneo mengi yamepata mvua ya kutosha na hivyo bei ya chakula nchini inatarajiwa kuimarika.

## **Mwenendo wa Viwango vya Riba**

**18. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016 viwango vya riba za amana na mikopo vilipungua ikilinganishwa na mwaka uliotangulia. Riba za amana za muda maalum zilipungua kutoka wastani wa asilimia 9.30 hadi asilimia 8.78. Viwango vya riba za amana za mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 11.16 mwaka 2015 hadi asilimia 11.03 mwaka 2016. Vile vile, viwango vya riba za mikopo ya hadi mwaka mmoja vilipungua kutoka wastani wa asilimia 14.22 kufikia asilimia 12.87 mwaka 2016. Mwenendo huu ulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa kibenki. Kufuatia hali hiyo, tofauti kati ya riba za amana na mikopo ya mwaka mmoja ilipungua kufikia asilimia 1.83 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 3.06 mwaka 2015. Hata hivyo, riba ya mikopo baina ya benki iliongezeka kufikia wastani wa asilimia 13.49 mwezi Desemba 2016 kutoka asilimia 7.29 kwa

muda kama huo mwaka 2015. Riba kwa dhamana za Serikali ilipungua kutoka asilimia 18.25 mwezi Desemba 2015 kufikia wastani wa asilimia 15.12 mwezi Desemba 2016.

**19. Mheshimiwa Spika**, kufikia Machi 2017, riba za amana za muda maalum ziliongezeka kidogo kuwa asilimia 10.89; na riba za amana za mwaka mmoja kufikia asilimia 12.03. Wakati huo huo, riba za mikopo ya hadi mwaka mmoja ziliongezeka kufikia asilimia 18.07. Ongezeko hili la riba za mikopo katika kipindi cha robo ya kwanza ya mwaka 2017 kunatokana na mabenki kuchukua tahadhari dhidi ya kuongezeka kwa makadirio ya mikopo chechefu na kupunguza maoteo ya faida. Kuongezeka kwa riba za amana kulichangiwa na kuongezeka kwa ushindani wa kibenki katika kuvutia amana. Kwa upande mwingine, riba za mikopo baina ya benki zilipungua kufikia wastani wa asilimia 8.16 na kwa dhamana za Serikali asilimia 14.52.

### **Amana katika Benki za Biashara**

**20. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka 2016, amana katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 2.3 kufikia shilingi bilioni 19,729.5 kutoka shilingi bilioni 19,293.7 mwaka 2015. Kati ya amana hizo, sekta binafsi ilichangia asilimia 97.1 ikilinganishwa na asilimia 95.6 mwaka 2015. Aidha, uwiano wa amana za fedha za kigeni katika amana zote ulipungua kufikia asilimia 31.6 mwaka 2016 kutoka asilimia 32.8 mwaka 2015. Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2017, amana katika benki za biashara ziliongezeka kufikia shilingi bilioni 19,853.40, ambapo sekta binafsi ilichangia asilimia 96.4.

### **Mwenendo wa Mikopo kwa Sekta Binafsi**

**21. Mheshimiwa Spika**, mikopo ya mabenki kwa sekta binafsi kwa mwaka 2016 iliongezeka kwa asilimia 7.2 kufikia Shilingi bilioni 16,608.9 ikilinganishwa na Shilingi bilioni 15,492.7 mwaka 2015. Ukuaji huu ulikuwa chini ya kiwango cha mwaka 2015 cha asilimia 24.8. Kiasi cha mikopo kilichotolewa kwa sekta binafsi mwaka 2016 kilifikia asilimia 16.2 ya Pato la Taifa ikilinganishwa na asilimia 17.1 mwaka 2015. Kiwango

cha mikopo kilichotolewa kwa shughuli za uzalishaji; kilimo, uchukuzi na mawasiliano, viwanda, huduma za kifedha, umeme, majengo na ujenzi, kilipungua mwaka 2016 ikilinganishwa na mwaka 2015. Wakati huo huo, mikopo ya shughuli za madini na uchimbaji mawe, biashara, utalii, hoteli na migahawa na shughuli binafsi iliimarika, japo kwa kasi ndogo. Mikopo iliyoelekezwa katika shughuli za biashara, ilikuwa asilimia 21 ya mikopo yote na shughuli binafsi asilimia 18.6. Mwenendo huu ulichangiwa, kwa kiasi kikubwa, na kupungua kwa ukwasi katika mabanki kutokana na tahadhari zilichukuliwa na mabanki kufuatia kuongezeka kwa makisio ya viwango vya mikopo chechefu na kupungua kwa maoteo ya faida.

**22. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Januari hadi Machi 2017, mikopo ya benki za biashara kwa sekta binafsi iliendelea kuimarika, ikiongezeka kwa shilingi bilioni 77.4 kufikia shilingi bilioni 16,686.30. Hizi ni ishara njema za kuanza kuimarika kwa uchumi na shughuli za sekta binafsi hususan, za uzalishaji viwandani, majengo na mahoteli na mighahawa.

### **Ukuzaji Rasilimali**

**23. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni mojawapo wa nchi chache za Afrika zilizojiipambanua kwa kuwa na utulivu wa uchumi jumla kwa muda mrefu sasa. Hii ikiwa ni pamoja na kuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei wa wastani na mwenendo wa thamani ya shilingi umekuwa thabiti. Hali hii imekuwa kishawishi kikubwa cha mitaji kutoka nje kuja nchini. Kwa mwaka 2016, ukuzaji rasilimali, kwa bei za miaka husika, uliongezeka kwa asilimia 3.4 kutoka shilingi milioni 24,717,206 mwaka 2015 hadi Shilingi milioni 25,558,140. Hata hivyo, uwiano wa ukuzaji rasilimali na Pato la Taifa, kwa bei za miaka husika, ulipungua kufikia asilimia 24.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na asilimia 27.2 mwaka 2015. Kiwango cha ukuzaji rasilimali kwa bei za mwaka 2007, kilipungua kwa asilimia 4.3 kutoka Shilingi milioni 13,733,585 mwaka 2015 kufikia Shilingi milioni 13,140,451 mwaka 2016.

## Sekta ya Nje

**24. Mheshimiwa Spika**, Mwaka 2016, mwenendo wa biashara ya bidhaa na huduma kati ya Tanzania na nchi mbalimbali uliendelea vizuri. Thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje iliongezeka kwa asilimia 4.1 kufikia dola za Marekani milioni 9,285.6 mwaka 2016 ikilinganishwa na Dola milioni 8,918.1 mwaka 2015. Aidha, uagizaji wa bidhaa na huduma nje ilipungua kwa asilimia 14.0 kwa mwaka 2016 kutoka Dola milioni 12,528.2 mwaka 2015 kufikia dola za Marekani milioni 10,772.3. Mwenendo huo ulitokana na kupungua kwa thamani ya bidhaa nyingi zilizoagizwa kutoka nje isipokuwa kwa malighafi za viwandani zilizoongezeka ikichangiwa pia na kupungua kwa gharama za usafirishaji, huduma zitolewazo na Serikali, na huduma nyingine za kibiashara.

**25. Mheshimiwa Spika**, Biashara kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani ziliendelea kuimarika na masoko kubadilika, ambapo kwa mwaka 2016 sehemu kubwa ya mauzo yote nje ya nchi yalikuwenda katika nchi za Uswisi (asilimia 16.2), India (asilimia 12.4), Afrika ya kusini (asilimia 12.2), China (asilimia 6.2), Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (asilimia 5.6) na Kenya (asilimia 5.5). Hii inaonesha kuwa kumekuwa na mabadiliko kutoka masoko asilia, kama vile, Uingereza, Ujerumani na Canada. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi nchini Uswisi na India ni pamoja na dhahabu, mbegu za mafuta, vito vya thamani na mbogamboga. Bidhaa zilizouzwa Kenya zilikuwa chai, mahindi, vifaa vya ushonaji, mbogamboga na nafaka. Vile vile, bidhaa zilizouzwa Afrika ya Kusini zilikuwa dhahabu, madini ya shaba na chai. Pamoja na maendeleo haya, mauzo mengi nje ya nchi yaliendelea kuwa ya mazao ghafi yasiyoongezwa thamani na hivyo kupata thamani ndogo.

**26. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa bidhaa zilizoagizwa kutoka nje, kiasi kikubwa kilitoka katika nchi za China, India, Ufalme wa nchi za Kiarabu, Afrika ya Kusini, Japani na Kenya, nchi ambazo kwa pamoja zilichangia asilimia 60.6 ya bidhaa zote zilizoagizwa. Bidhaa zilizoagizwa

kutoka China ni pamoja na mitambo na bidhaa za marumaru, kwa Ufalme wa nchi za Kiarabu ni mafuta ya petroli na sukari na kwa upande wa Japani na Afrika ya Kusini ni magari na bidhaa za chuma, kuonesha kuwa uzalishaji nchini bado unategemea vipuri, malighafi na mitambo kutoka nje.

**27. Mheshimiwa Spika**, kufuatia mwenendo wa biashara kwa mwaka 2016, urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya Dola za Marekani milioni 1,489.5, ikipungua kwa asilimia 58.6 kutoka nakisi ya Dola za Marekani milioni 3,594.7 mwaka 2015. Hali hii kwa kiasi kikubwa, ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Hivyo, urari wa malipo yote, kwa mwaka 2016, ukijumuisha urari wa biashara ya bidhaa na huduma, mapato ya vitega uchumi, uhamisho wa mali, malipo ya kawaida, uhamisho wa mitaji na malipo ya fedha katika uwekezaji, ulikuwa na ziada ya dola za Marekani milioni 305.5 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 199.1 mwaka 2015. Katika kipindi cha Januari hadi Machi mwaka 2017, thamani ya mauzo ya bidhaa na huduma nje ilifikia Dola za Marekani milioni 2,224.8, ikichangiwa, kwa kiasi kikubwa, na mauzo ya bidhaa asilia na zisizo asilia hasa huduma za utalii, dhahabu, bidhaa za mboga mboga na matunda. Aidha, katika kipindi hicho, uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ulikuwa Dola za Marekani milioni 2,203.6 na hivyo kuendelea kuwa na ziada katika urari wa akaunti ya biashara ya bidhaa na huduma.

### **Akiba ya Fedha za Kigeni na Thamani ya Shilingi**

**28. Mheshimiwa Spika**, hadi kufikia mwezi Desemba 2016, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Marekani milioni 4,325.6 ikilinganishwa na Dola milioni 4,093.7 Desemba 2015. Kiasi hicho kilikuwa kinaweza kulipia gharama za kununua bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.2. Kufikia Machi 2017, akiba ya fedha za kigeni ilifikia Dola za Kimarekani milioni 4,482.6, kiasi kinachotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi 4.3. Kuongezeka kwa akiba ya fedha

za kigeni kumesaidia kurejesha utengamavu wa thamani ya shilingi. Katika kipindi cha mwaka 2016, mwenendo wa **thamani ya shilingi** ya Tanzania dhidi ya dola ya Marekani ulikuwa wa kuridhisha ukipungua kwa asilimia 8.8 tu ambapo dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa Shilingi 2,177.07 ikilinganishwa na shilingi 1,991.4 mwaka 2015.. Hadi kufikia Machi 2017, dola moja ya Marekani ilinunuliwa kwa wastani wa shilingi 2,223.9 kutoka Shilingi 2,172.6 ilivyokuwa ikinunuliwa mwishoni mwa mwaka 2016.

## **Mabadiliko ya Maisha ya Watu**

**29. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2012, Tanzania ina wastani wa ongezeko la watu la asilimia 2.7 kwa mwaka, ambapo kufikia mwaka 2016 ilikadiriwa kuwa na watu 48,676,698. Kwa makadirio haya, Tanzania inakuwa ni nchi ya tano kwa idadi ya watu Barani Afrika, ikitanguliwa na nchi nne (4) ambazo ni Nigeria, Ethiopia, Misri na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo. Idadi kubwa ya watu na kasi ya ongezeko imekuwa ni changamoto kubwa katika harakati za kupunguza umaskini na kuimarisha utoaji wa huduma. Kwa kuzingatia hali hii, Serikali imeendelea kuongeza na kuboresha upatikanaji wa elimu msingi hususan kwa wasichana. Kwa upande mwingine, idadi kubwa ya watu ni fursa pia kwa maana ya soko la bidhaa na huduma, ikiwa itaendana na maendeleo ya stadi, teknolojia, ujasiriamali na pato la kila mwananchi.

**30. Mheshimiwa Spika**, licha ya hatua hizi, bado kumekuwa na changamoto nyingine kufuatia kasi kubwa ya uhamiaji mijini, ambapo kwa sasa, takribani asilimia 30 ya watu nchini wanaishi mijini. Kasi hii ya mabadiliko ya idadi ya watu na uhamiaji mijini inadunisha kasi ya kuboresha upatikanaji wa nyumba na makazi yaliyopangwa na pia utoaji wa huduma zinazoendana na idadi ya wakazi wa mijini. Katika kukabiliana na changamoto hizi, Serikali imeendelea kuimarisha upimaji wa maeneo ya makazi, ujenzi wa nyumba za gharama nafuu na kuchukuwa hatua zinazolenga kuinua tija na faida katika shughuli za kilimo.

Hatua hizo ni pamoja na kuimarisha upatikanaji wa huduma za ugani, pembejeo, zana za kilimo, masoko, miundombinu ya umwagiliaji, na kuondoa utitiri wa kodi katika shughuli za kilimo. Hatua pia zimeendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuweka mazingira mazuri ya uwekezaji na uendeshaji wa shughuli za viwanda na biashara hasa vijijini. Lengo ni kupanua fursa za ajira mbadala kwa wakazi wa vijijini, ikiwa ndiyo njia ya kuaminika zaidi katika kudhibiti kasi ya watu kuhamia mijini. Huduma za mafunzo ya ufundi stadi zimezidi kuimarishwa ili wale wanaohamia mijini waweze kuajirika na kujiajiri kwa urahisi.

**31. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa ustawi wa jamii, maisha ya watu yameendelea kuboreka kama inavyohibitishwa na taarifa ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo ya Watu kwa mwaka 2016, ambapo kwa kigezo cha fahirisi ya maendeleo ya watu (HDI) ustawi wa watanzania umeendelea kuimarika kutoka alama 0.521 mwaka 2014 hadi alama 0.531 mwaka 2015. Kigezo hiki huzingatia viashiria kadhaa vya maendeleo na ustawi, hususan, muda wa kuishi baada ya kuzaliwa, elimu, na wastani wa kipato cha mwananchi. Kwa kutumia kigezo hiki Tanzania ni nchi ya pili kwa ustawi wa maisha ya wananchi katika Ukanda wa Afrika Mashariki baada ya Kenya iliyofikia alama 0.555 katika kipindi hiki.

**32. Mheshimiwa Spika**, mafanikio ya Tanzania ni matokeo ya jitihada zinazochukuliwa na Serikali katika kuboresha upatikanaji wa huduma za jamii kama vile elimu, afya, maji safi na salama, na umeme katika maeneo ya vijijini na mijini. Mfano, idadi ya wananchi waliofikiwa na huduma ya umeme hadi Machi 2017 ilifikia asilimia 67.5 ikilinganishwa na asilimia 40 iliyokuwa imefikiwa Aprili, 2016. Kwa maeneo ya mijini, idadi ya wananchi waliopata umeme ilifikia asilimia 97.3 Machi 2017 ikilinganishwa na asilimia 63.4 mwaka 2014/15, na upande wa maeneo ya vijijini ilifikia asilimia 49.5 Machi 2017 ikilinganishwa na asilimia 21.0 mwaka 2014/15. Kwa upande wa upatikanaji wa maji, idadi iliongezeka kutoka watu 21,900,000 Juni 2016 hadi 22,951,371 Machi 2017. Kumekuwa na mafanikio pia kwa upande wa elimu, ambapo



uandikishaji wa wanafunzi wa darasa la kwanza uliongezeka kutoka milioni 1.5 mwaka 2014 hadi milioni 2.1 mwaka 2016. Vile vile, idadi ya wananchi wanaonufaika na huduma ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) imeongezeka kutoka 3,377,023 mwaka 2015/16 hadi 3,880,088 Machi 2017. Wanufaika wa Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF) wameongezeka kutoka 8,717,130 mwaka 2015/16 hadi kufikia wanufaika 9,573,906 Machi 2017.

**33. Mheshimiwa Spika**, pamoja na kupunguza umasikini wa mahitaji ya msingi, ni dhamira ya Serikali kuhakikisha kuwa idadi ya Watanzania wanaokosa mlo kwa siku au kuishi kwa mlo mmoja inapungua kutoka kiwango cha asilimia 9.7 kwa sasa kufikia asilimia 5.7 na 4.4 ifikapo mwaka 2020 na 2025, kwa mtiririko huo. Hatua zinazochukuliwa kufikia lengo hili ni pamoja na kuimarisha uzalishaji na hivyo upatikanaji wa chakula katika kaya; kuongeza fursa za ajira mijini na vijijini; kuendelea na mpango wa kusaidia kaya masikini; na kuwezesha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wajasiriamali kupitia mifuko ya maendeleo ya vijana, wanawake na wajasiriamali wadogo.

**34. Mheshimiwa Spika**, licha ya mafanikio yaliyofikiwa, kiwango cha umaskini kwa maeneo ya vijijini bado ni kikubwa ikilinganishwa na maeneo ya mijini. Umaskini vijijini umepungua kutoka asilimia 39.4 mwaka 2007 hadi asilimia 33.3 mwaka 2012 ikimaanisha kuwa japo vijijini umaskini unapungua lakini bado ni chini ya wastani wa kitaifa. Mantiki yake ni kuwa kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi haijaligusa kundi kubwa la wananchi wa vijijini, ambao wengi wao hutegemea shughuli za kilimo, ufugaji na uvuvi. Sekta hizi, ambazo ndizo msingi wa ustawi wa maisha ya watu wa vijijini, zimekuwa na tija na kasi ndogo ya ukuaji kwa kipindi chote. Shabaha ya Serikali ni kupunguza wastani wa umaskini vijijini kutoka kiwango cha sasa cha asilimia 33.3 hadi kufikia asilimia 19.7 na 15 mwaka 2020 na mwaka 2025, kwa mtiririko huo.

**35. Mheshimiwa Spika**, kipimo cha mgawanyo wa kipato miongoni mwa wananchi (Gini coefficient) kwa upande wa

Tanzania Bara kinaonesha kuwa tofauti ya kipato imepungua kutoka 0.37 mwaka 2006/7 hadi 0.34 mwaka 2011/12. Hata hivyo, tofauti ya kipato kati ya jiji la Dar es Salaam na maeneo ya miji mingine na ile ya maeneo ya vijijini ni kubwa zaidi. Hali hii imechangiwa na tofauti ya upatikanaji wa huduma, miundombinu, fursa za ajira, athari za mazingira na mabadiliko ya tabia nchi katika shughuli msingi za jamii husika.

**36. Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Utafiti wa Afya ya Uzazi na Mtoto na Viashiria vya Malaria Tanzania 2015/16, vifo vya watoto wachanga chini ya mwaka mmoja vimepungua kutoka 51 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi 43 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16, vifo vya watoto chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 81 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2010 hadi vifo 67 kwa vizazi hai 1,000 mwaka 2015/16. Kushuka kwa viashiria hivi kunatokana na kuimarika kwa upatikanaji wa huduma za msingi za kijamii ikiwemo afya ya uzazi na mama na mtoto nchini.

**37. Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu hali ya uchumi yapo katika kitabu cha Hali ya Uchumi kwa mwaka 2016.

## **UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2016/17**

### **Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo 2016/17**

**38. Mheshimiwa Spika**, mwaka 2016/17 ulikuwa mwaka wa kwanza wa utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano. Mpango huu utatekelezwa hadi 2020/21, ambapo msukumo ni kuchochea mageuzi ya uchumi kupitia ujenzi wa uchumi wa viwanda na kufungamanisha maendeleo ya uchumi na maendeleo ya watu. Kwa kuzingatia hili, Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2016/17 ulijielekeza katika maeneo makuu manne ya kipaumbele, ikiwa ni:-

(i) Kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda;

- (ii) Kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu;
- (iii) Kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na
- (iv) Kuimarisha usimamizi wa utekelezaji wa Mpango.

**39. Mheshimiwa Spika**, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa 2016/17 yamefafanuliwa kwa kina katika hotuba za mipango na bajeti za Mawaziri wa sekta husika. Kwa maana hiyo nitajikita kuelezea hatua zilizofikiwa katika utekelezaji wa baadhi tu ya miradi ya maendeleo kwa mwaka 2016/17.

### **Miradi Iliyopewa Msukumo wa Kipekee**

**40. Mheshimiwa Spika**, Hii ni miongoni mwa miradi ya kimkakati iliyobainishwa kwa utekelezaji katika Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano, 2016/17 – 2020/21. Utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:

(i) **Ujenzi wa Reli ya Kati**: kusainiwa kwa mkataba wa kusanifu na kujenga awamu ya kwanza ya mradi kutoka Dar es Salaam – Morogoro (Km 205) ambapo mkandarasi ameanza maandalizi ya ujenzi ikiwemo ujenzi wa kambi, ofisi pamoja na kiwanda cha kukarabati mataruma. Mkandarasi amelipwa Shilingi bilioni 300 malipo ya awali (advance payment) na Mheshimiwa Rais alizindua kazi ya ujenzi tarehe 12 Aprili 2017. Taratibu zinazoendelea ni kupata fedha na kuendelea na ujenzi sehemu za reli zilizobakia. Kwa sehemu ya Morogoro hadi Makutupora (Km 336), Serikali inaendelea na mazungumzo na Mkandarasi aliyepatikana; na kwa sehemu za Makutupora hadi Tabora (Km 294), Tabora hadi Isaka (Km 133) na Isaka hadi Mwanza (Km 249), Serikali ipo kwenye mazungumzo na baadhi ya mabanki ambayo yameonesha nia ya kutoa mkopo nafuu wa benki kwa ajili ya ujenzi.

(ii) **Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania**: Ndege mbili (2) zenye uwezo wa kubeba abiria 76 kila moja zilinunuliwa na zilianza kutoa huduma tangu Oktoba 2016. Vile vile, maandalizi ya ununuzi wa ndege nyingine 4 yamekamiliwa

na mikataba imesainiwa, ambapo malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Marekani milioni 56.89 tayari yamefanyika. Kati ya ndege hizo, moja inategemewa kuwasili Julai 2017; mbili zinategemewa kuwasili Juni 2018, na ya mwisho, ambayo itakuwa ya masafa marefu yenye uwezo wa kubeba abiria 262 inategemewa kuwasili Julai 2018.

**(iii) Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga:** maandalizi yote ya ujenzi wa miradi hii yamekamilika, ikiwa ni pamoja na kutenga fedha kwa ajili ya malipo ya fidia kwa wananchi watakaopisha mradi. Vile vile, kampuni ya *Sichuan Hongda (Group) Corporation Ltd*, ambayo ndio mbia katika miradi hii, wametenga jumla ya Dola za Kimarekani milioni 300 kwa ajili ya kulipia sehemu ya mtaji (equity) wao katika miradi. Mfumo uliokubalika na pande zote mbili ni mwekezaji kujenga mtambo wa kufua umeme, kumiliki na kuuendesha (Build Own and Operate, BOO). Mauziano ya umeme kwa TANESCO hayatajumuisha gharama za uwekezaji.

**(iv) Mradi wa Bomba la Mafuta kutoka Hoima Uganda – Bandari ya Tanga**

Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kusainiwa kwa mkataba wa makubaliano ya awali; kutolewa kwa vivutio vya kodi; kusainiwa kwa *Inter- Governmental Agreement*; kufanyika kwa tathmini ya njia ya bomba; kufanyika kwa tathmini ya mahitaji ya njia ya bomba; kufanyika kwa tathmini ya masuala ya kijamii na mazingira; kufanyika kwa upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa gati ya kupokelea mafuta – Chongoleani katika bandari ya Tanga; na kutangazwa kwa zabuni za kuwapata wataalam elekezi kwa ajili ya uchunguzi wa udongo.

**(v) Ununuzi na Ukarabati wa Meli kwenye Maziwa Makuu:**

Hatua iliyofikiwa ni kuendelea na taratibu za ununuzi kwa ajili ya ujenzi wa meli mpya kwa ajili ya usafirishaji wa abiria na mizigo katika ziwa Victoria na ukarabati mkubwa wa Mv. Victoria na Mv. Butiama. Kwa upande wa Mv. Liemba

katika ziwa Tanganyika, mjenzi amepatikana ambaye ni M/ S LEDA SHIPYARD. Ujenzi wa meli mbili za mizigo ziwa Nyasa umekamilika.

**(vi) Uanzishwaji wa Shamba la Miwa na Kiwanda cha Sukari Mkulazi:** Shilingi Billioni 2 tayari zimewekezwa katika mradi huu. Kazi zilizofanyika ni: kupima ubora wa udongo; vitalu vya mbegu za miwa vimeandaliwa; na taratibu za kupata huduma ya wataalam wa kufanya upembuzi yakinifu, uchunguzi wa mbegu za miwa, tathmini ya athari za mazingira na ujenzi wa barabara za kuingia katika eneo la mradi zinaendelea.

**(vii) Ujenzi wa Mitambo ya Kusindika Gesi Kimiminika:** Hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kupatikana kwa eneo la mradi Likong'o mkoani Lindi; kuundwa kwa timu ya majadiliano na kuandaliwa kwa hadidu za rejea, kupitia nyaraka muhimu zinazohusu mradi (sera, sheria, mikataba, kanuni na mikakati ya Serikali); na kuanza kwa majadiliano na kampuni zinazoshiriki katika mradi juu ya masuala yatakayozingatiwa katika kuandaa mkataba kati ya kampuni husika na Serikali (Host Government Agreement – HGA).

**(viii) Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi**

**a. Kituo cha Biashara cha Kurasini:** kiasi cha fidia kilicholipwa kwa ajili ya kupata eneo la mradi ni Shilingi bilioni 101.04 na wananchi 1,019 tayari wamelipwa fidia. Eneo hili kwa sasa lipo chini ya umiliki wa Serikali kwa asilimia 100 na hivyo maandalizi ya mpango mahsusi wa uwekezaji katika eneo hilo yanaendelea.

**b. Eneo Maalum la Uwekezaji la Bagamoyo:** Shilingi bilioni 26.66 zimetumika kulipa fidia kwa wananchi 1,155 kati ya 2,273 wanaopaswa kupisha mradi kwenye eneo la hekta 2,339.6.

**c. Eneo Maalum la Uwekezaji la Mtwara:** Tayari eneo la hekta 10 kati ya hekta 110 za eneo lililotengwa kwa ajili ya

Mtwara SEZ limetangazwa kwa ajili ya matumizi ya bandari huru (Freeport Zone) na maandalizi ya kuweka miundombinu, hususan barabara, kwa eneo hilo yanaendelea.

## Kujenga Msingi wa Uchumi wa Viwanda

41. **Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza azma ya kujenga uchumi wa viwanda, mwelekeo umeanza kuwa vizuri. **Miradi ya viwanda** mbalimbali imeanzishwa kutokana na mchango wa sekta binafsi katika mkoa mbalimbali nchini, kwa mfano kwa mkoa wa Pwani una jumla ya miradi mipya ya viwanda 82. Aidha, baadhi ya miradi mikubwa ya viwanda iliyozinduliwa na kuwekwa mawe ya msingi kwa mkoa wa Pwani pekee ni pamoja na:- viwanda viwili vya Tywford Tiles (Chalinze) na Goodwill Ceramic (Mkuranga) vya kutengeza marumaru (tiles); kiwanda cha nondo cha Kiluwa Steel Industries Ltd (Mlandizi Pwani) ambacho kimeanza uzalishaji; kiwanda cha *Global Packaging* (Mailimoja Pwani) ambacho kinafanya kazi; kiwanda cha kutengeneza juisi ya matunda cha Bakhresa Food Product Ltd (Mkuranga) ambacho kimezinduliwa na kinafanya kazi; kiwanda cha Elyven Agric Co. Ltd (Bagamoyo); kiwanda cha Juisi cha Sayona Fruits Ltd (Mboga Pwani); na kiwanda cha KEDS Tanzania Co. Ltd (Kibaha Pwani).

42. **Mheshimiwa Spika**, Serikali imekuwa na mchango mkubwa kuwezesha sekta binafsi kuwekeza katika viwanda hivi, ikiwa ni pamoja na kusaidia upatikanaji wa ardhi, kuweka miundombinu inayohitajika, na kutoa vibali vya ujenzi na pia vivutio. Halmashauri na Serikali za Mitaa katika maeneo haya zimekuwa na msaada na ushirikiano mkubwa kwa wawekezaji ikiwemo kutoa maeneo ya viwanda ili kuhamasisha uwekezaji. Mathalan, Maswa wameanzisha kiwanda cha kuzalisha Chaki cha Maswa Youth Enterprises Ltd kwa utaratibu huo. Nitumie fursa hii kuwapongeza kwa dhati viongozi wa mkoa, wilaya, halmashauri na Serikali za Mitaa walioitikia kwa dhati wito wa Serikali kujielekeza katika kuvutia na kuwezesha uwekezaji. Niwatake pia viongozi wa Halmashauri zote nchini kuiga mfano wa wenzao

wanaofanya jitihada zote katika kuhakikisha kuwa Halmashauri zinaandaa mazingira mazuri na maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya sekta binafsi.

**43. Mheshimiwa Spika**, Serikali pia kupitia mashirika yake mbalimbali imeanza kuwekeza katika ujenzi wa viwanda, mwitiko wa pekee na wa kupongezwa ni wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, ambapo PPF na NSSF wanashirikiana kuwekeza katika kilimo cha miwa na uzalishaji wa sukari katika eneo la Mkulazi na Mbigiri (Morogoro); na LAPF wanajenga machinjio ya kisasa ya nyama (kwa Makunganya – Morogoro). Shirika la Taifa la Maendeleo (NDC) linashirikiana na sekta binafsi kwa ajili ya uwekezaji katika eneo la viwanda la TAMCO – Kibaha kwa uendelezaji wa viwanda vya nguo na uunganishaji wa magari na matrekta, ambapo kiwanda cha kuunganisha matrekta kimefikia hatua ya kuanza majaribio. Hatua nyingine zinazoendelea chini ya NDC ni pamoja na jitihada za kufufua Kiwanda cha General Tyre (Arusha); hatua za awali za uwekezaji katika mradi wa uchenjuaji wa Magadi Soda (Bonde la Engaruka). NDC pia kwa ubia na kampuni ya TCIMRL ya China imewekeza katika miradi ya Mchuchuma na Liganga.

### **Ujenzi wa Miundombinu na Mazingira Wezeshi**

**44. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa uchumi wa viwanda unahitaji miundombinu ya uhakika. Hivyo, Serikali imeendelea na utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuimarisha na kuboresha miundombinu na huduma za uchumi wa viwanda. Miongoni mwa miradi hii ni: ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi II (MW 240); upanuzi wa mtambo wa kufua umeme wa Kinyerezi I (MW 185); ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kV 400 Iringa – Singida - Shinyanga (km 670), kV 220 Makambako – Songea (km 250), na *North West Grid* kV 400 (Mbeya – Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi km 1,148); usambazaji umeme Vijijini na Makao Mkuu ya Wilaya (REA Turnkey Phase III), ambapo wateja 146,831 sawa na asilimia 58.7 ya lengo wameunganishwa; na ukarabati wa njia ya reli ya kati. Kwa upande wa barabara

hatua iliyofikiwa ni kukamilika kwa ujenzi wa barabara za Masasi – Songea – Mbambabay, sehemu ya Namtumbo – Tunduru (km 193), na Tunduru – Mangaka – Mtambaswala (km 202.5); barabara ya Dodoma – Babati (km 261); Bagamoyo – Msata na daraja la Ruvu chini; na kukamilika kwa Daraja la Kilombero katika barabara ya Ifakara – Mahenge. Ujenzi wa barabara ya Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi unaendelea na umefikia asilimia 16.4; na ujenzi wa barabara za juu za TAZARA na *Interchange* ya Ubungo umeanza.

### **Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu**

**45. Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu Serikali inaendelea kutekeleza sera ya elimumsingi bila malipo; uboreshaji wa miundombinu na huduma za kujifunzia na kufundishia; kukamilika kwa ujenzi wa mabweni katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kutoa mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu; kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Kampasi ya Mloganzila; na kukamilika kwa ukarabati wa vyuo vya ualimu kumi. Katika kuimarisha ujuzi na stadi za kazi, Serikali imekamilisha matayarisho ya Sera ya Taifa ya Ajira ya mwaka 2017, Miongozo ya Mafunzo Kazini kwa vitendo kwa wanafunzi (Apprenticeship Framework) na mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu (Internship Framework). Vile vile, Serikali imeingia mikataba na viwanda vya TOOKU Garment na Mazava Fabrics kwa ajili ya kutoa mafunzo ya stadi za ubunifu na ushonaji wa nguo viwandani. Maeneo mengine yaliyozingatwa ni pamoja na kupanua miundombinu ya upatikanaji wa maji safi na salama mijini na vijijini; huduma za afya na upimaji wa maeneo ya makazi.

**46. Mheshimiwa Spika**, maeneo mengine yaliyoendelea kutekelezwa ni yale yaliyotoa fursa za ajira na ushiriki wa wananchi wengi katika shughuli za uchumi wa viwanda, ikiwa ni pamoja na: kuandaliwa kwa program ya muda mrefu na mfupi ya upimaji na umilikishaji wa ardhi hususan kwa matumizi ya kilimo; kukamilika kwa ukarabati wa



maghala 106 katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Mufindi, Mbeya, Songea, Kalambo, Mbozi, Momba na Njombe; na kuingizwa nchini kwa tani 231,140 za mbolea.

**47. Mheshimiwa Spika, katika kuhamishia Shughuli za Serikali Kuu Dodoma:** awamu ya kwanza imekamilika ambapo majengo ya ofisi za Wizara katika kipindi cha mpito na nyumba za makazi kwa baadhi ya viongozi zimepatikana. TBA na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma wanaendelea na kukamilisha ukarabati wa nyumba za makazi na ofisi. Vile vile, Serikali kwa kupitia Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma inaendelea na upimaji wa viwanja vya makazi na ofisi, ambapo watumishi wa Umma wameandaliwa mkakati maalum utakaosaidia upatikanaji wa viwanja kwa ajili ya makazi. Aidha, Shirika la Nyumba la Taifa linaendelea na ujenzi wa nyumba mpya 300 za makazi na zinazotarajiwa kukamilika Septemba, 2017. Kwa upande mwingine, Serikali inaendelea na mazungumzo na kampuni binafsi kutoka Switzerland, China na Zimbabwe na pia ya ndani ambayo yameonesha nia ya kushiriki katika ujenzi wa miundombinu ya maji kwa mji mpya wa Dodoma. Taasisi za Serikali kama vile TBA, TANESCO, SUMATRA, TEMESA, TANROADS, TTCL na Halmashauri ya Manispaa ya Dodoma zimekamilisha maandalizi ya awali ya kuboresha miundombinu muhimu inayohitajika kuwezesha uendeshaji wa Serikali bila vikwazo katika kipindi hiki.

### **Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo**

**48. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2016/17 Serikali ilipanga kutumia Shilingi bilioni 11,820.503 kwa ajili ya bajeti ya maendeleo, ambapo, Shilingi bilioni 8,702.697 zilikuwa za ndani na bilioni 3,117.805 za nje. Hadi Aprili 2017, fedha zilizokuwa zimetolewa ni Shilingi bilioni 4,516.7, sawa na asilimia 38 ya bajeti ya maendeleo, ikijumuisha fedha zilizotolewa kwa Halmashauri. Fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha Shilingi bilioni 3,608.9 fedha za ndani na Shilingi bilioni 907.8 fedha za nje. Kwa ujumla kiasi cha fedha kilichotolewa ni chini ya maoteo ya mtiririko wa fedha kwa wakati husika. hii ilichangiwa na sababu mbalimbali,**

ikiwa ni pamoja na kuchelewa kupatikana kwa misaada na mikopo ya kibiashara kufuatia majadiliano na Washirika wa Maendeleo na mabenki kuchukua muda mrefu, kupanda kwa riba ya mikopo ya kibiashara katika soko la fedha kimataifa hivyo Serikali kufikia maamuzi ya kuahirisha kuchukua mikopo husika. Hata hivyo, miradi ambayo ina vyanzo vya fedha mahsusi kama vile Wakala wa Nishati Vijijini (REA), Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), Mfuko wa Barabara, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Mfuko wa Maji na Mfuko wa Reli ilipatiwa fedha zote zilizokusanywa katika kipindi husika.

**49. Mheshimiwa Spika**, Mikakati mbalimbali imewekwa kuhakikisha fedha zilizopangwa kwa ajili ya matumizi ya miradi ya maendeleo zinapatikana kwa kiasi cha kuridhisha. Miongoni mwa mikakati hiyo ni pamoja na kuendelea na majadiliano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo ili kuhakikisha fedha za misaada na mikopo nafuu zinapatikana kama zilivyoahidiwa; kuimarisha makusanyo ya ndani ya Serikali; na kuendelea kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi nchini. Aidha, Serikali ipo katika hatua za mwisho za majadiliano na benki ya Credit Suisse ili kupata mkopo wa Dola za Marekani Milioni 500 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

## **Changamoto za Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya 2016/17**

**50. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya mwaka 2016/17 umekabiliwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na mwenendo wa upatikanaji wa fedha, upatikanaji wa maeneo ya uwekezaji na matayarisho haffu ya miradi ambapo kwa baadhi ilionekana bayana kuwa ama ipitiwe upya au majadiliano yaanze upya ili kulinda maslahi ya Taifa.

**(i) Mwenendo wa Upatikanaji wa Fedha:** Kwa upande wa upatikanaji wa fedha kutoka makusanyo ya mapato ya ndani, haya yamekuwa yakiongezeka na yamekuwa yakipatikana kwa wakati. Kumekuwepo na kuchelewa

kupatikana kwa mikopo yenye masharti nafuu na ya kibiashara kutoka nje; na Majadiliano kuchukua muda mrefu hivyo kuchelewa kupatikana kwa fedha za kuelekeza baadhi ya miradi ya maendeleo.

Kumekuwa na kuchelewa kwa ukamilishaji wa taratibu za kufikia maafikiano na wakopeshaji, hivyo, mikopo kuchelewa kupatikana. Katika mwaka 2016/17, kwa makusudi kabisa, ilionekana ipo haja ya kusitisha mchakato wa kukopa baada ya riba za mabenki duniani kupanda sana kufikia wastani wa asilimia 9 kutoka asilimia 6.

Zipo hatua mbalimbali zilizochukuliwa kukabiliana na changamoto hii. Pamoja na kuzidi kuimarisha makusanyo ya ndani ya Serikali, msisitizo ni kuhakikisha kuwa fedha zinazopatikana zinaelekezwa kwenye miradi yenye tija; kuendelea kuboresha mazingira ya uendeshaji biashara ili kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi nchini, ikiwa ni pamoja na wawekezaji wadogo hususan upatikanaji wa mikopo nafuu na maeneo ya uwekezaji na pia kuhuisha sheria, kanuni, taratibu na kupunguza ada, kodi na tozo za uwekezaji na uendeshaji biashara. Aidha, Serikali inaendelea na majadiliano na baadhi ya taasisi za fedha na mabenki ili kupata mkopo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**(ii) Upatikanaji wa Maeneo ya Uwekezaji:** Baadhi ya miradi imekuwa na utekelezaji hafifu kutokana na kuwepo migogoro ya ardhi na kutokamilika kwa hatua za kulipa fidia. Uhakiki umeonesha kuwepo kwa udanganyifu katika gharama na watu wanaostahili kulipwa fidia katika maeneo mengine. Hali hii ililazimisha madai kupitiwa upya na hivyo kuchelewa kuanza kwa utekelezaji. Hatua zilizochukuliwa na Serikali ni kuongeza kasi ya kupata Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZ na SEZ) na maeneo ya viwanda kwa ngazi zote za mikoa. Halmashauri zote zimeagizwa na tayari baadhi zimetenga maeneo ya viwanda na biashara ndogo ndogo. Vile vile, mashirika ya umma yenye ardhi kama vile NDC yametumia maeneo hayo kuingia ubia na wawekezaji binafsi.

(iii) **Mapungufu katika Maandalizi ya Miradi:** Serikali katika hatua za kuimarisha maandalizi ya miradi, ambapo imeandaa na kuweka utaratibu wa maofisa kutumia kikamilifu Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma. Pamoja na kuandaa Mwongozo huo, Serikali imechukua hatua ya kutoa mafunzo kwa wataalam 422 wanaohusika na uratibu wa miradi ya maendeleo kwa Mikoa na Halmashauri zote pamoja na Wizara, Taasisi, Idara Zinazojitegemea na Wakala wa Serikali.

**51. Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yapo katika kitabu cha Mpango (Sura ya Tatu).

## **MPANGO WA MAENDELEO WA MWAKA 2017/18**

### **Mazingira Yanayoongoza Mpango**

**52. Mheshimiwa Spika,** Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21). Msukumo wake ni kufanikisha utekelezaji wa malengo ya Mpango wa Miaka mitano hasa kwa miradi ambayo utekelezaji wake unaendelea tokea 2016/17.

**53. Mheshimiwa Spika,** utayarishaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 umezingatia yafuatayo kama mwongozo: Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2016/17 - 2020/21); sera na mikakati mbalimbali ya kisékta, kikanda (EAC na SADC) na Umoja wa Afrika; Agenda ya 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu; Agenda ya 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Ilani ya CCM ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015. Vile vile, umezingatia mwenendo wa uchumi wa Taifa, kikanda na kidunia kwa mwaka 2016 na maoteo kwa mwaka 2017. Umezingatia pia hali halisi ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2016/17 na changamoto za utekelezaji zilizojitokeza.

## Ushirikishwaji wa Jamii katika Maandalizi ya Mpango

**54. Mheshimiwa Spika**, mchakato wa maandalizi ya Mpango huu umezingatia dhana ya ushirikishi mpana wa wadau ikiwa ni pamoja na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi za Serikali, Taasisi za Utafiti na Elimu ya Juu, Sekta Binafsi na Washirika wa Maendeleo. Pia uliweza kupata maoni ya Waheshimiwa Wabunge katika mkutano wa Tano wa Bunge la 11 kuhusu Mapendekezo ya Serikali kwa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/18. Katika mkutano tajwa, waheshimiwa wabunge walitoa maoni na mchango mkubwa uliotuwezeshwa kuandaa Mpango huu. Miongoni mwa maoni mahsusi ya Waheshimiwa Wabunge ni kuwa: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *standard gauge* upewe kipaumbele; kuboresha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara; utekelezaji wa mkakati wa kujenga zahanati katika kila kijiji na vituo vya afya kila kata; kuimarisha upatikanaji wa madawa na vifaa tiba; kuendeleza maeneo ya viwanda vidogo, na maeneo mahsusi ya EPZ/SEZ; kutoa kipaumbele kwa utekelezaji wa miradi ya makaa ya mawe - Mchuchuma na chuma - Liganga; kuboresha elimu ya juu na kuongeza wigo wa utoaji wa mikopo kwa wanafunzi; kuboresha miundombinu ya barabara; na programu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

**55. Mheshimiwa Spika**, maoni na ushauri wa wadau wengine ambao umezingatiwa katika maandalizi ya Mpango huu ni pamoja na: Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango; upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu na nafuu; uimarishwaji wa miundombinu msingi ya bandari na nishati ya umeme; na kuboresha utoaji wa huduma msingi za ustawi wa jamii hususan elimu, afya, maji, uboreshaji wa mipango miji, nyumba na makazi, na utunzaji wa mazingira.

## Shabaha na Malengo ya Uchumi Jumla kwa mwaka 2017/18

**56. Mheshimiwa Spika**, Shabaha na malengo ya uchumi jumla katika kipindi cha mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:-

- (ix) Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 7.1 mwaka 2017 ikilinganishwa na asilimia 7.0 mwaka 2016;
- (x) Kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja;
- (xi) Kuongeza ukusanyaji wa mapato ya ndani (ikijumuisha ya Serikali kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa) kufikia asilimia 16.5 ya Pato la Taifa;
- (xii) Mapato ya kodi kufikia asilimia 14.2 ya Pato la Taifa mwaka 2017/18;
- (xiii) Matumizi ya Serikali kufikia asilimia 24.9 ya Pato la Taifa;
- (xiv) Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) ya asilimia 3.8 ya Pato la Taifa;
- (xv) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango kinachokidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4); na
- (xvi) Kuhakikisha utulivu wa thamani ya Shilingi ya Tanzania.

## **Maeneo ya Kipaumbele 2017/18**

**57. Mheshimiwa Spika**, kwa kuzingatia shabaha na malengo haya, miradi iliyobainishwa kuwa ya kipaumbele kwa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2017/18 ni ile inayotarajiwa kutoa matokeo makubwa kuendana na malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 na Mpango wenyewe. Mingi ya miradi hii utekelezaji wake ulianza mwaka 2016/17, hivyo inaendelea. Hii ni pamoja na miradi ya: ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*; Kuhuisha Shirika la Ndege Tanzania, hususan kukamilisha malipo ya ununuzi wa ndege 4; miradi ya Chuma cha Liganga na Makaa ya Mawe ya Mchuchuma; Uanzishwaji/Uendelezaji wa

Kanda Maalum za Kiuchumi; Mtambo wa Kuchakata Gesi Asilia - Lindi; na Shamba la Kilimo na Uzalishaji Sukari Mkulazi. Malengo ya utekelezaji kwa maeneo haya kwa mwaka 2017/18 yameainishwa katika kitabu cha Mpango wa Maendeleo kwa Mwaka 2017/18 (Sura ya nne).

**58. Mheshimiwa Spika,** miradi mingine ya kipaumbele itakuwa katika maeneo yafuatayo:

**(a) Ujenzi wa Msingi wa Uchumi wa Viwanda:** ikihusisha miradi ya:- Uendelezaji wa Eneo la Viwanda TAMCO - Kibaha; Tathmini ya matumizi ya eneo la Kiwanda cha General Tyre – Arusha; Mradi wa Magadi Soda – Bonde la Engaruka, Arusha; kuimarisha Mfuko wa Taifa wa Maendeleo ya Wajasiriamali (NEDF); uendelezaji wa maeneo ya viwanda vidogo katika mikoa ya Morogoro, Dar es Salaam, Mbeya, Mwanza, Kigoma na Mtwara; ujenzi wa ofisi za SIDO katika mikoa mipya. Maeneo mengine ni pamoja na kuendeleza viwanda vya ngozi, kupanua mnyororo wa thamani wa pamba hadi nguo na uzalishaji wa madawa na vifaa tiba nchini. Kwa lengo hili, Serikali itaendelea kuhamasisha uwekezaji binafsi hususan katika viwanda vinavyotumia malighafi zinazopatikana kwa wingi nchini ikiwa ni pamoja na viwanda vya kusindika nyama, maziwa, maji, misitu, chokaa, mawe urembo, *gypsum* na mazao ya vyakula na matunda. Serikali itaendelea kuziimarisha taasisi zake ili kuwekeza katika viwanda kwa njia ya PPP.

**(b) Kufungamanisha Ukuaji wa Uchumi na Maendeleo ya Watu:** Miradi katika eneo hili ni ile inayolenga kuimarisha upatikanaji wa fursa za: **Elimu na Mafunzo ya Ufundi:** Kugharamia Elimumsingi bila malipo; Kupanua ruzuku na mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; Ununuzi wa vifaa kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum; ukarabati na upanuzi wa Maktaba ya Mkoa – Dodoma; na ujenzi wa Vyuo vitano vya VETA katika Mikoa ya Geita, Simiyu, Njombe, Rukwa na Kagera. Kwa upande wa **Afya na Maendeleo ya Jamii ni:** hatua zitaendelezwa za kuboresha Hospitali za Rufaa na mikoa; kuhakikisha upatikanaji wa vifaa vya kisasa; kuimarisha upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na

vitendanishi katika hospitali, vituo vya afya na zahanati; kuongeza uhibitaji wa magonjwa ya kuambikiza; na kudhibiti maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI, hususan kwa vijana.

**Miradi ya Maji:** ukarabati na upanuzi wa huduma za maji Vijijini; kuboresha huduma za maji katika Jiji la Dar es Salaam; mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kwenda Kahama, Nzega, Igunga, Tabora hadi Sikonge; ujenzi, ukarabati na upanuzi wa huduma za maji mijini na vijijini; na kutoa maji mto Ruvuma kwenda Manispaa ya Mtwara-Mikindani; kujenga na kuimarisha hifadhi ya vyanzo vya maji na misitu, upandaji miti, uvunaji wa maji, kuhimiza matumizi ya teknolojia jadidifu na hifadhi ya mazingira. Hatua nyingine ni pamoja na kupanua upatikanaji wa maji safi, utunzaji wa mazingira, na kuimarisha uhimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabia nchi.

**(c) Mazingira Wezeshi kwa Uendeshaji Biashara:** katika eneo hili, Serikali itaendelea na azma yake ya kupanua miundombinu ya huduma za kiuchumi kufikia azma yake ya kuboresha mazingira ya biashara ikihusisha miradi inayoendelea ya ukarabati wa miundombinu ya reli; miradi ya barabara na madaraja katika barabara za Kidahwe – Kasulu – Kibondo – Nyakanazi, Manyoni – Tabora – Uvinza, Tabora – Koga – Mpanda; Ujenzi wa barabara za juu za TAZARA na Ubungo *Interchange*; ujenzi wa Daraja la Selander na miundombinu ya mabasi yaendayo haraka (awamu ya II, III na IV) jijini Dar es Salaam. Aidha, miradi ya bandari ikijumuisha bandari za Dar es Salaam, Mtwara, Tanga, Bagamoyo, bandari kavu ya Ruvu na bandari za Maziwa Makuu (Victoria, Tanganyika na Nyasa). Kwa upande wa usafiri wa anga, Serikali itaendelea na ujenzi wa jengo la abiria (terminal III) katika uwanja wa ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere; upanuzi wa uwanja wa ndege wa Kigoma, Tabora na Mwanza; ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege vya Geita, Sumbawanga, Shinyanga, Mtwara, Musoma, Iringa na Songea; na ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa Kilimanjaro.

**(d) Kuimarisha Utekelezaji wa Mpango na Miradi:** Serikali itaendelea kuchukua hatua ya kuimarisha mitaji ya benki za ndani za maendeleo (TIB na TADB) na kuanza utaratibu wa



kuzitumia kama vyombo vyake vya ukusanyaji wa mikopo ya muda mrefu na ya gharama nafuu kwa wawekezaji. Aidha, eneo hili litajumuisha miradi ya kuendeleza na kusimamia matumizi ya ardhi; kuimarisha mipango miji; maendeleo ya nyumba na makazi; kuweka mfumo utakaowezesha nchi kufaidika na ushirikiano wa kikanda na kimataifa; kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria.

Serikali itaendelea kuweka mazingira wezeshi ili kuchochea ushiriki na maendeleo ya sekta binafsi, hususan, sekta binafsi ya ndani, katika utekelezaji wa Mpango na ujenzi wa viwanda. Serikali itaendelea kuboresha kanuni, taratibu na mifumo ya taasisi ya usimamizi wa biashara na uwekezaji nchini. Kwa kuzingatia hili, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

(viii) Kufanya mapitio ya sera, sheria na taratibu zinazochochea ushiriki wa sekta binafsi, ama kuwekeza moja kwa moja au kwa ubia na sekta ya umma;

(ix) Kutenga maeneo ya uwekezaji ili kupunguzia sekta binafsi usumbufu hususan upatikanaji wa ardhi ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo mahsusi ya uwekezaji (EPZ, SEZ na kuanzisha *land bank* chini ya TIC), na kuyaweke maeneo hayo miundombinu msingi, na kuikodisha kwa wawekezaji kwa gharama nafuu;

(x) Kujenga miundombinu wezeshi (barabara, umeme, maji na reli) na kuifikisha katika maeneo ya shughuli za wawekezaji;

(xi) Kusimamia utekelezaji wa sheria na taratibu na kuhakikisha kuwepo kwa amani na usalama;

(xii) Kuimarisha mifuko maalum ya kuchochea ushiriki wa sekta binafsi, kwa mfano *SAGCOT Catalytic Fund* na *PPP Facilitation Fund*;

(xiii) Kuboresha huduma kwa wawekezaji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha "one stop centre" chini ya TIC, bandari

ya Dar es Salaam na vituo vya utoaji huduma ya pamoja mipakani (one stop border post); na

(xiv) Kuweka utaratibu utakaoboresha upatikanaji wa mikopo ya muda mrefu kwa gharama nafuu ikiwa ni pamoja na kuimarisha mitaji ya benki maalum za maendeleo (TADB) na (TIB).

**(e) Kuhamishia Makao Makuu ya Shughuli za Serikali Kuu Dodoma:** katika mwaka 2017/18 Serikali itaendelea na utekelezaji wa azma ya kuhamishia shughuli za Serikali makao makuu Dodoma. Katika utekelezaji wa azma hii, Wizara zimeelekezwa kutenga fedha za kugharamia stahili za watumishi kwa kutumia ukomo wa bajeti uliotengwa kwenye mafungu yao. Ofisi ya Waziri Mkuu inaendelea kuratibu upatikanaji wa maeneo ya kujenga ofisi na nyumba za viongozi wa Serikali kwa kuzingatia mahitaji na maboresho ya mpango wa ardhi katika mji wa Dodoma.

**59. Mheshimiwa Spika,** kwa kuitikia wito wa Serikali wa kujenga uchumi wa viwanda, mifuko ya hifadhi ya jamii imeonesha nia ya kuwekeza katika miradi ya viwanda katika maeneo mbalimbali nchini. Baadhi ya miradi ambayo inatarajiwa kutekelezwa na mifuko hii katika mwaka 2017/18 ni pamoja na ufufuaji wa: kiwanda cha sukari katika Gereza la Mbigiri Dakawa Morogoro; kiwanda cha kutengeneza viatu katika Gereza la Karanga Moshi; kiwanda cha nguo cha urafiki; Dar Es Salaam; kiwanda cha Morogoro Canvas Mill; kiwanda cha chai cha Mponde kilichopo Lushoto Mkoani Tanga; kiwanda cha Kilimajaro Machine Tools, Kilimanjaro (KMTC) na kiwanda cha Kubangua Korosho cha Tandahimba na Newala. Vile vile, mifuko hii inatarajia kuanzisha viwanda vipya katika maeneo mbalimbali, vikiwemo: kiwanda cha dawa; kiwanda cha kuzalisha bidhaa za hospitali na gesi ya oksijeni; kiwanda cha kusindika zabibu, Chinangali Dodoma; viwanda vya kusindika nafaka na ukamuaji wa mafuta; na kiwanda cha kuzalishaji wanga kutokana na zao la muhogo na viazi vitamu huko Lindi.

**60. Mheshimiwa Spika,** maelezo ya kina kuhusu Miradi

ya Kipaumbele yapo katika kitabu cha Mpango (Sura ya Nne).  
**Vihatarishi Vinavyoweza Kuathiri Utekelezaji wa Mpango**

**61. Mheshimiwa Spika**, vipo vihatarishi mbalimbali ambavyo vinaweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Vihatarishi hivyo vinaweza kuwa vya ndani au vya nje. Kihatarishi kikuu cha ndani ni ufinyu wa rasilimali fedha na uwepo wa tofauti za mpangilio wa vipaumbele, mpango-kazi na mtiririko wa upatikanaji fedha baina ya taasisi za utekelezaji. Vihatarishi vya nje ni pamoja na: mitikisiko ya kiuchumi kikanda na kimataifa; majanga asilia na athari za mabadiliko ya tabianchi; na mabadiliko ya kiteknolojia.

**62. Mheshimiwa Spika**, Serikali kwa kushirikiana na wadau katika kutekeleza Mpango huu, imebainisha na kuweka tahadhari kwa kuchukua hatua zifuatazo:- kuandaa bajeti yenye mwelekeo wa kupunguza utegemezi wa kibajeti kwa kuwianisha vyanzo vya mapato na mkakati wa kuyakusanya na kuwianisha matumizi na upatikanaji wa mapato ya Serikali; kuboresha mazingira ya biashara kwa lengo la kuimarisha sekta binafsi kuchangia utekelezaji wa baadhi ya miradi; na kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Mpango na namna bora ya utekelezaji ili kuongeza ushiriki wa jamii na sekta binafsi.

## **Ugharamiaji wa Mpango 2017/18**

### ***Sekta ya Umma***

**63. Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2017/18, Shilingi bilioni 11,999.6 zimetengwa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambapo Shilingi bilioni 8,969.8 ni fedha za ndani na Shilingi bilioni 3,029.8 ni fedha za nje. Hivyo, fedha zilizotengwa katika bajeti ya maendeleo zimeongezeka kutoka Shilingi bilioni 11,820.5 mwaka 2016/17 hadi Shilingi bilioni 11,999.6 kwa mwaka 2017/18, ikiwa ni sawa na asilimia 38 ya bajeti yote. Kiasi hiki ni kikubwa kwa asilimia 1.2 ya makadirio ya kutenga Shilingi bilioni 11.80 kila mwaka kutoka mapato ya Serikali kama ilivyojidhihirisha

katika mapitio ya utekelezaji kwa mwaka 2016/17. Serikali itahakikisha kuwa kiasi cha fedha kilichopangwa kwa matumizi ya maendeleo kinapatikana na kugawiwa kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo iliyokusudiwa na kwa wakati. Hivyo, pamoja na juhudi za kupanua na kukusanya mapato katika vyanzo vya kawaida vya Serikali, msisitizo umewekwa katika kubaini na kukusanya kutoka vyanzo vipya. Mfumo wa ukusanyaji katika baadhi ya maeneo utafanyiwa mabadiliko ili kuongeza ufanisi.

### ***Mashirika na Taasisi za Umma***

**64. Mheshimiwa Spika**, katika historia ya nchi yetu na pia nchi nyingi zinazoendelea, Mashirika ya Umma yamekuwa na mchango mkubwa katika kuchangia maendeleo ya nchi husika. Kwa kutambua hili, Serikali imeelekeza mashirika na taasisi zake za umma za kibiashara kuchangia katika kugharamia utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo nchini. Taasisi hizi zinaweza kutekeleza hili kupitia mapato na/au kwa kukopa kwa ridhaa ya Serikali kutokana na dhamana ya mali zao ili kugharamia utekelezaji wa miradi itakayobainishwa kuwa ya kipaumbele.

### ***Sekta Binafsi***

**65. Mheshimiwa Spika**, kama ilivyojidhihirisha mwaka 2016/17, sekta binafsi, ya ndani na nje, imepokea kwa hamasa wito wa Serikali wa kuchochea uwekezaji hasa katika maeneo mengine zaidi ya kilimo na madini. Serikali kupitia Baraza la Taifa la Biashara itaendelea kusimamia utekelezaji wa maazimio yenye lengo la kuimarisha mazingira wezeshi ya uwekezaji na uendeshaji biashara nchini. Katika kuvutia uwekezaji kwa njia ya ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, Serikali itaendelea kuimarisha Mfuko wa fedha wa miradi ya ubia (PPP Facilitation Fund) kwa lengo la kugharamia uandaaji wa upembuzi yakinifu kwa miradi inayotarajiwa kutekelezwa kwa njia ya ubia kati ya Serikali na sekta binafsi. Matokeo tarajiwa ni ongezeko la uwekezaji wa sekta binafsi katika miradi ya kipaumbele kwa njia ya ubia. Serikali pia imeamua, kwa makusudi kuondoa mlolongo

wa kodi kwa sekta ya kilimo na biashara ndogo ndogo kwa ajili ya kuinua uwekezaji katika sekta hizi. Vile vile, imechukua hatua za kuhakikisha upatikanaji wa maeneo ya viwanda na biashara ndogo kwa urahisi. Msukumo pia umewekwa kuboresha upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu na ya muda mrefu kwa wawekezaji, ikiwa ni pamoja na kuimarisha benki za maendeleo nchini.

**66. Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu Ugharamiaji wa Mpango yapo katika kitabu cha Mpango (Sura ya Tano).

### **Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji wa Taarifa**

**67. Mheshimiwa Spika**, moja ya changamoto za utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ni udhaifu katika ufuatiliaji wa miradi. Udhaifu huu unatokana na changamoto za upatikanaji wa rasilimali fedha pamoja na upungufu wa watumishi wenye uzoefu na utaalim wa ufuatiliaji na tathmini.

**68. Mheshimiwa Spika**, Serikali katika kuimarisha eneo hili imeamua kuweka mfumo wa mafunzo na malezi yatakayoharakisha kuimarisha utaalim wa kupanga, kutayarisha, kusimamia, kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi. Ninatumia fursa hii kuwaelekeza Maafisa Masuhuli kutenga fedha za ufuatiliaji na tathmini kama sehemu ya gharama za utekelezaji wa miradi husika.

**69. Mheshimiwa Spika**, hatua pia zimechukuliwa kwa lengo la kuhuisha nyenzo za ufuatiliaji na tathmini. Hii ni pamoja na kuandaa na kutoa mafunzo juu ya matumizi ya Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma. Kwa mwaka 2017/18, mafunzo yatatolewa kwa maafisa wa ufuatiliaji na tathmini kuwawezesha kujua hatua za msingi katika kuandaa, kuratibu na kutathmini miradi ya maendeleo. Serikali kupitia Tume ya Mipango itaandaa mfumo wa kuhifadhi taarifa za miradi ya maendeleo kwa ajili ya kuimarisha upatikanaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini.

**70. Mheshimiwa Spika**, kwa lengo la kuimarisha vigezo vya kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miradi, Serikali kupitia Tume ya Mipango itaratibu zoezi hilo kupitia Mkakati wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Hatua hii itasaidia kuboresha upatikanaji wa taarifa za ufuatiliaji na tathmini ya miradi husika kwa kuzingatia vigezo vya utekelezaji vilivyokusudiwa kwa kipindi husika.

**71. Mheshimiwa Spika**, maelezo ya kina kuhusu Ufuatiliaji, Tathmini na Utoaji Taarifa yapo katika kitabu cha Mpango (Sura ya Sita).

## MAJUMUISHO NA HITIMISHO

### Majumuisho

**72. Mheshimiwa Spika**, tangu Serikali ilipotangaza dhamira ya kujenga uchumi wa viwanda kumekuwa na mwitiko wa uwekezaji, wa umma na binafsi, unaotia matumaini makubwa. Jitihada hizi hazina budi kuungwa mkono, hususan, kwa kuweka kusudio la kuendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji na uendeshaji biashara nchini. Hivyo, hatua za mapitio ya sera, sheria, kanuni na mfumo taasisi wa usimamizi zitaendelea kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa tunakuwa na mfumo unaoakisi kusudio hili kwa vitendo. Aidha, hasa kutokana na ukweli kuwa sehemu kubwa ya viwanda vitakavyoanzishwa vitatumia malighafi zinazopatikana kwa wingi hapa nchini, hatua za makusudi zitaendelea kuchukuliwa kwa lengo la kuongeza uzalishaji, tija na ubora wa malighafi zinazozalishwa nchini ili kukidhi mahitaji ya soko linalozidi kukua na kubadilika.

**73. Mheshimiwa Spika**, kuna kasi kubwa ya mabadiliko ya mfumo wa maisha na matarajio ya jamii, hasa kundi kubwa la vijana. Matarajio haya ya vijana yanaweza kufikiwa tu ikiwa wataweza kuajiriwa au kuwa na shughuli za kujajiri wenyewe. Kwa mantiki hii ni wajibu wa msingi kabisa wa Serikali kuzidi kupanua fursa za uwekezaji. Uwekezaji unaweza kuwa ama wa Serikali moja kwa moja, ubia kati yake na

sekta binafsi au wa sekta binafsi moja kwa moja. Kwa kutambua hili, Serikali inahitaji sana ushirikiano na mshikamano kati yake na sekta binafsi. Ushirikiano na mshikamano huu unapaswa kuwa mpana na wa kina katika nyanja zote, kuanzia kuibua, kupanga, kutekeleza na kufuatilia na kutathmini hatua za utekelezaji. Katika kutekeleza hilo, msukumo umewekwa katika kuimarisha ushirikiano na sekta binafsi kwa kuandaa mikutano na mashauriano ya mara kwa mara ikiwa pamoja na ya Baraza la Biashara Tanzania (TNBC) itakayojadili na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa changamoto zilizopo.

**74. Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Tano ilitangaza toka mwanzo kabisa azma yake ya kujitanabaisha kuwa ya ukweli na uwajibikaji hasa katika kusimamia matumizi ya rasilimali zinazopatikana kwa manufaa ya Taifa na kila mwananchi. Kutokana na hili, Serikali inaendelea kujielekeza katika kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani kwa kufanyia mapitio ya mifumo na muundo wa usimamizi wa makusanyo ya kodi, malimbikizo ya kodi, kupanua wigo wa kodi kwa kusajili walipa kodi wapya, pamoja na utekelezaji wa mikakati ya kuongeza makusanyo ya kodi. Msukumo pia umewekwa katika kuongeza matumizi ya teknolojia ya kielektroniki ili kupunguza athari za mapungufu ya kibinadamu katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi fedha na kumbukumbu. Hatua hizi zote ndizo zitawezesha ustawi wa uchumi na utekelezaji bora wa Mpango wa Maendeleo.

**75. Mheshimiwa Spika**, mafanikio yaliyopatikana katika uchumi na utekelezaji wa Mpango yamechangiwa na wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi wakiwemo nchi marafiki, washirika wa maendeleo, sekta binafsi na wananchi kwa ujumla. Kwa niaba ya Serikali, ninawashukuru wadau hao kwa michango yao.

**76. Mheshimiwa Spika**, kabla ya kumaliza hotuba yangu napenda kumshukuru Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango Mhe. Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb), Mawaziri na Makatibu Wakuu wa Wizara zote, Wakuu wa Idara za Serikali na Taasisi zinazojitegemea kwa ushirikiano wao wakati wote

wa maandalizi ya kutayarisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18. Kipekee napenda kuwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu Bw. Doto James kwa kusimamia vizuri kazi za kila siku za Wizara. Aidha, niwatambue Bw. Maduka Kessy, Kaimu Katibu Mtendaji, viongozi na watumishi wote wa Tume ya Mipango kwa kufanikisha maandalizi ya hotuba hii.

## Hitimisho

**77. Mheshimiwa Spika**, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge na wananchi wote kwa kunisikiliza. Aidha, hotuba hii na vitabu vya Hali ya uchumi 2016, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18 vinapatikana katika tovuti ya Wizara ya Fedha na Mipango [www.mof.go.tz](http://www.mof.go.tz) na [www.mipango.go.tz](http://www.mipango.go.tz).

**78. Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo naomba sasa Waheshimiwa Wabunge wapokee, kujadili na kupitisha Taarifa ya Hali ya Uchumi 2016 na Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2017/18.

**79. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Hotuba hii ilihusu Hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka mmoja uliopita hadi sasa, vilevile na Mpango wa Maendeleo wa mwaka mmoja wa 2017/2018. Ni hotuba muhimu sana na ni msingi muhimu kwa hotuba itakayotolewa leo jioni ambayo itakuwa ni hotuba ya bajeti. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba nichukue nafasi hii kuwatambulisha baadhi ya wadau wetu wa maendeleo ambao wamefika hapa leo, ambao wako *Speakers gallery, Development Partners Representatives can you stand up please!* Karibuni sana na tunawashukuruni sana kwa niaba ya wananchi wa Tanzania kwa jinsi mlivyoshirikiana nasi katika mipango mbalimbali ya maendeleo ya Taifa letu kwa mwaka huu unaoishia wa fedha. Ahsanteni sana. *(Makofi)*



Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka kwamba tarehe 5 Aprili kabla ya kuanza kwa Mkutano wa Bunge la Bajeti na kama ilivyoelekezwa kwenye Kanuni ya 98(4), Serikali kwa kushauriana na Kamati ya Bajeti ilifanya majumuisho kuzingatia ushauri wa Kamati za Bunge za Kisekta kuhusu utekelezaji wa bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na maombi ya fedha kwa mwaka 2017/2018.

Waheshimiwa Wabunge, tarehe 7 Juni, jana Kamati ya Bajeti, Kamati ya Uongozi na Serikali walikutana kwa mujibu wa Kanuni ya 105(1), kwa lengo la kufanya majumuisho kwa kuzingatia hoja zilizojitokeza wakati wa kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara mbalimbali, kwa mwaka wa fedha 2016/2017 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hizo kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Waheshimiwa Wabunge, katika kikao hicho ambacho mimi nilikuwa ni Mwenyekiti, Serikali ilitoa ufafanuzi kuhusu hoja mbalimbali kwa Kamati ya Bajeti na Kamati ya Uongozi. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge taarifa ya hoja hizo zilizojadiliwa jana itawasilishwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti hapa Bungeni siku ya Jumatatu tarehe 12 Juni, 2017 wakati atakaposoma taarifa ya Kamati ya Bajeti kuhusu hali ya Uchumi wa Taifa kwa mwaka 2016 na Mpango wa Maendeleo ya Taifa kwa mwaka 2016/2017. Pamoja na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa mwaka wa 2016/2017 na mapendekezo ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2017/2018.

Waheshimiwa Wabunge, kwa jinsi hiyo na kwa hatua hii tuliyofikia najua mnahitaji muda, Mheshimiwa Waziri anahitaji muda ili tuweze kukutana hapa saa 10 kamili juu ya alama ambapo Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango ataanza kusoma bajeti ya Taifa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hii sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi leo saa 10 kamili jioni.

*(Saa 5.35 Asubuhi Bunge lilisitishwa hadi Saa 10.00 Jioni)*

(Saa 10.00 Jioni Bunge Lilirudia)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Tunaendelea na Kikao cha 44 cha Mkutano wetu wa Saba. Katibu.

**DKT. THOMAS KASHILILAH – KATIBU WA BUNGE:**

### HOJA ZA SERIKALI

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018**

**SPIKA:** Ahsante sana Katibu wa Bunge, sasa moja kwa moja bila kupoteza muda namkaribisha Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya kusoma Bajeti ya Taifa.

*(Hapa Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliingia ukumbini na kushangiliwa)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, karibu sana. Unayo masaa mawili kamili.

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018. Bajeti hii inawasilishwa kwa kuzingatia matakwa ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Ibara ya 137 ikisomwa pamoja na Sheria ya Bajeti Namba 11 ya mwaka 2015 Kifungu cha 26.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii, nawasilisha vitabu vinne vinavyoelezea kwa kina Makadirio ya Bajeti kwa mafungu. Kitabu cha Kwanza ni Makadirio ya Mapato, Kitabu cha Pili ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Taasisi na Wakala wa Serikali, Kitabu cha Tatu ni Makadirio ya Matumizi ya Kawaida kwa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na Kitabu cha Nne ni Makadirio ya Matumizi ya Maendeleo kwa Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, upo Muswada wa

Sheria ya Fedha wa Mwaka 2017 pamoja na Muswada wa Sheria ya Matumizi ya Serikali wa Mwaka 2017 ambayo ni sehemu ya bajeti hii.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa baraka na amani anayoendelea kujiaalia nchi yetu na pia kwa kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu kuwasilisha Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2017/2018.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda nichukue fursa hii kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuniadini katika dhamana hii kubwa ya kuongoza Wizara nyeti ya Fedha na Mipango. Aidha, namshukuru sana kwa kuniongoza na kunitia moyo pale mawimbi yalipozidi kuwa makubwa. Maneno yake mazito kwangu kwamba aliniteua ili nipigwe mawe badala yake na badala ya Watanzania maskini na kuwa nimtegemee Mungu daima, yamekuwa ndiyo nguvu yangu katika kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, nampongeza Mheshimiwa Rais pamoja na wasaidizi wake wakuu, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Ruangwa kwa kazi kubwa wanayoendelea kuifanya ya kutuletea maendeleo Watanzania wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kuwapongeza Viongozi Wakuu wa Mihimili ya Dola, nikianza na wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mbunge wa Jimbo la Kongwa, lakini pia Mheshimiwa Dkt. Tulia Ackson Mbunge Naibu Spika. Nawapongeza kwa umahiri na busara zenu katika kuongoza Bunge hili. Vilevile, nawapongeza kwa dhati Mheshimiwa Profesa Ibrahim Juma, Kaimu Jaji Mkuu, kwa kuongoza vyema mhimili wa Mahakama katika kutoa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama, nikianza na Mkuu wa Majeshi, Jenerali Venance Mabeyo; Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro; Kamishna Jenerali wa Magereza, Dkt. Juma Ali Malewa; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji Dkt. Anna Makakala; Mkurugenzi wa Usalama wa Taifa, Dkt. Modestus Kipilimba; Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Kamishna wa Polisi, Valentino Mlowola; Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Madawa ya Kulevya Bwana Rogers William Siang'a; na Kamishna Jenerali wa Zimamoto na Uokoaji Bwana Thobias Andengenyeye; pamoja na Makamanda, Askari na Watumishi wote wa vyombo hivyo kwa uhodari wao katika kuilinda nchi yetu na kuhakikisha amani, usalama na uhuru wetu wa kisiasa na kiuchumi vinadumishwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kuwapongeza Wabunge wapya walioingia katika Bunge hili Mwaka huu wa Fedha ambao ni Mheshimiwa Juma Ali Juma, Mbunge wa Dimani (CCM); Mheshimiwa Mchungaji Dkt. Getrude Pangalile Rwakatare; Mbunge wa Viti Maalum (CCM); na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge, Mbunge wa Viti maalum (CHADEMA).

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge walioteuliwa na Rais, Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo (Mbunge); Mheshimiwa Anne Kilango Malecela, (Mbunge); Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mbunge); na Mheshimiwa Profesa Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mbunge); ambaye sasa ni Waziri wa Katiba na Sheria. Hongera sana kwenu nyote.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, niwapongeze Waheshimiwa Wabunge waliochaguliwa na Bunge hili kuiwakilisha nchi yetu ya Tanzania katika Bunge la Afrika Mashariki ambao ni, Mheshimiwa Fancy Nkuhi, Mheshimiwa Happiness Lugiko, Mheshimiwa Maryam Ussi Yahya, Mheshimiwa Dkt. Abdallah Makame, Mheshimiwa Dkt. Ngwaru Maghembe, Mheshimiwa Mhandisi Habibu Mnyaa,

Mheshimiwa Alhaji Adam Kimbisa, Mheshimiwa Pamela Massay na Mheshimiwa Josephine Lemoyani. Nawatakia kazi njema na kuwasisitiza wasiyumbe katika kusimamia maslahi ya kimkakati yaani *strategic interests* ya Taifa letu katika mijadala ya Bunge hilo la Afrika Mashariki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa pole kwa Watanzania waliopatwa na majanga mbalimbali na misiba, nikianza na Bunge ambalo liliwapoteza wenzetu, Mheshimiwa Hafidh Ali Tahir aliyekuwa Mbunge wa Dimani (CCM); na Mheshimiwa Dkt. Ely Marco Macha aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CHADEMA). Aidha, Bunge liliondokewa na Spika mstaafu, Mheshimiwa Samuel John Sitta, mzee wa kasi na viwango.

Mheshimiwa Spika, vilevile, natoa pole kwa wazazi na ndugu wa wanafunzi 32, Walimu wawili na dereva mmoja wa shule ya Lucky Vincent waliofariki kwa ajali ya gari tarehe 6 Mei, 2017 katika Wilaya ya Karatu. Vivyo hivyo, natoa pole kwa ndugu wa askari wetu nane na wananchi wengine ambao wameuawa na kundi la kihalifu katika Wilaya za Kibiti na Rufiji kwa nyakati tofauti katika mwaka huu. Mungu azilaze roho za marehemu wote hao mahala pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Spika, nawiwa kuishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti inayoongozwa na Mheshimiwa Hawa Abdulrahman Ghasia, Mbunge wa Mtwara Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kwa kupitia na kuchambua mapendekezo ya bajeti ninayowasilisha hivi sasa na kutoa maoni na ushauri uliochangia kuboresha Bajeti hii ya Serikali kwa mwaka 2017/2018. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, napenda kuwashukuru Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Kisekta na Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushauri na mapendekezo mliyotoa kwa Serikali wakati wa kuchambua Bajeti za kisekta. Namshukuru pia Mheshimiwa George Mcheche Masaju (Mbunge),

Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kutayarisha kwa wakati Muswada wa Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017 na Muswada wa Sheria ya Matumizi wa mwaka 2017. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kachwamba Kijaji, Mbunge wa Kondo, ambaye ni Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa ushirikiano na msaada anaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara yangu. Aidha, napenda kumshukuru Bwana Doto James, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango na Mlipaji Mkuu wa Serikali kwa usimamizi wa kazi za kila siku za Wizara na uratibu mzuri wa maandalizi ya bajeti hii, akisaidiwa na Naibu Makatibu Wakuu, Bibi Dorothy Mwanyika, Bibi Amina Khamis Shaaban na Dkt. Khatibu Kazungu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naendelea kumshukuru sana Profesa Benno Ndulu, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania kwa kuongoza kwa weledi taasisi hii nyeti yenye jukumu la kusimamia Sekta ya Fedha na kulinda utulivu na ukuaji wa uchumi wa Taifa. Aidha, napenda kutambua kazi nzuri ya viongozi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania katika kukusanya mapato ya Serikali wakiongozwa na Ndugu Charles Kichere, Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Dkt. Oswald Mashindano, Msajili wa Hazina na Dkt. Albina Chuwa, Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu. Vilevile, nawashukuru Kaimu Katibu Mtendaji wa Tume ya Mipango, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha, Wakuu wa Idara na Vitengo vya Wizara, pamoja na watumishi wote wa Wizara na Taasisi zake kwa kazi kubwa waliyoifanya katika kukamilisha bajeti hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, bajeti hii imezingatia mawazo na mapendekezo ya wadau mbalimbali wakiwemo jumuiya ya wafanyabiashara na washirika wa maendeleo. Nawashukuru wote kwa mawazo na ushauri. Kipekee nawashukuru Wajumbe wa kikosi kazi cha maboresho ya mfumo wa kodi ambayo inaundwa na wawakilishi wa sekta binafsi na

wataalam wa kodi kutoka vyyuo vikuu na taasisi za utafiti. Aidha, naishukuru Kamati ya Ushauri kwa Waziri wa Fedha kuhusu hatua za mapato yaani (*Advisory Committee on Revenue Measures*). Uchambuzi na ushauri wao umechangia kufikia hatua mpya za kodi nitakazopendekeza hivi punde.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii inawasilisha bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Serikali inaleta Bajeti hii kwa dhamira ya kuongeza kasi ya kutekeleza malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia Ilani ya Uchaguzi ya CCM, 2015 - 2020, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/2017 mpaka 2020/2021, Mpango wa Maendeleo wa Muda Mrefu na Malengo ya Maendeleo Endelevu, 2030.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba ya uzinduzi wa Bunge la 11 tarehe 20/11/2015, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwaeleza Watanzania kwamba, vipaumbele vya Serikali yake kuhusu uchumi ni kuendeleza na kuimarisha misingi imara ya uchumi wa nchi yetu iliyojengwa katika awamu za uongozi zilizotangulia. Vipaumbele hivyo ni vifuatavyo:

(i) Kuendeleza ukuaji wa uchumi na kujenga uchumi wa kipato cha kati ambapo sura na maisha ya Watanzania walio wengi yafananefanane na nchi ya kipato cha kati;

(ii) Kuongeza mapato, kuziba mianya ya upotevu wa fedha za Serikali, kupunguza matumizi yasiyo ya lazima, na kusimamia sheria za manunuzi ya umma;

(iii) Ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi (barabara, reli, usafiri wa anga na wa majini na pia umeme) ili kushawishi na kuvutia wawekezaji wa ndani na wa nje;

(iv) Kuhakikisha kwamba madini na maliasili zetu zinatumika kwa manufaa ya Taifa letu;

(v) Kuweka mkazo mkubwa na kusimamia uendelezaji wa viwanda kwa kutambua kwamba Sekta Binafsi ndiyo mhimili mkubwa wa kujenga uchumi wa viwanda. Aidha, aina ya viwanda tunavyotaka ni vile ambavyo vina sifa ya kuzalisha ajira nyingi, sehemu kubwa ya malighafi husika inatoka ndani na vile vya kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini;

(vi) Kuboresha kilimo cha mazao, mifugo na uvuvi na hasa kuongeza thamani na kuzifanya shughuli hizi kuwa za kisasa zaidi kwa kutoa mafunzo, pembejeo, zana na wataalam;

(vii) Kuweka mkazo katika kuendeleza utalii, ardhi na utunzaji wa mazingira;

(viii) Kuongeza ubora wa elimu, huduma za afya, maji na umeme;

(ix) Kupambana na tatizo kubwa la rushwa, uofisadi na madawa ya kulevya; na

(x) Kufanya mabadiliko makubwa ya kiutendaji Serikalini ili kupunguza urasimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, mapitio ya mwenendo wa uchumi wa Taifa na tathmini ya utekelezaji wa Bajeti ya Serikali katika Mwaka 2016/2017 yamelenga kutoa picha ya utekelezaji wa vipaumbele hivyo vya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Mheshimiwa Spika, katika hotuba niliyosoma leo asubuhi, nilieleza kwa kirefu hali ya uchumi wetu ilivyokuwa katika mwaka 2016 na miezi minne ya kwanza ya mwaka huu wa 2017. Inatosha nirejee kuwaambia Watanzania kwamba uchumi wa Taifa umeendelea kuimarika ambapo Tanzania ilikuwa miongoni mwa nchi tano za Afrika zilizoongoza kwa kuwa na kasi kubwa ya ukuaji wa uchumi. *(Makofi)*



Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa takwimu za uchumi za Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF World Economic Outlook Database*), nchi hizo tano ni Ivory Coast ambayo ilikua kwa asilimia 7.9, Tanzania asilimia 7.1, Senegal asilimia 6.6, Djibouti asilimia 6.5, na Ethiopia asilimia 6.5. Aidha, Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Fedha Duniani, Ndugu Tao Zhang alipotembelea Tanzania kwa mara ya kwanza mwezi Mei 2017, alitoa tathmini yake kwamba uchumi wa Tanzania umebaki kuwa imara kutokana na maboresho ya kisera yaliyotekelezwa chini ya uongozi thabiti wa Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na hasa katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani na vita dhidi ya rushwa na ufisadi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jarida la Benki ya Dunia (*Tanzania Economic Update*) lililochapishwa Aprili 2017 linabainisha waziwazi kuwa uchumi wa Taifa ni imara kwa kuangalia viashiria mbalimbali kama ukuaji wa uchumi, mfumuko wa bei, urari wa biashara, akiba ya fedha za kigeni na thamani ya shilingi na naomba kunukuu kwa Kkiingereza:

*" Tanzania's economic performance continues to rank among the highest in the region. The real GDP growth rate has consistently outpaced its EAC peers. The inflation rate remains relatively low. The current account deficit has significantly improved, with gross reserves sufficient to cover four months of imports. The shilling has also remained stable in 2016, following significant depreciation and volatility in 2015."*  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo, pamekuwa na maeneo ambayo yametawala mijadala kuhusu afya ya uchumi wa Taifa, ambayo napenda kuyaelezea kwa kifupi. Maeneo hayo ni pamoja na ukwasi katika uchumi, kufungwa kwa biashara na madai kwamba sekta binafsi imepoteza matumaini na kujiamini (*private sector confidence*) kutokana na baadhi ya hatua zilizochukuliwa na Serikali bila ushirikishwaji wa wadau.

Mheshimiwa Spika, Hali ya Ukwasi Katika Uchumi;

ukwasi ni kiasi cha fedha kilichopo katika uchumi kinachojumuisha fedha taslim zilizoko kwenye mzunguko nje ya mabanki na rasilimali fedha nyingine ambazo zinaweza kubadilishwa na kuwa fedha taslimu bila kikwazo. Utoshelevu wa ukwasi katika uchumi hupimwa kwa viashiria mbalimbali vikiwemo ujazi wa fedha, mwenendo wa mikopo kwa sekta binafsi, kiwango cha mitaji ya mabanki, uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslim na amana zinazoweza kuhitajika katika muda mfupi na upatikanaji wa huduma za kifedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichoishia mwezi Machi 2017, hali ya baadhi ya vigezo vya ukwasi inaonyesha kuwa ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (*M3*) na *M3* inajumuisha sarafu na noti zilizoko katika mzunguko nje ya mabanki, amana za muda mfupi, muda maalum na amana katika fedha za kigeni zilizopo katika mabanki, uliongezeka na kufikia shilingi trilioni 22.53 kutoka shilingi trilioni 21.65 katika kipindi kama hicho mwaka 2016, sawa na ongezeko la asilimia 4.1. Aidha, sekta ya kibanki iliendelea kuwa imara na himilivu, ikiwa na viwango vya mitaji na ukwasi ulio juu ya ukomo unaohitajika kisheria kama ifuatavyo:-

Kwa kutumia kigezo cha uwiano kati ya mali inayoweza kubadilishwa kuwa fedha taslim na amana zinazoweza kuhitajika kwa muda mfupi (*Liquid Assets to Demand Liabilities*), uwiano huu ulikuwa asilimia 35.9 mwezi Machi, 2017 ikilinganishwa na uwiano wa chini unaohitajika kisheria wa asilimia 20.

Mheshimiwa Spika, vilevile, uwiano wa mtaji wa msingi na rasilimali za benki ulikuwa asilimia 19.0 ambao uko juu ya kiwango cha chini kinachohitajika kisheria cha asilimia 10. Kadhalika, amana za wateja katika benki za biashara ziliongezeka kwa asilimia 0.3 kutoka shilingi trilioni 18.84 mwezi Machi, 2016 hadi shilingi trilioni 18.89 mwezi Machi, 2017.

Mheshimiwa Spika, takwimu pia zinaonesha kuwa ukwasi wa mabanki ulianza kutetereka kutokana na

kuongezeka kwa mikopo chechefu kutoka asilimia 8.3 mwezi Machi 2016 hadi asilimia 10.9 Machi 2017 ikilinganishwa na kiwango kinachohitajika cha asilimia tano. Mikopo kwa sekta binafsi iliongezeka kidogo kwa asilimia 3.7 katika kipindi cha mwaka ulioishia Machi, 2017 ikilinganishwa na ongezeko la asilimia 23.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2016. Kupungua kwa kiwango cha ukuaji huo kulitokana kwa kiasi kikubwa na kuyumba kwa biashara duniani ambako kuliathiri nchi nyingine duniani ikiwemo Tanzania. Napenda kuchukua nafasi hii kuyataka mabenzi yote nchini kusimamia sawasawa taratibu za kibenki katika utoaji wa mikopo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu imechukua hatua ikiwa ni pamoja na kupunguza riba ambazo benki za biashara hukopa kutoka Benki Kuu (*Discount Rate*) ili kuongeza ukwasi katika benki za biashara na hivyo kuziwezesha kukopa kwa gharama nafuu zaidi. Riba hiyo imepunguzwa kutoka asilimia 16.0 iliyokuwa ikitumika tangu mwezi Novemba, 2013 hadi asilimia 12.0 ambayo imeanza kutumika rasmi tarehe 6 Machi, 2017.

Mheshimiwa Spika, aidha, katika kuimarisha zaidi soko la fedha nchini, Benki Kuu ilipunguza kiwango cha amana ambacho benki za biashara zinatakiwa kuhifadhi Benki kuu kama dhamana (*Statutory Minimum Reserve Requirement*) kutoka asilimia 10.0 hadi asilimia 8.0 ili kuziwezesha benki za biashara kuwa na ukwasi zaidi kwa ajili ya kukopesha sekta binafsi. Hatua hii imeanza kutumika rasmi mwezi Aprili 2017. Ni matumaini ya Serikali kuwa hatua hizi zitaziwezesha benki za biashara nchini kuongeza ukwasi wa kutosha kuwakopesha wananchi kwa riba nafuu.

Mheshimiwa Spika, katika hatua nyingine, mwaka 2016/2017, benki tatu za biashara zilifungwa kutokana na sababu mbalimbali. Benki hizo ni Benki ya Twiga, *FBME Bank Limited*; na *Mbinga Community Bank*. Mnamo tarehe 28 Oktoba, 2016, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilichukua usimamizi wa benki ya Twiga baada ya kubaini kuwa benki

hiyo ilikuwa na upungufu mkubwa wa mtaji kinyume na matakwa ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na Kanuni zake.

Mheshimiwa Spika, upungufu huu wa mtaji ulionekana kuhatarisha usalama wa sekta ya fedha na pia kuendelea kutoa huduma za kibenki kwa benki ya Twiga kungehatarisha usalama wa amana za wateja wake. Hata hivyo, baada ya kukamilika kwa zoezi la kutathmini hali ya kifedha ya benki hiyo, Serikali iliruhusu baadhi ya huduma za benki hiyo ziendeleo huku ikiendelea na mchakato wa kupitia na kuchambua njia mbadala za kutatua tatizo la mtaji linaloikabili benki ya Twiga. Kwa sasa Serikali inapitia maombi yaliyoletwa na wawekezaji mbalimbali wanaotaka kununua hisa na kuongeza mtaji wa benki hiyo.

Mheshimiwa Spika, tarehe 8 Mei, 2017, Serikali ilisimamisha shughuli zote za *FBME Bank Limited*; kufuta leseni yake ya kufanya shughuli za kibenki, kuiweka chini ya ufilisi na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana kama mfilisi. Uamuzi huu ulifikiwa kutokana na mwelekeo wa benki hiyo kuwa mashakani kufuatia Mahakama ya Marekani kukubaliana na ombi la Taasisi ya Marekani ya Kupambana na Uhalifu wa Kifedha (*FinCEN*) la kuifungia *FBME* kutumia mfumo wa kibenki wa Marekani kutokana na tuhuma za kujihusisha na biashara ya utakatishaji wa fedha haramu.

Mheshimiwa Spika, naomba tena kupitia hotuba hii ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2017/2018 kuyaonya mabenki yote yatacakayobainika kujihushisha na biashara ya utakatishaji fedha haramu au kufadhili ugaidi au kwenda kinyume na sheria za nchi, Serikali itachukua hatua kali za kufuta leseni za kufanya shughuli za kibenki hapa nchini mara moja na hatua nyingine kwa mujibu wa Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake na hata Sheria za Kimataifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Benki Kuu ya Tanzania ilichukua hatua nyingine ya kuifunga Mbinga *Community Bank Plc*, kusitisha shughuli zake zote za kibenki

na kufuta leseni yake ya biashara ya kibenki kuanzia tarehe 12 Mei, 2017. Benki hiyo iliwekwa chini ya ufilisi na kuiteua Bodi ya Bima ya Amana kama mfilisi.

Mheshimiwa Spika, uamuzi huu ulichukuliwa baada ya Serikali kujiridhisha kuwa Mbinga *Community Bank Plc* ina upungufu mkubwa wa mtaji na ukwasi kinyume na matakwa ya Sheria ya Mabenki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na kanuni zake. Upungufu huu wa mtaji na ukwasi ungeweza kuhatarisha usalama wa sekta ya fedha na wa amana za wateja. Serikali inapenda kuuhakikishia umma wa Watanzania kuwa itaendelea kulinda maslahi ya wenye amana katika mabenki yaliyopo nchini kwa lengo la kulinda utulivu katika sekta za fedha.

Mheshimiwa Spika, wigo wa utoaji huduma za kifedha kwa wananchi walio wengi zaidi na kwa gharama nafuu umepanuka sana kutokana na mtandao mkubwa wa mabenki na taasisi nyingine za fedha zipatazo 64; benki za biashara 40, benki za maendeleo tatu (3), benki za jumuiya 11, huduma ndogo za kifedha – (*micro finance*) tano (5), taasisi zinazotoa mikopo binafsi (*private credit*) mbili (2) na kampuni za huduma za kifedha za kukodisha (*lease finance*) tatu (3).

Mheshimiwa Spika, sambamba na hizi, kuna huduma za kifedha na malipo kupitia huduma za benki zinazohamishika (*mobile banking*), mawakala na simu za mkononi. Hivi sasa, inakadiriwa kuwa Watanzania zaidi ya milioni 17 wanafanya miamala kwenye mfumo wa malipo kupitia simu za mkononi.

Mheshimiwa Spika, kufungwa kwa biashara; suala hili lilikuwa likizungumzwa sana na wananchi na pia hapa Bungeni ni kuhusu kuongezeka kwa kasi ya kufunga biashara hususan, eneo la Kariakoo katika Jiji la Dar es Salaam na katika miji mingine. Kwa mujibu wa taarifa zilizofikishwa TRA, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2016 hadi Machi, 2017, jumla ya biashara 7,277 zilifungwa katika mikoa mbalimbali nchini.

Mheshimiwa Spika, mwenendo huu kwa ujumla siyo mzuri kwa sababu wananchi wanapoteza ajira na kipato, Serikali inakosa mapato ya kodi na uchumi unadorora. Hivyo, ni muhimu pale wimbi la kufungwa kwa biashara linapotokea jitihada zifanyike kuelewa aina gani za biashara zinafungwa, kwa nini zinafungwa na hatua gani zichukuliwe kudhibiti hali hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ziko sababu mbalimbali zinazoweza kuwa zimepelekea hali hiyo, ikiwa ni pamoja na ushindani mkali wa kibiashara, usimamizi dhaifu wa biashara, kuongezeka kwa gharama za kufanya biashara kama vile usafirishaji, kodi na tozo mbalimbali na kutozingatia masharti ya kufanya biashara. *(Makoffi)*

Mheshimiwa Spika, pia, imedhihirika kwamba, wafanyabiashara wengi wameanza mazoea ya kutoa taarifa kwa Mamlaka ya Mapato mara wanapofunga biashara zao. Hii ilitokana na elimu iliyotolewa na mamlaka kuhusu umuhimu wa kutoa taarifa ambazo zimewafanya walipa kodi kufahamu kuwa unapofunga biashara bila kutoa taarifa, kodi inajilimbikiza na wataendelea kudaiwa na Mamlaka ya Mapato.

Mheshimiwa Spika, ni vema kutambua kwamba kufunguliwa au kufungwa kwa biashara ni jambo la kawaida kabisa katika uendeshaji wa biashara. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, katika kipindi hicho hicho cha Julai, 2016 mpaka Machi, 2017, Mamlaka ya Mapato ilisajili biashara mpya zipatazo 224,738. Narudia tena, katika kipindi hicho hicho cha Julai, 2016 mpaka Machi, 2017, Mamlaka ya Mapato ilisajili biashara mpya zipatazo 224,738. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivyo, ni muhimu sana picha inayotolewa isiwe ya upande mmoja peke yake. Ni vema pia kujua kwamba kufungwa kwa biashara sio kwa Tanzania peke yake ni jambo ambalo linatokea katika vipindi mbalimbali katika historia za Mataifa na kwa viwango tofauti tofauti. Watu wengi miongoni mwetu tumesoma kuhusu anguko kuu la biashara lililotokea katika bara la Ulaya

na Amerika kati ya mwaka 1929-1939 likijulikana kama " *the Great Depression*". China nako katika miaka 1980 biashara nyingi zilipigwa na dhoruba ambapo baadhi zilizama lakini nyingine ziliendelea kukua. Haya yameelezwa vizuri sana katika kitabu cha Tian Tao na wenzake kinachoitwa *Huawei Leadership, Culture and Connectivity* kilichochapishwa mwaka 2017. Naomba kunukuu kwa lugha ya Kiingereza kutoka ukurasa wa 43 wa Kirumi wa kitabu hicho:

*"From the 1980s onward, China was swept up in the largest wave of commercial development in human history. Businesses at the time were like ships, each raised up and carried along by the sheer momentum of the wave. Some, however, soon capsized and were swallowed up, while most drifted along, going with the flow. Others crashed against barriers in the sea or got stranded on deserted islands. Only a few rose atop the crest of the wave and survived, eventually sailed towards new lands."* Mwisho wa kunukuu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda, Biashara na Uwekezaji kwa kushirikiana na Wizara yangu inaendelea kufuatilia kwa karibu mwenendo wa biashara nchini na itachukua hatua stahiki itakapobidi kufanya hivyo. Wito wa Serikali kwa wafanyabiashara nchini ni kwamba fanyeni biashara zenu bila hofu kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu za nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, yamekuwepo madai ya kuwa wafanyabiashara wamepoteza kujiamini kutokana na matamshi ya baadhi ya Viongozi na hatua zilizochukuliwa na Serikali bila kuwashirikisha wafanyabiashara ambazo zimezua hofu. Napenda niwahakikishie wafanyabiashara kuwa, Serikali ya Awamu ya Tano inaamini kwa dhati kuwa sekta binafsi ndiyo injini ya uchumi na inathamini sana na kupongeza mchango mkubwa sana wa wafanyabiashara katika uchumi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, ni ukweli ulio dhahiri kwamba, sehemu kubwa ya uzalishaji wa bidhaa na huduma mbalimbali kwa ajili ya matumizi nchini na mauzo nje

ambayo ndio yanayotupatia fedha za kigeni unafanywa na sekta binafsi, kwa hiyo ni lazima tuwapongeze. Pia sekta binafsi ndiyo Mwajiri Mkuu na chanzo kikuu cha mapato ya Serikali. Hivyo, sekta binafsi ndiyo mbia mkuu wa Serikali katika kazi ya kuharakisha maendeleo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu mkubwa wa sekta binafsi na wafanyabiashara, Serikali imekuwa ikifanya jitihada za kujenga mazingira mazuri ya kufanya biashara. Katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, Serikali iliendelea na jitihada za kuimarisha utulivu wa uchumi jumla, kupunguza urasimu, kuharakisha maamuzi, kuimarisha ulinzi na usalama na kuhakikisha upatikanaji wa miundombinu imara na huduma bora zikiwemo za umeme wa uhakika na mikopo kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, hayo yote ni maeneo ambayo Serikali inayapa kipaumbele na itaendelea kuyapa kipaumbele na itaendelea kufanya hivyo. Aidha, Serikali bado ina dhamira ya dhati kuendeleza mashauriano na wafanyabiashara kupitia utaratibu wa mikutano ya Baraza la Taifa la Biashara, Taasisi za Sekta Binafsi na makongamano mengine.

Mheshimiwa Spika, tumeanza kuona viashiria bora zaidi katika eneo hili la kuboresha mazingira ya biashara. Taarifa ya Benki ya Dunia ya mwaka 2017 imeonesha kuwa, Tanzania ilikuwa nchi ya 132 kwa urahisi wa kufanya biashara ikiwa imepiga hatua kwa nafasi 12 kutoka nafasi ya 144 mwaka 2016. Aidha, kwa mujibu wa taarifa ya Fahirisi ya Uwekezaji Afrika ya mwaka 2016 (*Africa Investment Index, 2016*) iliyotolewa na taasisi inayoitwa “*Quantum Global Research Lab*” ya Uingereza, Tanzania ilikuwa nchi ya kwanza miongoni mwa nchi za Afrika Mashariki kwa kuvutia uwekezaji na ya nane kwa Afrika, ikiwa imepiga hatua kutoka nafasi ya 19 mwaka 2015. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuzungumza na wafanyabiashara ili kupata maoni na ushauri wao kuhusu



sera mbalimbali na mwenendo wa uchumi kwa ujumla na kutatua kero zao. Nia ya Serikali ni kuhakikisha wanafanya biashara katika mazingira mazuri yanayotabirika ili biashara hizo zikue na kushamiri, ajira ziongezeke na Serikali ipate kodi stahiki kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo na huduma za jamii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania itaendelea kuboresha mfumo wa kodi na kuweka mazingira rafiki kwa wafanyabiashara na kuwawezesha kufanya biashara zao kwa urahisi. Aidha, Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali, itaendelea na jitihada za kuelimisha umma juu ya umuhimu wa kurasimisha shughuli zao za kiuchumi. Pamoja na kutoa elimu, napenda kusisitiza kuwa, kulipa kodi ni wajibu wa msingi wa kila raia kwa maendeleo ya Taifa, lazima Watanzania tulipe kodi. Serikali hii haitavumilia uporaji wa rasilimali za nchi na ukwepaji kodi kwa kivuli cha kulinda imani ya wafanyabiashara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda nitumie pia fursa hii niwakumbushe watumishi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwamba, kodi zinatozwa kwa kuongozwa na sheria na kanuni zake, matumizi ya vitisho na unyanyasaji kwa walipa kodi...

Naomba nirudie, kodi zinatozwa kwa kuongozwa na sheria na kanuni zake, matumizi ya vitisho na unyanyasaji kwa walipa kodi, kuwadai rushwa au kuwazidishia makadirio ya kodi ili kuwakomoa, hayo ni mambo ya hovyoy na hayakubaliki hata kidogo. Wale watumishi wa Mamlaka ya Mapato ambao naamini ni wachache tu wanaojihusisha na vitendo hivyo, wakome kabisa kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Watumishi wa Mamlaka ya Mapato na vyombo vingine vyote vya Serikali vinavyokusanya mapato, wale tutakaowabaini kwamba wanafanya mambo ya hovyoy tutawachukulia hatua kali kwa mujibu wa Sheria za Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, aidha, natoa rai kwa wafanyabiashara wetu na wananchi wazalendo kutupatia taarifa za ukweli kuhusu mwenendo mbaya wa mtumishi yeyote wa Mamlaka ya Mapato ili zifanyiwe kazi na Serikali. Nawaomba pia mfanye hivyo hivyo kwa kutupatia taarifa kuhusu wafanyabiashara wanaokwepa kodi ili tuwashughulikie ipasavyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nieleze thathmini ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2016/2017. Katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017, mapato kutoka vyanzo vyote yalifikia shilingi trilioni 20.7, sawa na asilimia 70.1 ya lengo la mwaka la shilingi bilioni 29.5. Mchanganuo wa mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

(i) Mapato ya kodi yalifikia shilingi trilioni 11.6 sawa na asilimia 77.1 ya lengo la mwaka la kukusanya shilingi trilioni 15.1;

(ii) Mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi trilioni 1.6 sawa na asilimia 59.8 ya lengo la mwaka la shilingi trilioni 2.6;

(iii) Mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalikuwa shilingi bilioni 399.3 sawa na asilimia 60.0 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 665.4 kwa mwaka;

(iv) Mikopo kutoka vyanzo vya ndani ilifikia Shilingi bilioni 4,715.6, sawa na asilimia 87.7 ya shilingi bilioni 5,374.3 zilizotarajiwa kukopwa kwa mwaka kutoka katika chanzo hiki; na

(v) Misaada na mikopo yenye masharti nafuu kutoka nje iliyopokelewa hadi Aprili, 2017 ni shilingi bilioni 2,340.1, sawa na asilimia 65.0 ya lengo la shilingi bilioni 3,600.8 zilizoahidiwa na Washirika wa Maendeleo kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, katika bajeti ya mwaka 2016/2017, Serikali ilipanga kukopa kiasi cha shilingi bilioni 2,100.9 kutoka

kwenye vyanzo vya kibiashara ili kugharamia miradi mbalimbali ya maendeleo, lakini haikuweza kukopa kutokana na hali ya soko la fedha la Kimataifa kutokuwa zuri. Hata hivyo, Serikali inakamilisha majadiliano na wakopeshaji ambapo kiasi cha dola za Marekani milioni 500 kinatarajiwa kupatikana kabla ya mwisho wa mwezi wa Juni, 2017.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kudhibiti upotevu wa mapato katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kudhibiti upotevu wa mapato. Katika kutekeleza azma hii, baadhi ya taasisi zimeanza kutumia mifumo ya kielektroniki katika kukusanya mapato. Katika Halmashauri zinatumia Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali za Mitaa (*Local Government Revenue Collection System*) na Jeshi la Polisi katika Mkoa wa Dar es Salaam linatumia Mfumo wa Udhibiti wa Vyombo vya Moto Barabarani (*Traffic Management System*).

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali imekamilisha mfumo wa kielektroniki (*Government e-Payment Gateway System*) utakaotumika katika ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Mfumo utaisaidia Serikali kuwa na uhakika wa mapato yanayokusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali kwa wakati na kurahisisha ulipaji wa kodi, tozo na ada mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, aidha, tarehe 01 Juni, 2017 Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alizindua mfumo mpya wa ukusanyaji mapato kwa njia za kielektroniki. Mfumo huo unalenga kupata taarifa sahihi za mlipa kodi na mtoa huduma hususan makampuni ya simu, mabenki na televisheni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Ukusanyaji wa Kodi ya Majengo; Sheria ya Fedha ya Mwaka 2016 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu inaipa Mamlaka ya Mapato Tanzania jukumu la kukusanya kodi ya majengo kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa zote nchini kuanzia mwaka 2016/2017. *TRA* ilipewa

jukumu hili kutokana na kuwa na ufanisi katika ukusanyaji na mtandao mpana ulioenea nchi nzima. Uamuzi huu haukuwa na maana ya kupora chanzo hiki cha mapato kutoka katika Halmashauri, bali kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa kodi kutoka katika chanzo hiki.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitishwa kwa Sheria hiyo ya Fedha, hatua iliyofuata ilikuwa ni kutolewa kwa Tangazo la Serikali No. 276 la tarehe 30 Septemba, 2016 lililoitaka *TRA* kuanza zoezi hilo kwa Halmashauri 30 za awali. Jukumu la kukusanya kodi ya majengo katika Halmashauri zilizobaki, liliendelea kubaki katika Halmashauri husika.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hicho, Serikali kupitia *TRA* ilifanya maandalizi ya utaratibu na mifumo ya ukusanyaji. Maandalizi hayo yalikusisha kutengeneza kanuni za ukusanyaji, kutengeneza mfumo wa ukusanyaji wa kodi hii, kuunda kitengo, kuweka wafanyakazi na vitendea kazi kabla ya kuanza ukusanyaji.

Mheshimiwa Spika, baada ya kukamilika kwa taratibu hizo, *TRA* ilianza rasmi kukusanya Kodi ya Majengo tarehe 1 Oktoba, 2016 katika Majiji, Manispaa na Miji 30. Hadi Mei, 2017, *TRA* imekusanya jumla ya Shilingi milioni 15,134.2. Ni matumaini ya Serikali kwamba kwa mwaka 2017/2018, *TRA* itafanya vizuri zaidi katika ukusanyaji wa kodi hii ya majengo. Maboresho ya kukusanya kodi hiyo nitayaeleza baadaye.

Mheshimiwa Spika, natoa rai kwa wadau wote wakiwemo wamiliki wa majengo, viongozi wa Halmashauri, Wakuu wa Wilaya na Mamlaka ya Mapato Tanzania kushirikiana bega kwa bega kuhakikisha wanafanikisha zoezi hili la ukusanyaji wa kodi ya majengo kwa maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi, katika kipindi cha Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 jumla ya shilingi bilioni 20,036.5 zilitolewa kwa Wizara, Idara Zinzajitegemea, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 15,480.9 zilizotolewa kwa ajili ya

matumizi ya kawaida sawa na asilimia 87.4 ya lengo la mwaka na shilingi bilioni 4,555.5 zilitolewa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo sawa na asilimia 38.5 ya lengo la shilingi bilioni 11,820.5 zilizotengwa kwa ajili ya bajeti ya maendeleo kwa mwaka. Fedha za maendeleo zilizotolewa zinajumuisha fedha za ndani, shilingi bilioni 3,647.7 na fedha za nje shilingi bilioni 907.8.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, baadhi ya fedha za nje za kugharamia miradi ya maendeleo hazikujumuishwa kwenye matumizi kutokana na sababu mbalimbali zikiwemo: kuchelewa kupata thamani halisi ya vifaa vilivyopelekwa moja kwa moja kwenye miradi kutokana na baadhi ya Washirika wa Maendeleo kuendelea kupeleka fedha moja kwa moja kwenye miradi bila kupitia mfumo wa malipo wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mahitaji yaliyopewa kipaumbele katika utoaji wa fedha za matumizi ya maendeleo kati ya Julai, 2016 hadi Aprili, 2017 ni pamoja na:-

(i) Ujenzi na ukarabati wa barabara kuu za Mikoa na Halmashauri. Zilizotoka kwenye Mfuko wa Barabara ni shilingi bilioni 675.9;

(ii) Miradi ya ujenzi wa barabara ikiwemo ulipaji wa madeni ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri shilingi bilioni 540.3; (*Makofi*)

(iii) Miradi ya uzalishaji wa umeme, uboreshaji wa njia za kupitisha umeme na usambazaji wa umeme vijijini shilingi bilioni 421.5; (*Makofi*)

(iv) Mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu, shilingi bilioni 393.2; (*Makofi*)

(v) Malipo ya awali ya ujenzi wa reli kwa kiwango cha *standard gauge*, awamu ya kwanza katika eneo la Dar – Morogoro (Kilomita 205) shilingi bilioni 300; (*Makofi*)

(vi) Ununuzi wa ndege mbili na malipo ya awali ya ununuzi wa ndege nne, shilingi bilioni 234.9; *(Makofi)*

(vii) Usambazaji wa maji mijini na vijijini shilingi bilioni 186.4; na *(Makofi)*

(viii) Uboreshaji wa huduma za afya katika ngazi zote shilingi bilioni 170.6 ikiwemo ununuzi wa dawa na vifaa tiba shilingi bilioni 156.1. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utoaji wa fedha za matumizi ya kawaida unajumuisha shilingi bilioni 5,320.3, sawa na asilimia 80.6 ya lengo la mwaka kwa ajili ya kugharamia mishahara; shilingi bilioni 7,775.5, sawa na asilimia 97.2 ya lengo la mwaka kwa ajili ya kulipia Deni la Taifa na shilingi bilioni 2,385.1, sawa na asilimia 76.5 ya lengo la mwaka kwa ajili ya kugharamia matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopewa kipaumbele katika utoaji wa fedha za matumizi mengineyo ni pamoja na yafuatayo:-

(i) Kugharamia shughuli za vyombo vya ulinzi na usalama, shilingi bilioni 591.3; *(Makofi)*

(ii) Elimu msingi bila malipo shilingi bilioni 203.0; *(Makofi)*

(iii) Uendeshaji wa mitihani ya kitaifa shilingi bilioni 69.9; *(Makofi)*

(iv) Mfuko wa Bunge shilingi bilioni 69.1; *(Makofi)*

(v) Kugharamia balozi zetu nje ya nchi shilingi bilioni 68.7; *(Makofi)*

(vi) Posho ya madaktari wanafunzi shilingi bilioni 15.3; *(Makofi)*

(vii) Ruzuku ya pembejeo shilingi bilioni 15.0;  
(Makofi)

(viii) Ruzuku ya vyama vya siasa shilingi bilioni 14.2;  
na

(ix) Ununuzi wa chakula cha hifadhi ya Taifa shilingi  
bilioni 13.0. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kudhibiti matumizi kwa mwaka 2016/2017, Sera za Matumizi ya Serikali zililenga kusimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za Umma kwa kuzingatia Sheria ya Bajeti Na. 11 ya mwaka 2015; Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma Sura 348; Sheria ya Fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Sura 290; Sheria ya Ununuzi wa Umma ya mwaka 2013, Sura 410; na Kanuni zake husika, pamoja na miongozo mbalimbali ya Serikali. Lengo kuu lilikuwa ni kupunguza matumizi yasiyo na tija, kuziba mianya ya ufujaji wa fedha za Umma na kuelekeza kiasi kikubwa cha fedha kwenye maeneo ya kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2016/2017, Serikali imeendelea kudhibiti matumizi katika maeneo mbalimbali ikiwemo: kupunguza safari za nje kwa kuhakikisha kuwa vibali vinatolewa kwa safari zenye manufaa kwa Taifa; kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji kwa kufanya ukaguzi wa mara kwa mara; na kuendelea kudhibiti gharama za uendeshaji wa magari ikiwa ni pamoja na matengenezo, mafuta na vilainishi. Aidha, utaratibu wa kufanya mikutano na makongamano katika kumbi za Serikali na taasisi za Umma umeongeza udhibiti wa matumizi ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa malimbikizo, uhakiki na ulipaji wa madai; hadi kufikia mwezi Juni, 2016 madai yaliyokuwa yamewasilishwa na taasisi mbalimbali yalikuwa jumla ya shilingi bilioni 2,934.4 ambapo jumla ya shilingi bilioni 1,997.9 sawa na asilimia 68.1 zilizithibitika kuwa madai halali baada ya uhakiki. Kati ya madai yaliyohakikiwa, Serikali imelipa jumla ya shilingi bilioni 796.5 hadi mwezi Machi, 2017 na hivyo kubakia na madai ya shilingi bilioni 1,201.4.

Mheshimiwa Spika, kati ya madai hayo yaliyolipwa, shilingi bilioni 632.1 ni kwa ajili ya Wakandarasi na Wahandisi Washauri; shilingi bilioni 78.9 kwa ajili ya Wazabuni wa huduma na bidhaa ikiwemo shilingi bilioni 11.2 za Bohari Kuu ya Madawa (*MSD*); shilingi bilioni 67.6 kwa ajili ya malimbikizo ya madai ya watumishi; na shilingi bilioni 17.9 ni kwa ajili ya watoa huduma mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kati ya Julai hadi Desemba, 2016, malimbikizo ya madai mapya kutoka kwenye taasisi mbalimbali yalikuwa ya jumla ya shilingi bilioni 899.5. Hivyo, hadi Desemba, 2016, madai yote yalifikia shilingi bilioni 2,100.9. Madai hayo yamegawanyika kama ifuatavyo:-

- (i) Shilingi bilioni 910.30 Wakandarasi;
- ii) Shilingi bilioni 890.16 ni Wazabuni wa huduma na bidhaa;
- (iii) Shilingi bilioni 159.10 ni madai ya watumishi mbalimbali;
- (iv) Shilingi bilioni 75.45 ni ankara za maji, umeme na simu; na
- (v) Shilingi bilioni 65.89 ni pango la ofisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, kati ya madai ya Wazabuni wa huduma na bidhaa, lipo deni la *MSD* ambalo ni shilingi bilioni 145.89 linalotokana na malimbikizo ya ununuzi wa dawa na vifaa tiba vilivyochukuliwa na taasisi mbalimbali za Serikali na havikuwa vimelipiwa.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa deni la Taifa; Serikali imeendelea kusimamia Deni la Taifa kwa kuzingatia Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada Sura 134. Ili kuhakikisha kuwa deni la Taifa linaendelea kusimamiwa ipasavyo, Bunge lako Tukufu lilipitisha marekebisho ya sheria hiyo mwezi Novemba, 2016. Baadhi ya maeneo yaliyorekebishwa ni pamoja na kuongeza masharti kwa Taasisi



na Mashirika ya Umma yanayoomba dhamana ya Serikali ili kudhibiti utoaji wa dhamana hizo; kuweka utaratibu maalum wa kisheria ambao unahakikisha kwamba fedha zilizokopwa na Serikali ya Muungano kwa lengo la kugharamia miradi ya maendeleo Zanzibar inafika kama ilivyokusudiwa; na kuongeza Wajumbe kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika Kamati ya Kitaifa ya Kusimamia Deni la Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hadi Machi, 2017, deni la Taifa lilifikia shilingi bilioni 50,806.5. Kati ya kiasi hicho, deni la Serikali ni shilingi bilioni 42,883.6 na deni la sekta binafsi ni shilingi bilioni 7,922.9. Deni la Serikali limeongezeka kwa asilimia 9.2 kutoka shilingi bilioni 39,274.6 Machi, 2016 hadi shilingi bilioni 42,883.6 Machi, 2017.

Mheshimiwa Spika, ongezeko la deni la Serikali linatokana na mikopo mipya na ya zamani iliyopokelewa katika kipindi cha mwaka 2016/2017 kutoka vyanzo vya masharti nafuu na ya kibiashara, malimbikizo ya riba ya deni la nje kwenye nchi zisizo wanachama wa kundi la Paris ambazo zinatakiwa kutoa msamaha wa madeni lakini bado hazijatoa pamoja na kushuka kwa thamani ya shilingi dhidi ya dola za Marekani.

Mheshimiwa Spika, deni la Serikali linajumuisha deni la ndani la shilingi bilioni 12,073.7 sawa na asimilia 28.1 na deni la nje la shilingi bilioni 30,809.9 sawa na asilimia 71.9. Deni la nje linajumuisha mikopo ya masharti nafuu kutoka kwenye mashirika ya fedha ya Kimataifa, sawa na asilimia 56.8, mikopo kutoka nchi wahisani ilifikia asilimia 16.3 na mikopo kutoka mabenki ya kibiashara ya Kimataifa ilifikia asilimia 26.9 ya deni lote la nje. Mikopo hiyo ilitumika kugharamia miradi ya maendeleo hususan katika Sekta za Ujenzi, yaani barabara na reli, nishati, uchukuzi, elimu na maji.

Mheshimiwa Spika, tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa. Matokeo ya tathmini ya uhimilivu wa deni iliyofanyika mwezi Novemba, 2016 yalibainisha kuwa Deni la Taifa ni himilivu kwa muda mfupi, wa kati na mrefu. Katika tathmini hiyo, viashiria vinaonesha kwamba thamani ya sasa ya jumla

ya Deni la Taifa (*Present Value of Total Public Debt*) kwa pato la Taifa ni asilimia 34.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 56; thamani ya sasa ya deni la nje (*Present Value of External Debt*) kwa pato la Taifa ni asilimia 19.9 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 97.7 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 150; na thamani ya sasa ya deni la nje kwa mapato ya ndani ni asilimia 145.3 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 250. Viashiria hivyo vinapima uwezo wa nchi kukopa bila kuathiri uhimilivu wa deni (*solvency indicators*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kutokana na tathmini ya uhimilivu wa deni la Taifa, ambayo inapima uwezo wa nchi kulipa deni, uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani umefikia asilimia 11.5 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20 na uwiano wa ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mauzo ya bidhaa nje ni asilimia 7.8 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 20. Kwa kuzingatia viashiria hivyo ambavyo vipo chini ya ukomo unaokubalika Kimataifa, Tanzania bado ina uwezo wa kuendelea kukopa kutoka ndani na nje ya nchi ili kugharamia shughuli zake za maendeleo na pia ina uwezo wa kulipa mikopo inayoiva kwa kutumia mapato yake ya ndani na nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sera za bajeti kwa maka 2017/2018; kwa mujibu wa makubaliano ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, dhima ya Bajeti ya mwaka wa 2017/2018 ni kujenga uchumi wa viwanda utakaochochea ajira na ustawi endelevu wa jamii. Hii inaendana kabisa na msisitizo na vipaumbele vya Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ya kujenga Tanzania ya viwanda. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, shabaha za uchumi jumla; utekelezaji wa bajeti ya mwaka ujao unalenga kufikia shabaha za uchumi jumla kama ifuatavyo:-

(i) Pato la Taifa kukua kwa asilimia 7.1 mwaka 2017 kutoka 7% mwaka 2016;

(ii) Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei katika wigo wa tarakimu moja kati ya 5% na 8% mwaka 2017;

(iii) Mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yafike asilimia 15.8 ya pato la Taifa na kuendelea kuongezeka hadi asilimia 16.5 ya pato la Taifa mwaka wa 2017/2018;

(iv) Mapato ya kodi yanakadiriwa kuongezeka kufikia asilimia 14.2 ya pato la Taifa mwaka ujao wa fedha kutoka matarajio ya asilimia 13.3 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017;

(v) Matumizi ya Serikali yanatarajiwa kuongezeka kufikia asilimia 26.2 ya pato la Taifa mwaka 2017/2018 kutoka matarajio ya asilimia 23.7 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017;

(vi) Nakisi ya bajeti inatarajiwa kupungua kufikia 3.8% ya pato la Taifa kutoka asilimia 4.5 ya pato la Taifa mwaka 2016/2017;

(vii) Nakisi katika urari wa malipo ya kawaida inatarajiwa kuwa 7% ya pato la Taifa mwaka 2017/2018; na

(viii) Kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayotosheleza mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne.

Mheshimiwa Spika, Serikali imedhamiria kuongeza na kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kutekeleza sera zifuatazo:-

(i) Kuendelea kusimamia kikamilifu matumizi ya vifaa na mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato ili kuongeza ufanisi na kudhibiti upotevu wa mapato;

(ii) Kuendelea kupanua wigo wa walipa kodi ikiwa ni pamoja na kurasimisha sekta isiyo rasmi ili iweze kuingia katika mfumo wa kodi;

(iii) Kuimarisha ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi na kuboresha usimamizi wake;

(iv) Kuendelea kufanya uthamini wa majengo na kusimamia ulipaji ili kuongeza mapato yatokanayo na kodi ya majengo;

(v) Kurasimisha miliki ya ardhi kwa lengo la kuongeza mapato; na

(vi) Kuendelea kudhibiti na kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaendelea kupanua Soko la Fedha la ndani ili kuwa na washiriki wengi kutoka ndani na nje ya nchi kwenye soko watakaowezesha Serikali kupata fedha za kuziba nakisi kwenye bajeti kwa riba nafuu. Serikali itahakikisha kuwa mchakato wa upatikanaji wa fedha za mikopo yenye masharti ya kibiashara unaharakishwa kwa kuzingatia maslahi ya Taifa na kuhakikisha fedha zitakazopatikana zinaelekezwa kwenye miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za Serikali kutaka kuimarisha ushirikiano kati yake na Washirika wa Maendeleo na kuhakikisha fedha zinazoahidiwa zinatolewa kwa wakati, Serikali na Washirika wa Maendeleo walitafuta Washauri Elekezi Huru. Timu hiyo inaongozwa na Dkt. Donald Kaberuka, aliyekuwa Rais wa Benki ya Maendeleo ya Afrika. Washauri Elekezi walipewa kazi ya kutathmini na kutoa mapendekezo ya kuimarisha ushirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo na muundo wa utoaji fedha.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya mapendekezo ya Washauri Elekezi katika kuimarisha ushirikiano yanajumuisha yafuatayo:-

Kwanza, ni kuanzisha majadiliano thabiti. Majadiliano yanalenga kufanya mapitio na kuimarisha Mchakato wa Mapitio ya Matumizi ya Umma (*Public Expenditure Review*),

kupata matokeo kwenye ngazi ya kisekta pamoja na namna ya kushughulikia masuala nyeti pasipo kuathiri mchakato wa Bajeti. *(Makofi)*

Pili, ni kujenga uwezo wa kitaasisi. Lengo ni kujenga ujuzi wa kiwango cha juu kwenye maeneo mbalimbali, ikiwemo namna ya kufanya majadiliano ya kuvuna malliasili, masuala ya usimamizi wa fedha, sera za biashara, usimamizi wa deni la nje na utafiti na uchambuzi wa sera.

Tatu, ni kugharamia azma ya serikali kuleta maendeleo. Hii itahusisha kutafuta fedha kupitia ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma. Misaada na Mikopo ya Kibajeti *(GBS)* bado inaweza kutumiwa katika maeneo mahsusni kama vile kulipia madeni ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeanza kufanyia kazi mapendekezo ya Washauri Elekezi kwa kukamilisha Mwongozo wa Ushirikiano kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Mwongozo huu unaainisha masuala mbalimbali ikiwemo: Misingi ya ushirikiano, muundo wa majadiliano na mifumo ya misaada inayoendana na mahitaji ya nchi. Ni matarajio ya Serikali kwamba hatua hii itasaidia kuimarisha ushirikiano na hivyo kuwawezesha Washirika wa Maendeleo kutimiza ahadi zao kwa kutoa fedha kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2017/2018, Serikali itaendelea kuhakikisha kuwa fedha zinaelekezwa kwenye maeneo ya vipaumbele ili kutekeleza kikamilifu Mpango wa Maendeleo wa Mwaka. Nidhamu ya hali ya juu katika matumizi lazima isimamiwe kwa nguvu zote ili kuhakikisha thamani ya fedha inapatikana. Ili kufikia azma hiyo, Serikali itafanya yafuatayo:-

(i) Kuendelea kuhakikisha kuwa Mashirika ya Umma yaliyoundwa kwa lengo la kujiendesha kibiashara, yanajiendesha kwa faida bila kutegemea ruzuku ya Serikali; *(Makofi)*

(ii) Kuhakikisha mikataba inayoingiwa na Serikali na Taasisi zake inakuwa katika Shilingi za Kitanzania isipokuwa kwa mikataba inayohusisha biashara na huduma za Kimataifa; (*Makofi*)

(iii) Kuendelea kudhibiti matumizi ya umeme, simu na maji ikiwa ni pamoja na kutumia teknolojia zinazopunguza gharama katika matumizi hayo;

(iv) Kuendelea kudhibiti ulipaji wa mishahara kwa kulipa watumishi wanaostahili; na

(v) Kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEHAMA*) katika kufanikisha mawasiliano katika shughuli za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kudhibiti ulimbikizaji wa madeni, Serikali itachukua hatua zifuatazo:-

(i) Kutofanya matumizi pasipokuwa na kasma iliyoidhinishwa kwenye bajeti ya Fungu husika; (*Makofi*)

(ii) Kuhakikisha kuwa uagizwaji wa bidhaa unafanyika baada ya kutolewa kwa hati ya ununuzi (*LPO*) kwenye mfumo rasmi wa malipo (*Intergrated Financial Management System*); (*Makofi*)

(iii) Kuhakikisha kuwa ahadi (*commitment*) inafanyika baada ya kupatikana kwa fedha na kutoingia mikataba bila kuwa na ridhaa ya matumizi; na (*Makofi*)

(iv) Kuhakikisha kuwa makubaliano ya kukopa yanafanyika baada ya kupata kibali cha maandishi kutoka kwa Waziri wa Fedha na Mipango kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, Sura 134 pamoja na marekebisho yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka ujao wa Fedha ni sehemu ya utekelezaji wa

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Kama nilivyoeleza kwenye hotuba ya Hali ya Uchumi kwa Mwaka 2016, maeneo ya vipaumbele yanaakisi Mpango wa Miaka Mitano.

Kwanza ni kukuza uchumi na ujenzi wa msingi wa uchumi wa viwanda; pili, kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu; tatu, Kujenga mazingira wezeshi kwa uendeshaji biashara na uwekezaji; na nne ni kuimarisha usimamizi na utekelezaji wa Mpango. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mpango huu umeweka msisitizo katika kufanikisha utekelezaji wa Miradi Mikubwa ya Kielelezo ambayo ni Ujenzi wa Reli ya Kati kwa kiwango cha *Standard Gauge*; Kuhuisha Shirika la Ndege la Tanzania; Miradi ya Chuma Liganga na Makaa ya Mawe Mchuchuma – Njombe; Uanzishwaji wa Kanda Maalum za Kiuchumi; Mradi wa Gesi Kimiminika (*Liquefied Natural Gas - LNG*); Kituo cha Biashara cha Kurasini; Shamba la Kilimo na Uzalishaji Sukari Mkulazi; na Kusomesha Vijana wa Kitanzania kwa wingi kwenye fani na ujuzi maalum kwa ajili ya maendeleo ya watu na viwanda na kukuza sayansi, teknolojia na ubunifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu hatua za mapato na maboresho ya mfumo wa kodi, ada na tozo mbalimbali. Nitaanza na Hatua za Kiseru na zile za Kiutawala.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kuchukua hatua mbalimbali za kiseru na kiutawala ili kuimarisha na kurahisisha ukusanyaji wa mapato. Hatua hizo ni pamoja na zifuatazo:-

Kwanza, kuimarisha mifumo ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia vifaa na mifumo ya kielektroniki ili kuzuia uvujaji wa mapato ya Serikali. Mfumo uitwao *Government e-payment Gateway System* uko tayari kwa ajili ya matumizi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali. Wizara, Idara na Taasisi zote za Serikali zinaagizwa zianze kutumia mfumo huu. (*Makofi*)

Pili, Serikali imezindua mfumo mpya wa ukusanyaji mapato kwa njia ya kielektroniki [*Electronic Revenue Collection System*] ambao utadhibiti udanganyifu unaofanywa na Maafisa wa Serikali kwa kushirikiana na walipa kodi katika kukadiria kodi hii.

Mheshimiwa Spika, aidha, mfumo huu utawasaidia walipa kodi kwa kuwa na uhakika wa kiasi cha kodi wanachopaswa kulipa. Mfumo huu wa *e-RCS* utaanza rasmi katika mwaka huu wa fedha kwa usimamizi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), hiyo ni kwa upande wa Bara na kwa upande wa Zanzibar Mamlaka ya Mapato Zanzibar (*ZRB*). (*Makofi*)

Tatu, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Serikali itaendelea na ukusanyaji wa kodi ya majengo yaliyothaminiwa na yasiyothaminiwa kwenye Halmashauri zote nchini. Jukumu hili litasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania. Serikali itatoza Kodi ya Majengo kwa nyumba zote katika Miji, katika Majiji, Miji Midogo nchini kwa viwango vitakavyopangwa na Waziri wa Fedha na Mipango. Nyumba ambazo hazijafanyiwa uthamini zitatozwa kwa kiwango maalum (*flat rate*) cha Sh.10,000/= kwa nyumba na Sh.50,000/= kwa nyumba za ghorofa kwa kila ghorofa. (*Makofi*)

Nne, Kuwatambua rasmi wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi na wanaofanyia biashara katika maeneo yasiyo rasmi. Kwa mfano, mama lishe, wauzaji wa mitumba wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo kama mboga mboga, ndizi, matunda na kadhalika kwa kuwapatia vitambulisho maalum vya kazi wanazozifanya ili hatimaye wapatiwe maeneo rasmi ya kufanyia biashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hili lina wadau wengi, narudia. "Kuwatambua rasmi wafanyabiashara wadogo wadogo wasio rasmi na wanaofanyia biashara katika maeneo yasiyo rasmi, mfano mama lishe, wauzaji mitumba wadogo wadogo, wauza mazao ya kilimo wadogo kama mboga



mboga, ndizi, matunda na kadhalika, kwa kuwapatia vitambulisho maalum vya kazi wanazozifanya ili hatimaye wapatiwe maeneo rasmi ya kufanyia biashara." (Makofi)

Tano, ni kuendelea kusimamia na kuhimiza matumizi ya mashine za kielektroniki (*Electronic Fiscal Devices*) kwenye Wizara, Idara, Taasisi za Serikali na wafanyabiashara.

Sita, Serikali itafungua akaunti maalum (*Escrow Account*) kuanzia mwezi Julai, 2017 ili kurahisisha na kuhakikisha kwamba marejesho ya Ushuru wa Forodha wa Ziada (*Additional Import Duty*) wa asilimia 15 unaolipwa na waagizaji wa sukari ya viwandani yanafanyika kwa wakati. Hatua hii itaiwezesha Mamlaka ya Mapato kufanya marejesho kwa wakati kwa wazalishaji wanaotumia sukari hiyo katika kuzalisha bidhaa mbalimbali. (Makofi)

Saba, Serikali haitaruhusu usafirishaji wa madini kutoka migodini na kupeleka moja kwa moja nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, narudia tena; Serikali haitaruhusu usafirishaji wa madini kutoka migodini na kupeleka moja kwa moja nje ya nchi. Aidha, Serikali itaanzisha maeneo maalum (*clearing houses*) katika viwanja vya Kimataifa, migodini, bandarini, mipakani na kadhalika ambapo madini hayo yatathibitishwa na kupewa kibali cha kusafirisha madini hayo ambacho kitatozwa ada ya asilimia moja (*clearing fee*) ya thamani ya madini hayo. Serikali itatangaza rasmi tarehe ya kuanza utaratibu huu katika Sheria ya Fedha ya Mwaka 2017. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na hatua za kisera na za kiutawala za kuboresha ukusanyaji wa mapato, napenda kuwasilisha mapendekezo ya kufanya marekebisho ya mfumo wa kodi ikiwemo kurekebisha baadhi ya viwango vya kodi, tozo na ada chini ya sheria mbalimbali. Aidha, marekebisho hayo yanalenga pamoja na mambo mengine, kuongeza mapato ya Serikali, kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi hususan katika Sekta ya Viwanda, Kilimo, Usafirishaji na Kukuza

Ajira. Aidha, kama nilivyoeleza awali, marekebisho haya hayataathiri kwa kiwango kikubwa utulivu na utabirifu wa mfumo wa kodi. Marekebisho hayo ni pamoja na sheria zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani. Napendekeza kufanya maboresho kwenye Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, Sura ya 148, kama ifuatavyo:-

Kwanza, ni Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye bidhaa za mtaji (*capital goods*) ili kupunguza gharama za ununuzi na uagizaji wa mashine na mitambo ya kuzalishia na hivyo kuvutia uwekezaji katika Sekta ya Viwanda. Aidha, hatua hii itahusisha viwanda vya mafuta ya kula, nguo, ngozi, madawa ya binadamu na mifugo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuvutia uwekezaji katika Sekta za Viwanda, Kilimo na Mazao na Mifugo na Kukuza ajira na uchumi wa nchi. Aidha, hatua hii itawezesha viwanda vidogo na vya kati kupata unafuu wa gharama za kulipa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa mashine na mitambo watakayonunua kwa ajili ya kusindika na kutengeneza bidhaa mbalimbali. Mitambo na mashine zote zitakazosamehewa Kodi ya Ongezeko la Thamani zitaainishwa kwa kutumia *HS Codes*. (*Makofi*)

Pili, kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa kiwango cha asilimia sifuri katika huduma zinazotolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa na mizigo nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie, “kutoza Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa Kiwango cha asilimia sifuri katika huduma zinazotolewa kwenye usafirishaji wa bidhaa na mizigo nje ya nchi (*ancillary transport services*). Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za usafirishaji katika bandari zetu kwa kuifanya Tanzania kuwa njia bora zaidi ya kupitisha bidhaa zinazotoka nje ya nchi. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kupunguza gharama ya usafirishaji katika bandari zetu kwa kuifanya Tanzania kuwa njia bora zaidi ya kupitisha bidhaa zinazotoka nje ya nchi kwenda nchi nyingine na hususan nchi zisizo na bandari (*landlocked countries*). Hatua hii itahamasisha wasafirishaji kutoka nchi jirani kupitisha mizigo yao kwa wingi kwenye bandari zetu na hivyo kukuza uchumi wa nchi kutokana... (*Makofi/Vigelegele*)

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, natamani nihoji; hii bajeti bado inahitaji kuendelea kusomwa kweli! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri wa Fedha, endelea tu. (*Kicheko/Makofi*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, hatua hii pia itawezesha kukua kwa sekta ya bandari, kutachangia kuongezeka kwa ajira nchini. (*Makofi*)

Tatu, ni Kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye vyakula vya mifugo (*compounded animal feeds*) vinavyotengenezwa hapa nchini vinavyotambulika kwa *HS Code 2309*. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za kununua vyakula hivyo kwa wafugaji. (*Makofi*)

Nne, ni kufanya marekebisho kwenye sehemu ya kwanza ya jedwali la misamaha ya kodi kipengele cha 3(13) ili kusamehe Kodi ya Ongezeko la Thamani kwenye mayai ya kutotoleshea vifaranga (*fertilized eggs for incubation*). Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji wa vifaranga na kukuza sekta ndogo ya ufugaji ili iweze kuongeza mchango wake katika pato la Taifa. Hatua hizi zote za Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa ujumla zinatarajiwa kupunguza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 48,034.1. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura 332 kama ifuatavyo:-

Moja, ni kufanya marekebisho kwenye aya ya nne ya jedwali la kwanza la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kurekebisha muda uliotolewa katika kutoza kodi mbadala (*Alternative Minimum Tax*) kwa kampuni zinazopata hasara kwa miaka mitatu mfululizo badala ya miaka mitano mfululizo. Lengo la hatua hii ni kuonisha na aya ya nne ya kifungu cha nne cha sheria hiyo kinachotamka kwamba kodi hiyo itatozwa kwa miaka mitatu mfululizo.

Pili, kufanya marekebisho kwenye jedwali la tatu la Sheria ya Kodi ya Mapato ili kuongeza kiwango cha juu kinachotumika kama gharama ya kukokotoa uchakavu wa magari yasiyo ya kibiashara (*non-commercial motor vehicles*) kutoka shilingi milioni 15 hadi shilingi milioni 30. Lengo la hatua hii ni kufanya au kuhuisha gharama za magari hayo ziendane na gharama za halisi za soko. Marekebisho haya yamezingatia kwamba kiwango cha sasa cha shilingi milioni 15 ni cha muda mrefu na hakiakisi bei halisi ya magari kwa sasa katika soko. (*Makofi*)

Tatu, kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Kodi ya Mapato ili kupunguza kiwango cha Kodi ya Mapato ya Makampuni (*Corporate Income Tax*) kutoka asilimia 30 mpaka asilimia 10 kwa miaka mitano kuanzia mwaka mwekezaji atakapoanza uzalishaji, kwa waunganishaji (*assemblers*) wa magari, matrekta na boti za uvuvi. Lengo la hatua hii ni kuongeza ajira, kuongeza mapato ya Serikali na pia kuhamasisha uhaulishaji wa teknolojia (*technology transfer*). Aidha, Serikali itaingia mkataba wa makubaliano na utekelezaji (*Performance Agreement*) na kila muunganishaji ambao utainisha wajibu wa kila upande. (*Makofi*)

Nne, kuanza kutoza Kodi ya Zuio (*Withholding Tax*) kwa kiwango cha 5% kwenye bei ya kuuzia (*total market value*) ambayo itakua ni Kodi ya Zuio ya mwisho (*Final Withholding Tax*) kwa wachimbaji wadogo wadogo wa madini ya aina zote. Lengo la hatua hii ni kuiwezesha Serikali kupata mapato stahiki kutoka katika Sekta ya Madini. Serikali itatangaza tarehe rasmi ya kuanza utekelezaji katika Sheria ya Fedha ya mwaka 2017. Hatua hizi za Kodi ya Mapato kwa

ujumla wake zinatarajia kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 88.5.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, Sura 147 kama ifuatavyo: -

(i) kufanya marekebisho ya viwango maalum vya ushuru (*specific duty rates*) zinavyotozwa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa kiwango cha mfumuko wa bei cha 5%. Sababu yake ni kuwa pale ambapo Ushuru wa Bidhaa unatozwa kwa viwango maalum, ushuru huo hauakisi mfumuko wa bei na hivyo hupunguza mapato. Njia bora inayotumika kuondoa Upungufu huo ni kurekebisha viwango maalum vya ushuru ili kuendana na kiwango cha mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, utaratibu huu ni tofauti na pale ambapo ushuru wa bidhaa hutozwa kwa kiwango cha asilimia ya thamani ya bidhaa (*advalorem rates*) ambapo hapana sababu ya kurekebisha viwango vya ushuru kwa kuwa thamani ya bidhaa inazingatia mfumuko wa bei.

Mheshimiwa Spika, aidha, marekebisho haya ninayopendekeza ni kwa mujibu wa Sheria ya Ushuru wa Bidhaa Kifungu cha 124(2) inayoelekeza kuwa marekebisho ya viwango vya ushuru yanaweza kufanyika kila mwaka ili kuviwianisha na mfumuko wa bei na viashiria vingine vya uchumi jumla. Hata hivyo, kwa kuzingatia mkakati wa Taifa wa kukuza uchumi wa viwanda, baadhi ya bidhaa zinazozalishwa nchini hazitafanyiwa marekebisho hayo. Mabadiliko ninayopendekeza ni kama ifuatavyo:-

(a) Ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji baridi kutoka Sh.58/= kwa lita hadi Sh.61/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.3/= kwa lita;

(b) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya kunywa yaliyosindikwa kwenye chupa yaliyoagizwa kutoka nje kutoka

Sh.58/= kwa lita hadi Sh.61/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.3/= kwa lita. Aidha, Ushuru wa Bidhaa kwenye maji yanayozalishwa nchini utabaki kuwa Sh. 58/= kwa lita. (*Makofi*)

(c) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda yaani juisi iliyotengenezwa kwa matunda yanayozalishwa hapa nchini (*local juices*) utashuka kutoka Sh.9.5 kwa lita na kuwa Sh.9/= kwa lita;

(d) Ushuru wa bidhaa kwenye maji ya matunda iliyotengenezwa kwa matunda ambayo hayazalishwi hapa nchini (*imported juices*) kutoka Sh. 210/= kwa lita hadi Sh.221/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la asilimia 11 kwa lita;

(e) Ushuru wa bidhaa kwenye bia inayotengenezwa kwa nafaka ya hapa nchini na ambayo haijaoteshwa yaani (*Beer from Local Unmated Cereals*) kutoka Sh.429/= kwa lita hadi Sh.450/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.21/= kwa lita;

(f) Ushuru wa bidhaa kwenye bia nyingine zote kutoka Sh.729/= kwa lita hadi Sh.765/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.36/= kwa lita;

(g) Ushuru wa bidhaa kwenye bia zisizo za kilevi, ikijumuisha vinywaji vya kuongeza nguvu kutoka Sh.534/= kwa lita hadi Sh.561/= kwa lita ikiwa ni ongezeko la Sh.27/= kwa lita. (*Makofi*)

(h) Ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa ndani ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 75, utashuka kutoka Sh.202/= kwa lita na kuwa Sh.200/= kwa lita;

(i) Ushuru wa bidhaa kwenye mvinyo uliotengenezwa kwa zabibu inayozalishwa nje ya nchi kwa kiwango kinachozidi asilimia 25, kutoka Sh.2,236/= kwa lita hadi Sh.2,349/= kwa lita, ikiwa ni ongezeko la Sh.113/= kwa lita. (*Makofi*)

(j) Ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyoagizwa kutoka nje kutoka Sh.3,315/= kwa lita hadi Sh.3,481/= kwa lita, ikiwa ni ongezeko la Sh.166/= kwa lita. Aidha, ushuru wa bidhaa kwenye vinywaji vikali vinavyozalishwa nchini utabaki kuwa Sh.3,315/= kwa lita. (Makofi)

(k) Ushuru wa bidhaa kwenye sigara zisizo na kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka Sh.11,854/= hadi Sh.12,447/= kwa kila sigara 1,000, ikiwa ni ongezeko la Sh.593/= kwa kila sigara 1,000;

(l) Ushuru wa bidhaa kwenye sigara zenye kichungi zinazotengenezwa kutokana na tumbaku inayozalishwa hapa nchini kwa kiwango cha angalau asilimia 75, kutoka Sh.28,024/= hadi Sh.29,425/= kwa kila sigara 1,000, ikiwa ni ongezeko la Sh.1,401/= kwa kila sigara 1,000;

(m) Ushuru wa bidhaa kwenye sigara zenye sifa tofauti na (k) na (l) kutoka Sh.50,700/= hadi Sh.53,235/= kwa kila sigara 1,000 ikiwa ni ongezeko la Sh.2,535/= kwa kila sigara 1,000;

(n) Ushuru wa bidhaa kwenye tumbaku ambayo iko tayari kutengeneza sigara (*cut filler*) kutoka Sh.25,608/= hadi Sh.26,888/= kwa kilo, ikiwa ni ongezeko la Sh.1,280/= kwa kilo; na

(o) Ushuru wa bidhaa wa '*cigar*' unabaki kuwa asilimia 30.

Mheshimiwa Spika, pili, napendekeza kufuta Ada ya Mwaka ya Leseni ya Magari (*Annual Motor Vehicle Licence Fee*). (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, Waheshimiwa Wabunge hawajakusikia bado hili ulilozungumza, bado hawajasikika vizuri. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, napendekeza kufuta Ada ya Mwaka ya Leseni ya Magari *(Annual Motor Vehicle Licence Fee)* iliyokuwa inalipwa hata kwa magari ambayo hayatumiki ambayo imekuwa ikilalamikiwa kwa muda mrefu; badala yake ada hiyo itatozwa kwa magari yanayotembea tu. Kwa sababu hiyo, ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli, dizeli na taa utaongezeka kwa kiasi cha Sh.40/= kwa lita moja kutoka kiwango cha sasa cha Sh.339/= kwa lita hadi Sh.379/= kwa lita kwa mafuta ya petrol; kutoka kiwango cha sasa cha Sh.215/= kwa lita hadi Sh.255/= kwa lita kwa mafuta ya dizeli na kutoka kiwango cha sasa cha Sh.425/= kwa lita hadi Sh.465/= kwa lita kwa mafuta ya taa.

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuwaondolea wananchi usumbufu wa kudaiwa ada hii hata kwa magari ambayo hayatumiki. Hatua za ushuru wa bidhaa kwenye bidhaa zisizo za petroli kwa ujumla wake zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 27,801.8. *(Makofi/Vigelele)*

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Usalama Barabarani, Sura 168 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kama nilivyopendekeza, ni kufuta Ada ya Mwaka ya Leseni ya Magari ili ada hii ilipwe mara moja tu gari linaposajiliwa na baada ya hapo iendelee kulipwa kupitia ushuru wa bidhaa kwenye mafuta ya petroli na dizeli. Aidha, Serikali inatoa msamaha wa kodi, riba na adhabu zinazoambatana na madeni yote *(Tax Amnesty)* ya ada hiyo yaliyolimbikizwa kwa miaka ya nyuma... *(Makofi/Vigelele)*

*(Hapa Baadhi ya Waheshimiwa Wabunge waliimba CCM, CCM, CCM!)*



**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, aendelee, imetoshala!

**WABUNGE FULANI:** Aendelee!

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, endelea. (*Kicheko*)

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, naomba kurudia. Serikali inatoa msamaha wa kodi, riba na adhabu zinazoambatana na madeni yote ya ada hiyo yaliyolimvikizwa kwa miaka ya nyuma. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, inapendekezwa pia kuongeza Ada ya Leseni ya Magari wakati wa usajili mara ya kwanza (*Annual Motor Vehicle Licence Fee on First Registration*). Ongezeko la Ada ya Leseni ya Magari wakati wa usajili ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, gari lenye ujazo wa injini ya 501-1500 cc kutoka kiwango cha sasa cha Sh.150,000/= hadi Sh.200,000/=, ikiwa ni ongezeko la Sh.50,000/=; gari lenye ujazo wa injini ya cc 1501-2500 kutoka kiwango cha sasa cha Sh.200,000/= hadi Sh.250,000/=, ikiwa ni ongezeko la Sh.50,000/=; na gari lenye ujazo wa injini ya cc 2501 na zaidi kutoka kiwango cha sasa cha Sh.250,000/= hadi Sh.300,000/=, ikiwa ni ongezeko la Sh.50,000/=. Hatua hizi kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 77,603.5. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge mnisikilize vizuri. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kupunguza Ushuru wa Mazao (*Produce Cess*) unaotozwa na Halmashauri za Wilaya kutoka kiwango cha sasa cha 5% ya thamani ya mauzo (*Gross Value*) hadi 3% kwa mazao ya biashara na 2% kwa mazao ya chakula. Aidha, mtu anayesafirisha mazao yake kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine yasiyozidi tani moja asitozwe ushuru. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii...

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, kelele zilikuwa nyingi. Waheshimiwa Wabunge, tumsikilize Mheshimiwa Waziri, maana haya ni mambo ya wananchi. Mheshimiwa Waziri hebu rudia halafu uendelee. *(Makofi/Vigelegele)*

**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, narudia. Napendekeza kufanya marekebisho kwenye Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ili kupunguza Ushuru wa Mazao unaotozwa na Halmashauri za Wilaya kutoka kiwango cha sasa cha 5% ya thamani ya mauzo hadi 3% kwa mazao ya biashara na 2% kwa mazao ya chakula. Aidha, Mtu anayesafirisha mazao yake kutoka Halmashauri moja kwenda nyingine yasiyozidi tani moja asitozwe ushuru. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, lengo la hatua hii ni kuwawezesha wakulima wetu kupata bei stahiki ya mazao yao na hivyo kuboresha mapato yao. Hatua hii inatarajiwa kuhamasisha uzalishaji wa mazao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya kikao cha maandalizi ya bajeti tarehe 6 Mei, 2017 Mjini Arusha, Tanzania. Kikao hicho kilipendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha (*EAC- Common External Tariff*) na Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*EAC Customs Management Act, 2004*) kwa mwaka 2017/2018. Mapendekezo hayo yanalenga kwa kiwango kikubwa katika kukuza viwanda ndani ya nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kuongeza ajira na kunufaisha watu wote.

Mheshimiwa Spika, maeneo yaliyopendekezwa kufanyiwa marekebisho kwenye viwango vya Ushuru wa Pamoja wa Forodha ni kama ifuatavyo:-

Moja, kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 35 kwa mwaka mmoja kwenye ngano inayotambuliwa katika *HS Code* 1001.99.00 na *HS Code* 1001.99.90. Hatua hii itahusu viwanda vinavyotumia

bidhaa hii katika uzalishaji (*duty remission*). Aidha, imezingatia kwamba uzalishaji wa bidhaa hii katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ni mdogo na hivyo hautoshelezi mahitaji. Pia inatoa unafuu kwa viwanda na wazalishaji wa bidhaa na vyakula vinavyotumia ngano na kuimarisha utulivu wa bei wa bidhaa zinazozalishwa kwa kutumia ngano hiyo.

Pili, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri badala ya asilimia 10 kwenye malighafi inayotumika katika kutengeneza sabuni (*LABSA*) inayotambuliwa katika *HS Code* 3402.11.00, *HS Code* 3402.12.00 na *HS Code* 3402.19.00 kwa kipindi cha mwaka mmoja. Hatua hii itahusu viwanda vinavyotumia malighafi hii katika uzalishaji, (*duty remission*). Lengo la hatua hii ni kutoa unafuu wa gharama za uzalishaji kwa viwanda vidogo na vya kati vya kutengeneza sabuni na hivyo kuweza kuongeza uzalishaji na ajira.

Tatu, kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya asilimia 25 kwa mwaka mmoja kwenye viunganishi vya pikipiki. Hatua hii itahusu viwanda vinavyotumia viunganishi hivyo katika kuunganisha pikipiki (*duty remission for Motorcycle Assemblers*). Lengo la hatua hii ni kuendelea kuhamasisha uunganishaji wa pikipiki katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, wakati wataalam wanaandaa orodha ya viunganishi ambavyo vitastahili kupata msamaha wa Ushuru wa Forodha na ambavyo havitastahili. Baada ya kuainisha orodha ya viunganishi visivyostahili kupata msamaha wa Ushuru wa Forodha, waunganishaji watahamasishwa kuvitengeneza ndani ya nchi wanachama wa Jumuiya. (*Makofi*)

Nne, kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia sifuri kwenye mafuta ghafi ya kula (*crude palm oil*) yanayotambulika katika *HS Code* 1511.10.00 kwa mwaka mmoja. Hatua hii inalenga katika kuhamasisha kilimo cha mbegu za mafuta hapa nchini na kukuza viwanda vya kutengeneza mafuta ya kula. Aidha, inazingatia mkakati maalum wa kuendeleza na kulinda viwanda vya kuzalisha mafuta ya kula yanayotokana na mbegu zinazozalishwa

hapa nchini na kutumia fursa ya soko kubwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Tanzania ina nafasi kubwa ya kuweza kuongeza uzalishaji wa mbegu za mafuta. *(Makofi)*

Tano, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au kiwango maalum cha Dola za Kimarekani 250 kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwa kila tani moja ya ujazo (*metric ton*) kwenye bidhaa za chuma (*Flat rolled Iron or non-alloy Steel*) kwa mwaka mmoja zinazotambuliwa katika *HS Codes: 7210.41.00* mpaka *7212.60.00*. Hatua hii inalinda uzalishaji wa bidhaa za chuma zinazozalishwa na viwanda vya ndani dhidi ya ushindani wa bidhaa za aina hiyo zinazoingizwa kutoka nje ya jumuiya. *(Makofi)*

Sita, kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 au dola za Kimarekani 200 kwa kila tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za chuma (*Steel Rods and Bars and Hot rolled Angles, Sections*) Hatua hii inatekelezwa ili kulinda uzalishaji wa bidhaa hizo za chuma kutokana na ushindani unaosababishwa na uingizaji wa bidhaa hizo kutoka nje ya nchi. Aidha, hatua hii inahamasisha uwekezaji na kuongeza ajira.

Saba, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri badala ya asilimia 25 au Dola za Kimarekani 200 kwa tani ya chuma (*HS Code 7228.20.00*) kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwa wazalishaji wa spring za magari (*leaf spring*). Hatua hii itahusu viwanda vinavyotumia bidhaa hii katika uzalishaji (*duty remission*). Kiwango cha asilimia 25 au Dola za Kimarekani 200 kiliwekwa mwaka 2016/2017 kulinda wazalishaji wa bidhaa za chuma hapa nchini wakati wazalishaji wa spring za magari walikuwa wanahitaji kutumia bidhaa hizo kama malighafi. *(Makofi)*

Nane, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 au Dola za Kimarekani 125 kwa tani moja ya ujazo kutegemea kiwango kipi ni kikubwa kwenye bidhaa za chuma (*Flat-rolled products of iron or non alloy steel of a width of 600mm or more, cold rolled or cold reduced*) kwa mwaka mmoja. Lengo

la hatua hii ni kulinda viwanda vyetu kutokana na ushindani wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. (Makofi)

Tisa, kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri kwenye malighafi za kutengeneza chujio za hewa za magari (*air filters*). Hatua hii itahusu viwanda vyote vinavyotumia bidhaa hii katika uzalishaji wa chujio hizo (*duty remission*) katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha uzalishaji wa bidhaa hiyo na kukuza ajira. (Makofi)

Kumi, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 10 badala ya asilimia sifuri kwenye *gypsum powder* inayotambuliwa chini ya *HS Code* 2520.20.00 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kulinda viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo hapa nchini na kuhamasisha wawekezaji watumie *gypsum* inayopatikana hapa nchini katika kuzalisha *gypsum powder*; na kwa kufanya hivyo tutaongeza ajira na mapato. (Makofi)

Kumi na moja, kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia 10 badala ya kuongeza kiwango hicho hatua kwa hatua hadi kufikia asilimia 25 mwaka wa 2018/2019 kwenye sukari inayotumika viwandani. Hatua hii itahusu viwanda vyote vinavyotumia sukari hiyo katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Hatua ya kutoongeza Ushuru wa Forodha imezingatia kuwa sukari inayotumika viwandani ni malighafi ya maana katika kuzalisha chakula, vinywaji na madawa ambavyo ni muhimu kwa mahitaji ya binadamu.

Kumi na mbili, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri badala ya asilimia 10 kwenye mashine za kielektroniki za kukusanya mapato ya hazina (*Electronic Fiscal Devices*) zinazotambuliwa chini ya *HS Code* 8470.50.90 kwa mwaka mmoja. Lengo la hatua hii ni kuhamasisha wafanyabiashara na walipa kodi kutumia mashine hizo katika kufanya mauzo na kuongeza ufanisi katika usimamizi na udhibiti wa kodi. (Makofi)

Kumi na tatu, kuendelea kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia 10 kwenye bidhaa za karatasi. Hatua hii imeendelea kutekelezwa ili kuvilinda viwanda vya ndani vinavyozalisha karatasi hizo kutokana na ushindani wa bidhaa zinazoingizwa kutoka nje ya nchi. (Makofi)

Kumi na nne, kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya asilimia 25 kwenye malighafi na vifaa vinavyoagizwa nje ya nchi kwa ajili ya kuunganisha na kutengeneza vifaa ambavyo ni mahsusi kwa ajili ya matumizi ya walemavu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba nirudie ili ndugu zetu wasikie. Ni kutoza Ushuru wa Forodha kwa kiwango cha asilimia sifuri badala ya asilimia 25 kwenye malighafi na vifaa vinavyoagizwa nje ya nchi kwa ajili ya kuunganisha na kutengeneza vifaa ambavyo ni mahsusi kwa ajili ya matumizi ya walemavu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, aidha, hatua hii itahusu waunganishaji wa vifaa hivyo tu. Hivyo waunganishaji (*assemblers*) wa vifaa hivyo watanufaika na punguzo la ushuru huo. Aidha, lengo la kuchukua hatua hii ni kuhamasisha uwekezaji katika kuzalisha vifaa hivyo muhimu ndani ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na kukuza ajira. (Makofi)

Kumi na tano, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia 25 badala ya asilimia sifuri kwenye muundo wa *aluminium* inayotambuliwa kwenye *HS Code 7610.90.00* kwa mwaka mmoja. Hatua ya kuweka kiwango hiki cha ushuru inalenga katika kutofautisha vifaa vyenye kufanana lakini vina ubora tofauti, hali ambayo inasababisha ukwepaji kodi.

Kumi na sita, kufanya marekebisho katika uandishi wa *HS Code 4911.99.20* ili kujumuisha karatasi zinazotumika kwenye shule katika kujibu maswali (*examination answer sheet*) ili nazo ziweze kutozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia

sifuri kama vile karatasi za maswali (*question papers*) zinavyotozwa. Hatua hii itapunguza gharama za kutoa elimu nchini. (*Makofi*)

Kumi na saba, kutoza Ushuru wa Forodha wa asilimia sifuri kwenye vifaa vinavyotumika katika ujenzi na uunganishaji wa meli (*inputs for use in the manufacture and assembling of ships*). Hatua hii itawahusu wajenzi na waunganishaji wa meli. Lengo ni kutoa unafuu wa gharama katika kutengeneza meli au kuunganisha. Aidha, hatua hii itahamasisha uvuvi, kuimarisha usafiri wa majini na kuongeza ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mawaziri wa Fedha wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki walifanya pia marekebisho kwenye Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (*The East African- Customs Management Act, 2004*) kama ifuatavyo:-

Kwanza, kufanya marekebisho katika Kifungu B cha Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa kufuta aya ya 25 ili kuondoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye taa zinazojulikana kama *Compact Fluorescent Bulbs (CFL)* na *Light Emitting Bulbs (LEI)*. Hatua hii imezingatia kwamba msamaha huo hauna tija hivi sasa kwa kuwa bidhaa hizo ni zile ambazo zimetengenezwa kwa kiwango kilichokamilika kwa matumizi (*finished goods*) na hivyo zinastahili kutozwa Ushuru wa Forodha wa asilimia 25.

Pili, kufanya marekebisho katika sehemu ya 203 ya Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na kuongeza adhabu (*fine*) kutoka Dola za Kimarekani 10,000 hadi dola za Kimarekani 20,000 au asilimia 50 ya kodi iliyostahili kulipwa kutegemea kiwango kipi ni kikubwa. Lengo ni kuweka adhabu kali kwa makosa yanayofanywa na waagizaji mizigo kama vile kuwasilisha nyaraka zisizo sahihi, taarifa zisizo sahihi, kukwepa kodi kwa njia ya kughushi na kadhalika. Hatua hii

imezingatia adhabu ya juu inayotozwa hivi sasa ni dola za Kimarekani 10,000 ambazo ni ndogo na haziwezi kupunguza makosa ya namna hiyo.

Tatu, kufanya marekebisho katika Kifungu cha 218 cha Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kumpa mamlaka Kamishna wa Forodha kumrejeshea mlipa kodi bidhaa ambazo zilikuwa zimezuiliwa badala ya utaratibu wa sasa unaotoa mamlaka hayo kwa Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Nne, kufanya marekebisho katika aya ya 30 ya Jedwali la Tano la Sheria ya Forodha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuongeza usambazaji wa mafuta na gesi katika misamaha inayotolewa kwenye miradi ya gesi na mafuta. Hatua hii ina lengo la kutoa msamaha wa Ushuru wa Forodha kwenye miradi ya mabomba ya mafuta inayotekelezwa na nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za Ushuru wa Forodha kwa pamoja zinatarajiwa kuongeza mapato ya Serikali kwa kiasi cha shilingi milioni 16,053.9.

Mheshimiwa Spika, marekebisho madogo madogo katika baadhi ya Sheria za Kodi na Sheria nyingine mbalimbali; napendekeza kufanya marekebisho mengine madogo madogo yasiyo ya kisera katika sheria mbalimbali za kodi pamoja na sheria nyingine mbalimbali ili ziwe sanjari na azma ya kurahisisha utekelezaji wake. Marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 na Matangazo ya Serikali *(Government Notices)*.

Mheshimiwa Spika, napendekeza kufanya marekebisho ya viwango vya ada na tozo mbalimbali zinazotozwa na Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea ili kuvihuisha kulingana na hali halisi ya ukuaji wa uchumi. Aidha, marekebisho hayo yataainishwa katika Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2017 na Matangazo ya Serikali. Marekebisho hayo yatajumuisha:-



(i) Kufuta ada ya ukaguzi wa viwango, ada ya ukaguzi wa mionzi na ada ya wakala wa vipimo kwenye mbolea inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania, Tume ya Mionzi Tanzania na Wakala wa Vipimo Tanzania. Lengo la hatua hii ni kuwapunguzia wakulima wetu gharama za pembejeo na hivyo kuongeza tija katika uzalishaji. *(Makofi)*

(ii) Kufuta ada ya ukaguzi wa viwango kwa mazao ya biashara kama pamba, chai, korosho na kahawa inayotozwa na Shirika la Viwango Tanzania. Lengo la hatua hii ni kupunguza gharama za uzalishaji kwa viwanda vinavyosindikika mazao haya na pia kuongeza mapato kwa wakulima; *(Makofi)*

(iii) Kufuta Ushuru wa Huduma *(Service Levy)* kwenye nyumba za kulala wageni ambazo zinatuzwa *Guest House Levy*. *(Makofi)*

(iv) Kufuta Ushuru wa Mabango kwa mabango yanayoelekeza mahali huduma za jamii... *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, naomba kurudia, kufuta Ushuru wa Mabango kwa mabango yanayoelekeza mahali huduma za jamii hususani shule na hospitali au zahanati zinapopatikana. Aidha, kuanzia tarehe 1 Julai, 2017 Mamlaka ya Mapato Tanzania itaanza kukusanya Ushuru wa Mabango ya Matangazo kwa nchi nzima. *(Makofi)*

(v) Kufuta ada ya vibali vinavyotolewa na Mamlaka za Serikali za Mitaa mfano vibali vya machinjio (isipokuwa ada ya machinjio na ada ya ukaguzi wa nyama), ada ya vibali vya kusafirisha mifugo na ada ya vibali vya kuanzisha maduka ya dawa. *(Makofi)*

(vi) Kufuta ada ya makanyagio minadani; na *(Makofi)*

(vii) Kufanya marekebisho ya kiwango cha faini kwa makosa ya watakaoenda kinyume na masharti ya Sheria

ya Fedha za Serikali za Mitaa kutoka kiasi kisichozidi Sh.50,000/= na kifungo kisichozidi miezi 12 hadi kiasi kisichopungua Sh.200,000/= na kisichozidi Sh.1,000,000/= au kifungo kisichopungua miezi 12 na kisichozidi miaka miwili.

Mheshimiwa Spika, Serikali itaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya tozo na ada zinazotowza na mashirika, taasisi na wakala mbalimbali ili kuendelea kuweka mazingira bora ya kufanya biashara/kuwekeza na kuondoa kero kwa wananchi. Hii itajumuisha kupitia upya na kuvisawazisha viwango vya tozo na ada hizo na pia kuondoa tozo na ada za usumbufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hatua hizi za kodi zinazopendekezwa zitaanza kutekelezwa tarehe 1 Julai, 2017, isipokuwa pale ilipoelezwa vinginevyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Sura ya Bajeti; kwa kuzingatia shabaha na sera za bajeti kwa mwaka 2017/2018, sura ya bajeti inaonesha kuwa jumla ya shilingi trilioni 31.7 zinatarajiwa kukusanywa na kutumika katika kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, jumla ya mapato ya ndani ikijumuisha mapato ya Halmashauri yanatarajiwa kuwa shilingi trilioni 19.9, sawa na asilimia 63 ya bajeti yote. Kati ya mapato hayo, Serikali inalenga kukusanya mapato ya kodi ya jumla ya shilingi trilioni 17.1 sawa na asilimia 85.6 ya mapato ya ndani. Aidha, mapato yasiyo ya kodi ni shilingi trilioni 2.1 na mapato kutoka vyanzo vya Halmashauri ni shilingi bilioni 687.3.

Mheshimiwa Spika, Washirika wa Maendeleo wanatarajiwa kuchangia shilingi trilioni 3.9 ambayo ni asilimia 12.5 ya bajeti yote. Misaada na mikopo hii inajumuisha miradi ya maendeleo shilingi bilioni 2,473.8; mifuko ya pamoja ya kisekta shilingi bilioni 556.1; na misaada ya kibajeti *(GBS)* shilingi bilioni 941.2.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 7.7 kutoka soko la ndani na nje kwa masharti ya

kibiashara. Mikopo ya ndani inatarajiwa kuwa shilingi trilioni 6.1, ambapo shilingi trilioni 4.9 ni kwa ajili ya kulipia dhamana za Serikali zinazoiva na shilingi trilioni 1.2 sawa na asilimia moja ya pato la Taifa ni mikopo mipya kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Ili kuongeza kasi katika ujenzi wa miundombinu, Serikali inatarajia kukopa shilingi trilioni 1.5 kutoka soko la nje.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali itaongeza jitihada za ukusanyaji wa mapato ya ndani pamoja na mikopo ya ndani na nje ili kutekeleza miradi ya maendeleo. Miradi mikubwa ya maendeleo ikiwemo awamu zinazofuata za ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha *standard gauge* na uboreshaji wa bandari mbalimbali nchini, vitatekelezwa kulingana na mpangokazi kutegemea mwenendo wa mapato ya ndani na nje utakaojidhihirisha baada ya kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Julai hadi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, aidha, mara baada ya ridhaa ya Serikali kupatikana, utaratibu wa kutoa hatifungani maalum (*special non-cash bond*) utatekelezwa ili kusaidia kupunguza madeni yaliyohakikiwa ya Serikali kwa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka ujao wa fedha, Serikali inapanga kutumia jumla ya shilingi trilioni 31.7. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 19.7 zimetengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, ikijumuisha shilingi trilioni 7.2 za mishahara na shilingi trilioni 9.4 kwa ajili ya kulipia deni la umma na huduma nyinginezo. Aidha, matumizi ya maendeleo yatakuwa shilingi trilioni 11.9 sawa na asilimia 38 ya bajeti yote, ambapo shilingi trilioni 8.9 ni fedha za ndani na shilingi trilioni 3.0 ni fedha za nje.

Mheshimiwa Spika, kiwango hiki kimezingatia wigo wa asilimia 30 hadi asilimia 40 ya bajeti yote iliyoidhinishwa katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia mfumo wa bajeti kama nilivyoeleza, sura ya bajeti kwa mwaka 2017/2018 tumeionesha kwenye Jedwali Na. A.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, hatua zilizopendekezwa kwenye bajeti hii zinalenga kujenga msingi madhubuti wa uchumi wa viwanda na kupanua fursa za ajira na biashara. Dhamira yetu sote ni kufikia kiwango cha uchumi wa kipato cha kati ifikapo 2025. Ili kushiriki katika mafanikio hayo, ni lazima kila mmoja wetu ashiriki katika shughuli halali ya uzalishaji na afanye hivyo kwa juhudi na maarifa ili kuleta tija. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufanikiwa kwa bajeti hii kunahitaji nidhamu ya hali ya juu katika usimamizi wa mapato na matumizi. Ili kufikia azma hii, juhudi za pamoja kati ya Serikali na wadau wote zinahitajika ikiwa ni pamoja na kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika uchumi kwa kuwekeza zaidi katika maeneo ya kipaumbele. Natoa rai kwa kila Mtanzania kutimiza wajibu wake ili Bajeti hii iweze kutekelezwa kama ilivyopangwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mojawapo ya masharti ambayo nchi yetu haina budi kuyatimiza ili Tanzania ifikie mapinduzi ya kiuchumi na kijamii kwa haraka ni pamoja na kuwa na viongozi wenye sifa za kuleta na kusimamia mabadiliko na sifa za viongozi wa aina hiyo ni zifuatazo:-

(1) Wanafanya jitihada kuwa binadamu wema, wanaojali na kusaidia watu wengine hasa wanyonge, wanakuwa na maadili mema, ni waaminifu na wanatenga muda kutafakari juu ya utumishi wao kwa umma. *(Makofi)*

(2) Wanakuwa na dira kuhusu wapi pa kuipeleka nchi kutoka ilipo sasa na kujiwekea malengo makubwa. *(Makofi)*

(3) Wanaweka viashiria vya mafanikio kwa kila programu na mradi utakaotekelezwa. *(Makofi)*

(4) Wanasimamia kidete muda wa utekelezaji.  
(Makofi)

(5) Wanatoa maamuzi magumu na maelekezo thabiti kwa kutambua kuwa hakuna mchezo usio na maumivu sambamba na kuandaa na kuwawezesha viongozi watakaopokea kijiti. (Makofi)

(6) Wanateua kwa umakini na kufanya kazi pamoja na timu hiyo madhubuti ya ushindi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naamini na Bunge lako Tukufu na Watanzania walio wengi watakubaliana nami kuwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anazo sifa zote hizi.  
(Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Spika, narudia tena, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anazo sifa zote hizi. Ni kiongozi mzalendo, anayependa na kujivunia nchi yake ya Tanzania; ni kiongozi ambaye amejielekeza kuijenga Tanzania mpya; anao moyo thabiti, nia njema na amejifunga kuwatumikia Watanzania wote na hasa wanyonge; ana msimamo thabiti usioyumba; anayo dhamira ya dhati ya kusimamia utendaji uliotukuka; anachukia rushwa na ubadhirifu na ufisadi na wizi wa rasilimali za umma; anao uthubutu wa kufanya mambo mapya tofauti lakini yenye maslahi kwa Taifa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nirudie, ana uthubutu wa kufanya mambo mapya tofauti yenye maslahi kwa Taifa kinyume na mazoea, hata kama hayawapendezi baadhi ya watu.  
(Makofi/Vigelele)

Mheshimiwa Spika, sasa Watanzania wote tumeanza kuona matokeo. Ndani ya kipindi kifupi cha miezi 18 ya uongozi wake, Mheshimiwa Rais amefanya mambo mengi makubwa sana. Mengi yamefufua matumaini na ari ya wananchi walio wengi, lakini kwa wachache yamekuwa machungu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba niyarejee kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Ametengua uteuzi wa viongozi mbalimbali ambao aliwaona hawaendi na dhamira na kasi yake; amekamata makontena yaliyoondolewa bandarini bila kulipa kodi stahiki; amewaondoa Serikalini watumishi wasio na sifa au vyeti halali na wanafunzi hewa; ameimarisha matumizi ya fedha za Umma; amedhibiti mishahara na madai hewa; amerejesha nidhamu kwa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali; kulipa madeni ya umeme, maji na huduma nyingine; amegharamia elimu msingi bila malipo, ameongeza ukusanyaji wa kodi kutoka wastani wa shilingi bilioni 800 kwa mwezi hadi wastani wa Sh.1,200,000,000,000/=. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia amethubutu kutekeleza uamuzi wa muda mrefu wa kuhamishia Makao Makuu ya Serikali Dodoma; amemtaka kila Mtanzania afanye kazi; ameanza utekelezaji wa kujenga reli yetu kwa kiwango cha *standard gauge*; na amenunua ndege mbili mpya na kufanya malipo ya awali kwa ndege nyingine nne ili kufufua Shirika letu la Ndege na kuinua utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vile vile ameshawishi Serikali ya Uganda kuridhia mradi mkubwa wa bomba la mafuta lijengwe kutoka Hoima – Uganda hadi Bandari ya Tanga katika mazingira makali sana ya ushindani mkali; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa barabara mbalimbali nchini ikiwemo *flyover*, TAZARA na *interchange* Ubungo na ujenzi wa miradi ya miundombinu ya umeme, maji na meli mpya. Katika uongozi wake ajenda ya kujenga uchumi wa viwanda imepata mwitikio mkubwa sana kutoka sekta binafsi nchini na hususan Ukanda wa Pwani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafurahi kuwaambia Watanzania wenzangu kuwa hatua hizo ni uwekezaji wa lazima na ni uwekezaji wa busara (*sensible investment*). Bajeti hii ya mwaka 2017/2018 itaendelea kuimarisha matokeo haya na kuchukua hatua zaidi ili twende mbele kwa haraka zaidi. Ukiona vinaelea, ujue vimeundwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa Watanzania wenzangu na hasa sisi viongozi na wananchi wote, ni kwamba lazima tujitoe kujenga Tanzania, tumuunge mkono Rais wetu kwa vitendo na kwa kila mtu kufanya kazi kweli kweli tukijielekeza kutekeleza dira na malengo ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga ustawi wa uchumi imara unaotengeneza ajira, fursa mpya na mgawanyo wa haki na usawa wa rasilimali za Watanzania kwa wananchi wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tulinde umoja na amani yetu kama mboni ya jicho na tena letu liwe moja katika masuala yote yenye maslahi kwa Taifa letu. Naomba nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali kuwashukuru na kuwapongeza kwa dhati kabisa wananchi wote ambao wanalipa kodi stahiki ambao ndio wananchi waliofanikisha maendeleo niliyoyataja. Serikali inawaahidi kutumia vizuri mapato yatokanayo na kodi zenu kuwaletea maendeleo. Wale mnaojaribu kukwepa kodi, mkono wa sheria utachukua mkondo wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapokaribia kumaliza hotuba hii, naomba kuwatambua na kuwashukuru Washirika wetu wa Maendeleo wanaotarajia kuchangia Bajeti ya Serikali jumla ya shilingi bilioni 3,971.1 kwa mwaka 2017/2018 kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Benki ya Maendeleo ya Afrika (shilingi bilioni 410.9), Abu Dhabi/OPEC (shilingi bilioni 20), AFD ya Ufaransa (shilingi bilioni 27.3), BADEA (shilingi bilioni 10), Ubelgiji (shilingi bilioni 13.7), Denmark (shilingi bilioni 47), DFID (shilingi bilioni 364.4), Jumuiya ya Ulaya (shilingi bilioni 150.3), Finland (shilingi bilioni 25.7), Ujerumani (shilingi bilioni 58.4), Global Fund (shilingi bilioni 431.2), IFAD (shilingi bilioni 45.3), India (shilingi bilioni 80), Ireland (shilingi bilioni 18.3), JICA/Japan (shilingi bilioni 57.4), Mfuko wa Maendeleo wa Kuwait (shilingi bilioni 20), Norway (shilingi bilioni 22.3), OPEC Fund (shilingi bilioni 8.5), Poland (shilingi bilioni 61.1), Sweden (shilingi

bilioni 172.5), Korea ya Kusini (shilingi bilioni 20), Uswisi (shilingi bilioni 12.1), *UNICEF* (shilingi bilioni 27.2), *USAID* (shilingi bilioni 3.4) na Benki ya Dunia (shilingi bilioni 1,862.3).

Mheshimiwa Spika, fedha zilizoingizwa kwenye Bajeti hii zinazingatia historia ya utoaji wa fedha za kugharamia miradi kutoka kwa Wahisani wetu wa Maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutambua uhusiano mzuri tulionao na Shirika la Fedha la Kimataifa (*IMF*) chini ya Mpango wa Ushauri wa Kiseru (*Policy Support Instrument*). Ni matumaini yetu kuwa Bodi ya Shirika la Fedha Duniani itakubali kuendeleza awamu nyingine ya *PSI* baada ya mwezi Desemba, 2017.

Mheshimiwa Spika, rai yangu kwa marafiki wote wa nchi yetu ni kuwa, endeeleni kuiunga mkono Serikali ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, hususan katika azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda. Watanzania wamesikia kiasi cha fedha mlizowaahidi, naomba mtimize ahadi zenu kwa wakati, nasi tunaahidi kutumia michango yenu adhimu kwa ufanisi na uwazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nihitimishe kwa kumshukuru kwa namna ya pekee kabisa, mke wangu na rafiki yangu mpenzi, mama Mbonimpaye Mpango pamoja na watoto na wajukuu wetu kwa kunitunza na kuniombea kwa Mungu kila siku ili niweze kutekeleza vema dhamana niliyopewa ya kuwatumikia Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, kwa heshima kubwa, nawashukuru sana ndugu zangu, wana wa Wilaya ya Buhigwe na wananchi wa Mkoa wa Kigoma kwa ujumla kwa upendo na kunitakia heri ili niendeele kutekeleza wajibu wangu ipasavyo. *(Kicheko/Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Wabunge waliongea bila mpangilio)*



**WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Spika, walinilea na kunifundisha kupenda kufanya kazi, nami nawaahidi kuwa nitakuwa mwaminifu, sitawaangusha.

Ahsanteni sana Waheshimiwa Wabunge, viongozi na wananchi wote kwa kunisikiliza. Mungu ibariki Tanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi/Vigelegele)*

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono karibu na Bunge zima. Waheshimiwa Wabunge, haijapata kutokea. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Hii ndiyo Bajeti ya pili ya Serikali ya Awamu ya Tano ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli. Kilichosomwa na Mheshimiwa Waziri ni Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.

Waheshimiwa Wabunge, vitabu vyote mnavyo, mwendelee kuvisoma, kuanzia Jumatatu tutaanza na Mwenyekiti wa Bajeti, Kambi Rasmi ya Upinzani watatoa mawazo yao na Waheshimiwa Wabunge tutaanza kuichakata bajeti hii kwa kujadili. Kwa kweli hapajawahi kuwa, kwa miaka mingi na bajeti nzuri kama hii. Kwa mwendo huu, 2020 *it's a walkover*. *(Makofi/Kicheko/Vigelegele)*

Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, tunawashukuru sana wasaidizi wako, Naibu Waziri na wengine wote kwa kazi kubwa mliyofanya. Kwa kweli tumekusikia na hata wananchi wa Buhigwe wamekusikia. *(Kicheko/Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu ya muda, kwenye *gallery* ya kushoto kwangu wapo wageni ambao ni Makatibu Wakuu wa Wizara zetu mbalimbali, Watendaji wa Wizara ndani ya Wizara ya Fedha na Mipango, Wakuu wa Mashirika wako kule na Watendaji wengine ndani ya Serikali. *(Makofi)*

Pia tuna Viongozi wa Dini na Wawakilishi waliotoka katika Mkoa wa Dodoma pamoja na wazee wetu wa Mkoa wa Dodoma wanawakilishwa pale. *(Makofi)*

Pia mkono wangu wa kulia kwenye *gallery* ile tunao wageni wakiongozwa na Bi. Mary Kawar ambao ni wageni wetu kutoka Umoja wa Mataifa na mashirika yake, tunao pale katika *gallery* ile ya kulia. *(Makofi)*

Vile vile tunao wageni ambao tuliwatambulisha asubuhi, Washirika wetu wa Maendeleo (*Development Partners*) wakiongozwa na Ndugu Roeland va De Geer. Karibuni sana. *(Makofi)*

Tunao Waheshimiwa Mabalizi kutoka nchi mbalimbali, niwataje walivyo; tuna Balozi wa Afrika Kusini, yupo nasi jioni ya leo Dennis Mseleku, Balozi wa Uingereza – Sarah Cooke, Balozi wa Zambia – Judith Kapijimpanga, Balozi wa Syria - Abdulmonem Annan, Balozi wa Uswizi – Florence Mattli, Balozi wa *Sweden* – Katarina Rangnitt, Balozi mdogo wa Sudan – Abuzeid Ahmed, Balozi wa Norway – Anne Kaftan, Balozi wa Namibia – Theresia Samaria, Balozi wa Msumbiji, majirani – Monica Mussa, Balozi wa Malawi – Hawa Ndilowe, Balozi wa *Finland* – Pekka Hukka, Balozi wa *DRC* – Jean Mutamba na Balozi wa Ubelgiji nchini, Paul Cartier. *(Makofi)*

Pia tuna viongozi na Watendaji Waandamizi wa Mkoa wa Dodoma ambao wote nawakaribisha sana wenyeji wetu. Tuna familia ya Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mpango, mama watoto yupo, watoto wa Mheshimiwa wapo na mjukuu Catherine Mpango yupo. *(Makofi)*

Vile vile tunaye Kaimu Mkuu wa Mabalazi nchini Tanzania ambaye ni Balozi wa Zimbabwe nchini ambaye ni Meja Jenerali Edzai Absolom Chimonyo. *(Makofi)*

Pia tunaye Balozi wa Morocco nchini, Abdelilah Benryane. Karibu sana. *(Makofi)*

Tunao Watendaji Wakuu wa Serikali akiwemo Gavana wa Benki Kuu, Profesa Benno Ndullu, tunaye CAG – Profesa Mussa Assad, Katibu Mkuu wa Fedha na Mipango – Ndugu Doto James na Kaimu Katibu Mtendaji, Tume ya Mipango – Ndugu Maduka Kessy. *(Makofi)*

Nikirudi kwenye *Gallery* ya Spika, tuna wageni ambao ni wageni wangu, Dkt. Heri Goroka ambaye ni daktari wetu kule India, ambaye pia ni mwambata wa afya kule India.

Kwa Waheshimiwa Wabunge wengi ambao mmewahi kufika huko, huyo ndio amekuwa akituhudumia kwa kila hali. Dkt. Goroka yuko wapi, hebu simama bwana. Karibu sana Mjengoni. *(Kicheko/Makofi)*

Waziri wa Afya, tunapenda kutambua kazi nzuri inayofanywa na Dkt. Goroka pale *New Delhi*. *(Makofi)*

Pia tuna wageni ambao kama nilivyosema ni wangu; Mkurugenzi wa Halmashauri ya Kongwa, Ngusa Izengo, Katibu wa CCM Wilaya ya Kongwa – Mfaume Kiziga, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa – White Zuberi, Mkuu wa Wilaya ya Kongwa – Deogratius Ndejemi, Kaimu Mkuu wa Chuo cha *Saint John* – Profesa Emmanuel Mbennah na mke wake Mama Ruth Mbennah. *(Makofi)*

Wageni wengine walioko katika Jukwaa la Spika ni Mheshimiwa Balozi John Kijazi – Katibu Mkuu Kiongozi, lakini pia tunaye mgeni maalum kabisa kwenye Jukwaa la Spika naye sio mwingine bali ni Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi, Abdulrahman Kinana. Karibu sana Katibu Mkuu. *(Makofi/ Vigelegele)*

Tunao pia Viongozi Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama kama ifuatavyo:-

Tunaye Mnadhimu Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama anayemwakilisha Mkuu wa Majeshi Nchini, Luteni Jenerali James Mwakibolwa; karibu sana. Tunaye Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa, Dkt. Modestus Kapilimba; lakini pia kuna mgeni maalum amefika hapa kwa mara ya kwanza kwa wadhifa wake, sio mwingine bali ni Inspekta Jenerali wa Polisi, Simon Sirro. *(Makofi)*

Tunaye Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa, Meja Jenerali Michael Isamuhyo; tunaye Kamishna Jenerali wa Magereza, Dkt. Juma Malewa; Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Thobias Andengeny; Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dkt. Anna Makakala. Tunaye Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Valentino Mlowola na Mratibu wa Baraza la Usalama wa Taifa, Brigedia Jenerali Martin Busungu. *(Makofi/Vigelele)*

Pia tunaye Mwenyekiti wa Baraza la Vyama, Mheshimiwa Shibuda John Magale. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kama tulivyotangaziana hapo kabla, nafurahi kuwajulisha kwamba Mheshimiwa Waziri Mkuu anawaalika katika futari mara tu baada ya kikao hiki kufungwa, ambayo itafanyika hapo nyuma katika Jengo la Utawala katika viwanja vyetu vya Bunge.

Katika futari hii tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge wote, Watumishi wa Bunge wote na wageni wote ambao mpo katika *galleries* mjiunge nasi kwenye futari hiyo. *(Makofi)*

Kwa ajili ya wageni wetu na hasa Mabalazi kutoka nje, *I am honored to inform you that The Prime Minister of The United Republic of Tanzania, Honorable Kassim Majaliwa (Member of Parliament) cordially invites all Heads of Diplomatic Missions and Representatives of International Organisations here present to join all Members of Parliament*

*and other dignitaries at iftar immediately after this Budget presentation at Parliament grounds behind there and Protocol Officers will lead the way for you. (Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, katika kumalizia, nafahamu kuna mashindano yanaendelea ya mpira ya *Sportpesa*. Nafurahi kuwaambia kwamba mpaka jioni hii ilipofika Yanga ilikuwa imefunga *AFC Leopards* magoli mawili, lakini na Yanga nayo imefunga na *AFC Leopards* magoli manne. Tunawapongeza Wanayanga. *(Makofi/ Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua tuliyoifikia jioni ya leo, tumemaliza shughuli zote hapa Mezani. Kama nilivyosema, kesho ni siku ya kupitia makabrasha yetu na vitabu mbalimbali ambavyo tumepewa na Wizara ya Fedha na Mipango na kwa hiyo basi, Jumamosi na Jumapili ni hivyo hivyo, tutakutana hapa siku ya Jumatatu.

Kwa jinsi hiyo, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi Jumatatu, tarehe 12 Juni, saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 12.22 Jioni Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu, Tarehe 12 Juni, 2017 Saa Tatu Asubuhi)*